# DHANA YA UCHIMUZI KATIKA UENDELEZAJI WA RIWAYA YA KIMAJARIBIO YA *MAFAMBA*

NA:

FERINDA KIENDE MUGWIKA

IDARA YA ISIMU NA LUGHA,

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (MA) KATIKA KISWAHILI

@ 2012

University of NAIROBI Library
0532798 6

# IKIRARI

**TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJAWAHI KUTOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE CHOCHOTE**

______________________ 26/10/2012

**FERINDA KIENDE MUGWIKA** **TAREHE**

**(Mtahiniwa)**

**Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na chuo kikuu:**

______________________ 02/11/2012

**DKT. OMBOGA ZAJA** **TAREHE**

______________________ 05/11/2012

**DKT. SWALEH AMIRI** **TAREHE**

## SHUKRANI

Kukamilika kwa tasnifu hii kumetokana na juhudi za watu kadhaa ambao walichangia katika kuifaikisha. Ninatoa shukrani zangu za pekee kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siha njema na kunipa uwezo na nguvu za kuikamilisha kazi hii.

Kisha shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Omboga Zaja na Dkt. Swaleh Amiri kwa kuniongoza na kunielekeza ipasavyo. Ujuzi wenu, mapendekezo yenu ya kitaalamu yalinijenga na kunichochea katika kunipa mwelekeo ufaao na yamekuwa mchango mwema katika kuifanya kazi hii jinsi ilivyo. Dkt Zaja, asante sana kwa ushauri na mafunzo yote uliyoyatoa, nakushukuru pia kwa misingi mwafaka uliyoijenga kwangu katika somo la tafsiri, ilinijenga na imenifaa pakubwa katika kuifanya kazi hii. Asante Dkt. Swaleh, kama msimamizi wangu, nimepata kujifunza upya mambo ambayo nilikuwa nimefunzwa au kuyajua vingine. Licha ya udhaifu mwingi niliokuwa nao mwanzoni mwa kazi hii, mlijizatiti kunikosoa na kunielekeza. ASANTENI SANA

Pia, nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi waliopata kunifunza. Kweli mchango wenu katika usomi wangu ni wa dhati na hauwezi kupuuzwa kwani mihadhara yenu ilinitia changamoto za kuwa msomi shupavu katika uwanja huu. Hawa ni Dkt. Buregeya, Dkt. Mbatiah, Dkt. Zaja, Dkt. Ayub Mukhwana, Bw. B.G. Mungania, Dkt. Olali, Dkt. Kineene wa Mutiso, Prof. Abdulaziz, Prof. Kithaka wa Mberia na Prof. Habwe.

Vilevile, nawashukuru wenzangu ambao tulizama nao pamoja katika merikebu hii ya kiakademia, kiwango cha uzamili. Hawa ni Bw. Kiongera Kiarie Bw. Amolo Shadrack, Bi. Jackline Kinya Munene, Bi. Pauline Wangechi Kimani, Bi. Beatrice Mwenderani, Binti.

Zipporah Nyaboke na Binti. Everlyne Were. Changamoto zilikuwa nyingi, hasa tulipohisi kuwa mambo ni magumu lakini kwa uwezo wa Mola, bidii yetu kupitia kwa mijadala kadha tuliyoshiriki pamoja, ushirikiano tuliokuwa nao katika usomi na utafiti, tumeweza kutia nanga merikebu yetu na kuzama vilivyo.

Ninatoa shukrani za dhati kwa babangu Samuel Mugwika Ibutu na mamangu Isabella Karambu Mugwika kwa kunipa fursa ya kusoma hadi kiwango hichi. Nashukuru pia kwa juhudi zenu zote zilizoniwezesha kukamilisha shahada hii bila taswishi, kugharamia karo, pesa za matumizi ya kibinafsi na za kununua vitabu nilivyohitaji. Hali kadhalika, nawashukuru kwa kuninunulia tarakilishi iliyoniwezesha kupiga chapa kazi yangu, kusema kweli ingekuwa kazi ngumu kuiandika hii tasnifu. Asanteni kwa kinirahisishia kazi. Asanteni sana kwa ufahamu wenu kuhusiana na umuhimu wa masomo. Ni mengi mazuri mmejinyima ili kutuwezesha mimi na dadazangu Lorraine Nkirote, Elsy Kanyiri, Mildred Karimi na kakangu Ronald Kimathi kufikia viwango vya kielimu ambavyo tumevifikia. Kanyi, usiione safari ikiwa ndefu, jikaze kwa kutia bidii ya mchwa masomoni na Mungu atakuongoza. Nkii na Kim, msilegee, kumbukeni ‘Elimu ni Nguvu’ kwa imani Mungu atujalie mema zaidi. Shukrani kwa mapenzi yenu na kwa kunitia moyo kuwa yote yanawezekana. ASANTENI SANA NA MUNGU AWABARIKI

Shukrani zangu pia ziwaendee: Binamu yangu Makena, shangazi Doris Kanoti na Nyanyangu mpendwa Karuguru Mungania pamoja na familia yako. Doris,wema wako, ukarimu na juhudi zako za kunihimiza nijikaze kamwe sitazisahau. Nyanya, asante kwa mawaidha yako na ukarimu wako na kwa kunitia moyo wa kusoma. Nawashukuru nyote.

Hali kadhalika nawashukuru marafiki zangu walionitia moyo katika kipindi kigumu cha utafiti. Hawa ni Robert Maingi, Elly Nyaga, Patrick Okombo, Sylvia Mafuta, Cate Kamau na Judy

Mwangi. Patrick, asante sana kwa mawaidha yako kuhusiana na utafiti huu na vitabu vyako ulivyonipa, vilinifaa sana katika kuikamilisha tasnifu hii. Mungu awabariki

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapendwa:

**Samuel Mugwika Ibutu na Isabella Karambu Mugwika**

Kwa kunilea, kunielimisha na kunishauri vyema. Baraka za Mungu ziwe nanyi milele daima, Amen.

**ORODHA YA YALIYOMO** **UKURASA**

Ikirari....................................................................................................i
Shukrani..................................................................................................ii
Tabaruku..................................................................................................v
Orodha ya yaliyomo...................................................................................vi
Vifupisho vya maneno..................................................................................x
Ikisiri......................................................................................................xi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.1 usuli wa mada.......................................................................................1
1.2 Tatizo la utafiti......................................................................................9
1.3 Madhumuni ya utafiti.............................................................................10
1.4 Nadharia tete........................................................................................11
1.5 Sababu za kuchagua mada.......................................................................11
1.6 Upeo na mipaka....................................................................................13
1.7 Misingi ya nadharia................................................................................14
1.7.1 Kanuni kuu za Wana-Urasimu.................................................................19
1.7.1.1 Mtalaa wa kisayansi............................................................................19
1.7.1.2 Ostraneniya au uajinabishaji.................................................................24
1.7.1.3 Dhana ya fibula na szujet.....................................................................27
1.7.1.4 Matumizi ya lugha...............................................................................28
1.7.1.5 Mbinu za uwasilishaji...........................................................................29
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada. ..................................................................31
1.9 Njia za utafiti........................................................................................37
1.10 Tanbihi.............................................................................................39

**SURA YA PILI:**

**USUKAJI WA RIWAYA YA *MAFAMBA***

2.0 Utangulizi.............................................................................................40
2.1 Usukaji wa riwaya ya *Mafamba*...............................................................40
2.2 Hitimisho..............................................................................................53

## SURA YA TATU:

## UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA WAHUSIKA


3.0 Utangulizi....54

3.1 Wahusika wakuu....55

3.1.1 Maotad....56

3.1.2 LiMioe....62

3.1.3 Amrao....66

3.1.4 U....69

3.1.5 Wakazi wa Bikerani- Msiige....73

3.1.6 Mzee Twajua....79

3.2 Wahusika wadogo....83

3.2.1 Boyi....83

3.2.2 Damisi....84

3.2.3 Fadhila....85

3.2.4 Avadi....86

3.2.5 Askari wa Maotad....88

3.2.6 Nuhu....89

3.2.7 Shanata....90

3.2.8 Nikiabi....91

3.2.9 Ngwena....92

3.2.10 Arijojo....93

3.2.11 Saigeo....94

3.2.12 Mastanji....95

3.2.13 Rojoo....97

3.2.14 Bwana $O_2$....97

3.2.15 Bwana Paka....98

3.2.16 Engineer....98

3.2.17 Jogi....101

3.2.18 Madaktari wa Biande na Bae....102

3.2.19 Kasisi Mumu....103

3.2.20 Kamu....103

3.2.21 Kanga........103
3.2.22 Kanje........104
3.2.23 Wanabiashara katika soko la Tuga Amor........104
3.2.24 Hitimisho........105

**SURA YA NNE**

**UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA MATUMIZI YA LUGHA**

4.0 Utangulizi........107
4.1 Uchimuzi katika kiwango cha kisintaksia........107
4.1.1 Uchimuzi katika kiwango cha kimsamiati........107
4.1.1.1 Maneno ya Kingereza........107
4.1.1.2 Maneno ya Dholuo........109
4.1.1.3 Kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi........111
4.1.1.4 Maneno ya kale........115
4.1.1.5 Maneno ya kubuni........116
4.1.1.6 Maneno mageni........116
4.1.2.0 Uchimuzi katika kiwango cha muundo........118
4.1.2.1 Urudiaji........118
4.1.2.2 Urefu wa sentensi........120
4.1.2.3 Usambamba........121
4.1.2.4 Maswali ya balagha........123
4.2.0 Uchimuzi katika kiwango cha kisemantiki........127
4.2.1 Uhaishaji........127
4.2.2 Uhalisiaajabu........132
4.2.2.1 Kifungua kinywa cha kundi la BORA........133
4.2.2.2 Utabibu........134
4.2.2.3 Lugha katika sayari ya mbalimbali........134
4.2.3 Taswira........135
4.2.4 Sitiari........138
4.2.5 Matumizi ya italiki........140
4.2.6 Herufi kubwa........142
4.2.7 Kweli kinzani........144

4.2.8 Methali na misemo....145
4.2.9 Jazanda....148
4.2.10 Tashbiha....149
4.2.11 Kinaya....150
4.2.12 Chuku au udamisi....151
4.2.13 Ndoto....153
4.2.14 Nyimbo....155
4.2.15 Ukweli bunilizi....157
4.3 Hitimisho....160

**SURA YA TANO**

**HITIMISHO**

5.0 Utangulizi....162
5.1 Kuhusu madhumuni ya utafiti....162
5.2 Upimaji wa nadharia tete....164
5.3 Mapendekezo....165

**MAREJEREO**....167

## VIFUPISHO VYA MANENO VILIVYOTUMIWA

k.h.j……………………………………………………………………….. kama hapo juu

n,k……………………………………………………………………… na kadhalika

uk…………………………………………………………………………… ukurasa

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu dhana ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio au mpya ya *Mafamba* (2008). Ni riwaya ya kwanza ya Olali inayomulika hali ya kisiasa katika jamii yetu na harakati za wananchi za kuwang'oa viongozi wadhalimu. Katika kuitafiti kazi hii, tuliongozwa na mwelekeo wa kihakiki wa Urasimu wa Kirusi.

Utafiti huu unahusu nafasi ya uchimuzi katika riwaya ya *Mafamba.* Suala ambalo tumeshughulikia kwa kuangazia uchimuzi katika ngazi ya wahusika na matumizi ya lugha. Utafiti huu ulilenga kudhihirisha kuwa, uchimuzi ni nguzo kuu katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio au mpya ya *Mafamba.*

Tumeigawa tasnifu hii katika sura tano. Ili kufikia malengo yetu, sura ya kwanza imeshughulikia utangulizi kwa ujumla. Utangulizi huu unahusu usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, mipaka na upeo, misingi ya kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumezungumzia msuko wa riwaya ya *Mafamba* ambao unajenga msingi wa uelewa wa riwaya hii. Tumeiona riwaya hii kuwa ya kuvutia na kusisimua hasa kutokana na usimulizi wake unaoelezea masuala nyeti ya kisiasa ya jamii yetu katika mtindo mpya wa uandishi kwa njia inayokiuka sifa za uandishi wa riwaya za jadi.

Katika sura ya tatu tumeshughulikia uchimuzi katika kiwango cha wahusika. Uchimuzi huu unatokea katika kiwango cha maana au kisemantiki. Tumebainisha kwamba, uchimuzi wa wahusika katika riwaya ya *Mafamba* unabainika kupitia kwa usawiri wao kiasi cha kubatilisha dhana nzima ya uhusika hata ingawa matendo yao na wasifu wao unachukuana na hali ya kisasa ya maisha ya jamii yetu kwa jinsi tunapata kuwatambua, kutambua tabia zao na mielekeo yao.

Aidha kupitia kwa uchimuzi katika kiwango hiki, dhamira ya mwandishi na aidha maudhui katika riwaya hii yanabainika.

Sura ya tatu inahusu uchimuzi katika kiwango cha matumizi ya lugha. Ili kufanikisha lengo letu, tuliangazia vipengele vya matumizi ya lugha katika kiwango cha kimsamiati na kisemantiki. Utafiti wetu umebaini kuwa, viwango hivi vinachimuza sifa zilizozungumziwa na Wana-Urasimu kama uajinabishaji au kufanya kazi ya kifasihi kuonekana kuwa ngeni, matumizi ya mbinu kadha za uwasilishaji na matumizi ya kipekee ya lugha.

Sura ya tano inahusu hitimisho la utafiti. Katika sehemu hii, tumerejelea mada ya utafiti huu na maswala ya kimsingi tuliyoyaelezea katika sura ya kwanza. Kutokana na matokeo ya uchanganuzi data yetu, tumerejelea nadharia tete zetu ili kuzikubali na pia tumetoa mahitimisho na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa mada

Riwaya ya kimajaribio au "riwaya mpya" ni utunzi wa riwaya ambao unahusisha majaribio au matumizi ya sifa zinazoelezwa kama za kimajaribio, Wamitila (2008:127). Hii ina maana kuwa ni hali ya kimajaribio au mwondoko katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili kutoka mtindo uliyozoeleka. Hali hii imepelekea utunzi wa fasihi kupata mtekenyo wa mabadiliko ili kuepuka kupooza kutokana na mitindo iliyozoeleka na pia kuweza kukabiliana na mabadiliko kadhaa yanayozikumba jamii zetu za sasa. Jambo hili limewapa waandishi wa riwaya mpya fursa ya kuyaeleza mambo ambayo hayangeweza kuelezeka kwa mitindo ya kawaida. Hii ni kwa sababu utanzu huu umepitikiwa na nguvu na matukio muhimu ya kijamii, kitamaduni, kihistoria, kielimu, kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia ambayo hayawezi kuhimizika na hivyo, yamesababisha mabadiliko ya kimaudhui na kifani.

Riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili imeanza kujitokeza mwanzoni mwa miaka ya 1990, muda mfupi tu baada ya neno 'utandawazi' kuingia masikioni na kuzama akilini mwa wasomaji wa fasihi ya Kiswahili kuanzia miaka ya 1980[1]. Majaribio na mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili yalianza pale waandishi wengi wa Afrika Mashariki kama Kenya na Tanzania walipoanza kukataa kuitikia "hewalla" kwa kila walichokiona na kukisikia na aidha walipokataa kuitikia kanuni au sheria na pingamizi za ubunaji wa sanaa walizokuta zimewekwa[2]. Mwanzoni, 'njia bora' iliyotumika na waandishi katika kazi za fasihi ilikuwa ya uhalisia kwa sababu ya uwazi na unyoofu wake wa kimantiki na kwa kuwa uhalisia ulikuwa mtindo ambao ulizoeleka sio Afrika tu bali ulimwenguni kote. Mtindo huu ulikita mizizi kwa muda mrefu kwa sababu ya uwazi na

kutokuwa na changamano na kwa kuwa ulionekana kuwa njia bora iliyofichua na kuueleza umma matatizo ya kijamii na kisiasa waziwazi. Ilikuwa njia bora ya kuwasiliana na wananchi wa kawaida na hivyo, kubana uhuru wa waandishi kwa njia moja au nyingine.

Uhalisia ni mtindo wa uandishi unaozingatia uyakinifu wa maisha. Ni mbinu iliyokita mizizi katika karne ya kumi na tisa na ishirini, Wafula na Njogu (2007:61). Katika karne ya 19, huko Ulaya, mapinduzi ya kisiasa, ya kiviwanda yalikuwa yamelegea na maendeleo ya kiteknolojia kuendelezwa. Hivyo basi, wanajamii walijizatiti katika kukabiliana na matatizo yaliyohusiana na miji iliyopanuka, jambo ambalo lilipelekea kuzuka kwa makabwela. Hali hii ilisababisha haja ya kueleza hali halisi ya maisha ya binadamu na huu ukawa msingi wa uhalisia. Kwa mintarafu hii, mtindo huu ulikita mizizi katika kuelezea matatizo yaliyomkumba binadamu. Katika miaka ya hivi karibuni, mtazamo wa uhalisia umeshambuliwa kutokana na upanuzi wa kimajaribio wa kifasihi. Mathalani, kuibuka kwa sifa za kifantasia na bunilizi ya kisayansi ambazo ni sehemu za uhalisia, kumepelekea kuwepo kwa mtindo kama uhalisiaajabu. Yaani, uelezaji wa matukio ya kiajabu kwa njia inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida. Uhalisiaajabu ni mbinu inayotumika na waandishi wa riwaya mpya ili kuonyesha kuwa ingawa mambo wanayoshughulikia ni ya kiajabu hutokea katika maisha ya kawaida. Tangu kuvuma kwa upepo wa mageuzi ya kiuandishi, waandishi wamepata uhuru wa kisanaa na kifikra na dalili za uhuru huo zinadhihirika wazi katika mkondo huu wa riwaya mpya.

Riwaya ya kimajaribio kwa mujibu wa ufafanuzi wa Wamitila (2003:185), inarejelea aina ya riwaya iliyozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na inayoakisi matumizi ya mbinu ya kiubunifu na kukiuka kaida za jadi za uandishi wa riwaya. Kimsingi, katika riwaya ya kimajaribio, kunatumika mitindo mipya ya kiubunifu kama vile matumizi ya italiki katikati ya mtiririko fulani wa maelezo, mistari, dondoo, wino mzito au herufi zilizokolezwa na herufi kubwa kwa njia

zisizo za kawaida. Kwa sababu hizi, dalili za upya wa riwaya hii zimo katika usanii na maudhui yake. Kuhusiana na usanii, kuna mabadiliko mengi tena ya kushangaza na kutatiza kama vile kubuniwa kwa muundo mpya wa kifani na umbuji kwa kuzingatia mbinu inayojaribu kuasi uhalisia mkongwe na mkavu kwa makusudi. Matumizi ya mbinu za kifantasia katika viwango mbalimbali kama vya usimulizi, uhusika, mwingiliano matini wa wahusika, mwanya wa kisaikolojia ndani ya vichwa vyao, ndoto zinazoingiliana na ukweli wa mambo mbalimbali yanayohusika, matukio yenye mshikamano wa uzoevu na ugeni, mazingira na jinsi yanavyoshikana na matukio na kufungamana na mabaki ya uchawi, ushirikina na mazingaombwe, mwingiliano matini na mchezo wa lugha[3].

Kimaudhui, riwaya hii inayaangazia matatizo ya kijamii, kitaifa ama kimataifa kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko wa nje. Lengo la waandishi hawa ni kuyaweka dhahiri mambo kwa hadhira, mambo ambayo tayari yanajulikana na hadhira lengwa. Ingawa ni mambo yaliyoangaziwa na wanafasihi katika riwaya ya kimapokeo, katika riwaya hii mpya, yanaelezwa kwa msisitizo zaidi na kwa njia isiyo dhahiri, jambo ambalo linawapa waandishi nafasi ya kuelezea vituko na miujiza bila woga na aidha kukumbusha umma vitushi vinavyoathiri nchi na ulimwengu kwa jumla. Lengo lao haswa ni kuyakoleza kwa uwazi kwa hadhira na kuwaelimisha ili waweze kukabiliana nayo na kubadilisha kizazi kijacho. Mambo haya kwa uhakika, huathiri maisha yao kwa namna nyingi na huhusisha masuala kama ufisadi ambayo yanatekelezwa na wanasiasa na viongozi serikalini, uvunjaji wa sheria kutokana na ujeuri, uasherati- siku baada ya siku magazetini na katika idhaa za taifa, matangazo ya akina baba kuwanajisi watoto wao hayakosekani, wizi hata miongoni mwa walinda usalama, utandawazi umesababisha masuala tofauti yanayoathiri jamii kwa njia kadhaa kuibuka, na tamaa miongoni mwa masuala mengineyo. Haya ni mambo ambayo yamewafanya wananchi kukata tamaa, kupatwa na

maradhi, kupigwa na butwaa na kuwa na woga kutokana na jinsi maisha yanavyowaendea vibaya.

Riwaya mpya ya Kiswahili imeanza kuibuka katika miaka ya 1990, yaani mwishoni mwa karne ya ishirini kama ambavyo nimetaja hapo juu. Waandishi waliojizatiti katika uandishi huu ni kama E. Kezilahabi katika riwaya zake mbili: *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), riwaya ya E. Mbogo ya *Vipuli vya Figo* (1996), riwaya ya W. E. Mkufya *Ziraili na Zirani* (1999), riwaya za S. A. Mohamed *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia yao* (2006), riwaya za K. W. Wamitila *Bina-Adamu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) na *Mafamba* ya Tom Olali (2008) ambayo tunaihakiki.

Msukumo wetu wa kuichagua riwaya ya *Mafamba* kama riwaya ya kimajaribio umetokana na muundo wake unaodhihirisha viwango mbalimbali ambavyo vimejichimuza. Uchimuzi ni mbinu inayodokeza mambo au sifa fulani za kazi ya kifasihi kwa uwazi na kuyafanya yajitokeze waziwazi yakilinganishwa na mengine, mambo muhimu au yenye uzito husisitizwa.

Riwaya za kimajaribio za Kiswahili hudhihirisha sifa bainifu zinazozibainisha kutokana na riwaya za kihalisia. Ufafanuzi wetu utahusisha mifano kutoka riwaya ya *Nagona*, *Babu Alipofufuka* na *Mafamba.* Hata hivyo, tutataja riwaya nyinginezo ambazo sifa hizi zinabainika. Sababu ni kuwa, lengo letu ni kutathmini usuli wa mada bali sio kuhakiki riwaya zote mpya.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa Wamitila (2008:128), sifa hizi ni kwanza, upanuzi wa mwanda wa kisimulizi. Usimulizi katika riwaya hizi hauna mipaka dhahiri na huweza kuhusisha ulimwengu halisi, ulimwengu dhanifu au ulimwengu wa njozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti kuvunjwa kiasi kwamba matukio ya ulimwengu wa njozi yanafuata kanuni zilezile za matukio ya ulimwengu halisi. Hali hii hudhihirika wakati usimulizi unaachwa na riwaya au mhusika katika riwaya hujizoa kwenye tathmini ya kisaikolojia. Kwa njia hii, usimulizi unachimuzwa katika

kudhihirisha hali dhanifu na ya njozi. Sifa hii inapatikana katika riwaya za *Babu Alipofufuka, Nagona na Mafamba.*

Katika *Babu Alipofufuka*, kuna usimulizi unaohusisha ulimwengu dhanifu. Siku ya kwanza babu mzuka anapokwenda kujaribu kuzungumza na K, mwandishi anatujulisha kwamba, baina yake na K, kulikuwa na nafasi nyembamba kama unyusi. Babu hamfikii, anajaribu kumpungia mkono, kumshika kichwa hata kumpigia kelele lakini hafanikiwi hadi anapolazimika kupitia kwa dereva wake Mzula (2008:1). Pia katika *Nagona*, ukurasa wa kwanza, usimulizi wa aina hii unajitokeza. Kutokana na jinsi hadithi inavyoanza, ni kama msimulizi haelewi hali halisi ilivyo, mawazo yake yanaonekana kuwa ya kidhahania, ni kama mtu aliyekuwa katika ndoto. Usimulizi unaanza hivi;

> Yaelekea ilikuwa jioni, maana kulikuwa na mwanga hafifu wa ki-dhahabu humo bondeni nilimokuwa. Sikumbuki kuona jua na sikumbuki kuona mtu mwingine karibu nami...kama huo ndio ulikuwa mwanzo wa safari yangu, sina hakika. Lakini nilijikuta nimechoka.

Usimulizi katika *Mafamba* unahusisha maingiliano kati ya ulimwengu halisi na ulimwengu dhanifu. Ulimwengu halisi unajitokeza kwa mfano katika ukurasa wa kwanza. Hadithi inaanza kwa kutaja wakati halisi katika dira ya saa.

> Asubuhi Bikerani-Msiige...

Hali dhanifu inajitokeza mathalani katika ukurasa wa saba ambapo mtunzi anatuonyesha kuwa vyama katika jamii zetu vimeibuka kwa kuumbwa.

> NUKA ilikuwa sayari ya zamani sana. Muumba alipoiumba KARIFA, sayari ya NUKA iliumbwa yapata miaka 4000 iliyopita. Sayari nyingi ziliundwa kama vile NUZAPIFU, NUTA na ELIMO-FR.

Pili, ni ushikamano wa vitu visivyo vya kawaida hivi kwamba mbinu zinafungamanishwa na kuhusishwa na nyanja mbalimbali na utunzi wa riwaya. Kutokana na sifa hii, kuna matumizi ya mbinu za sanaa ya uchoraji au picha au matumizi ya mbinu za filamu. Katika *Mafamba*, taswira ya mambo au matukio mbalimbali ni picha halisi ya usawiri wavyo kulingana na ufahamu wetu. Mtunzi, katika ukurasa wa kwanza anatuchorea picha halisi ya mtaa wa Bikerani-Msiige ambapo kuna vyumba vya madongoporomoka vilivyoelekezana milango ya mabati na vilivyopeana migongo kuhimizana, milango ya vyoo ni magunia matupu ya sukari.

Sifa nyingine ni uchanganuzi wa unga'muzi bwete ambapo kuna uhusishaji wa ungamuzi bwete na mhusika wa riwaya anayetawala. Istilahi hii kulingana na Wamitila (2003:298) inarejelea matumizi ya akili ya binadamu ambayo huhodhi fikra, mawazo, hofu, na mitazamo hasi ambayo haiwezi kukubalika na jamii. Hofu na mawazo hayo hujitokeza katika ndoto. Sifa hii inajitokeza katika riwaya za *Bina- Adamu!*, *Mafamba* na hata *Musaleo*. Mhusika Maotad katika *Mafamba,* anatawaliwa na mawazo hasi ya kukataa kung'atuka mamlakani kutokana na kupenda mafamba. Ndoto ya kijinamizi inayomjia mara kwa mara inadhihirisha hofu yake ya kunyanganywa mamlaka. Mafamba ni istilahi inayomaanisha mambo yafanywayo pasi na uadilifu kama kwa njia ya rushwa na ufisadi, Kamusi ya karne ya 21 (2011: 275).

Mkabala mpya wa dhana ya wakati ni sifa nyingine ya riwaya hizi. Mpaka wa jadi baina ya nyakati unavunjwa kiasi kwamba matukio yanaacha kuzingatia kanuni za uhalisi wa kiwakati. Dhana hii huhusishwa na ndoto na inadhihirika katika riwaya za *Ziraili na Zirani, Nagona, Mzingile, Mafamba* na *Babu Alipofufuka*. Mathalani katika *Babu Alipofufuka*, wakati K na Babu wanapofika shamba kwa kina K, K anahisi kwamba wamechukua miaka elfu moja ilhali safari imekuwa fupi sana. Wanapokuwa kwao, K anataka kujua huo ni mwaka gani na Mzuka anamjibu kwamba inaweza kuwa 1800 au 2100. Mzuka anamwambia kuwa ikiwa ni mwaka wa

1800 au 2100 ni sawa baina ya kwenda mbele na nyuma (2008:94). Hivi kwamba, ikiwa miaka 1800 imepita, basi itakuja tena na kama miaka 2100 haijafika, picha halisi ya itakavyokuwa imeanza kuonyesha. Katika hali halisi, Mzuka alinuia kumbainishia K ambaye ni mfano wa viongozi barani Afrika kuwa, heshima ya mwafrika iliyoondolewa na wakoloni kutokea enzi hizo, leo hii inaondoshwa na mwafrika mwenyewe kwa wenzake na kuwa kesho mwafrika pekee ndiye atakayebakia bila heshima ulimwenguni.

Mwisho, ni mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia. Matumizi ya ndoto, usawiri wa wahusika kuegemea kwenye visasili, kuwepo kwa visasili au mmuliko mkubwa kwenye msukumo wa kisaikolojia. Mbinu hizi husababisha kuwepo kwa mipaka kati ya yanayowezekana na yasiyowezekana. Riwaya zenye sifa hii ni kama *Musaleo!, Bina- Adamu!, Babu Alipofufuka, Mafamba* na *Nagona.* Katika *Nagona*, binadamu anasawiriwa kama kiumbe katika mji fulani ambaye amevichoma vitabu vyote, hana njia ya usemi, na ambaye anaishi katika ulimwengu wa ndoto zisizoisha. 'Mimi' anakutanishwa na wanafilosofia kadha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia kama Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Nietzsche, na Freud ambao walikufa miaka iliyopita wakiwa katika duara wakijadiliana na roho zao, mwandishi anafanya hivi kuwakumbusha wanadamu umuhimu wa kujitakasa. Hii ni kama ndoto, ni mambo yasiyowezekana katika hali halisi. Lengo la mtunzi ni kudhihirisha kwamba, kuna hukumu baada ya maisha yetu duniani.

Katika *Babu Alipofufuka*, ndoto na uhalisia vimechanganyika. Huu ni utamaduni ambao huchota baadhi ya vipengele vya maisha kabla ya ukoloni, sehemu ndogo ya urithi wa kikoloni pamoja na tamaduni za kuupinga ukoloni, (Wamitila 2002:169). K anapokuwa mdogo, anaota ndoto ya kumiliki na kuendeshwa kwenye gari linalokwenda pasi na kusikika mlio, gari linalomfanya mtu ajihisi hayupo katika dunia hii. Na huyu hapa leo, ndiye yeye K, ndoto si ndoto tena (2008:18).

Mwandishi anatuonyesha kuwa ndoto ya ukubwa aliyokuwa akiota K hivi sasa ni halisi, si ndoto tena. Ingawa hivyo, tukiangazia maisha anayoishi K kwa undani hasa anapoimiliki *limonsin*, ofisi, wafanyakazi chungu nzima, kasri kubwa na makubwa anayopitia akiwa kiongozi ni kama anaishi katika ndoto na wala sio uhalisi.

Katika *Mafamba*, wahusika wana msukumo wa kisaikolojia, mhusika Maotad kwa mfano anasumbuka ndani kwa ndani kutokana na tamaa ya uongozi, hataki kung'atuka mamlakani. Wengine kama Amrao wanajizatiti kuungana hata na Maotad ili aghalabu wapate kukikalia kiti cha "enzi". Kutokana na ufafanuzi huu ni wazi kuwa riwaya ya *Mafamba* inaafiki sifa bainifu za riwaya mpya.

Riwaya ya *Mafamba* (2008) inaangazia hali ya utawala nchini Kenya hasa katika kipindi cha mwisho cha utawala wa Maotad pamoja na harakati zote za kumtimua uongozini kama kinara wa NUKA na mtawala mbaya aliyeongoza kwa takriban miaka 400. Mwandishi anasimulia uozo katika sayari ya NUKA chini ya uongozi wa Maotad. Yeye na viongozi wengine wanaoabudu mafamba wanajihusisha katika nyendo chafu ambazo zinakashifiwa na viongozi wa sayari za upinzani kama Amrao na LiMioe miongoni mwa wengine. Hata baada ya Maotad kutimuliwa uongozini na wanasayari ya BORA, mtunzi anadhihirisha uozo na tamaa ya viongozi nchini. Wao, baada ya kubadilisha hali mbaya ya nchi iliyozuliwa na wafuasi wa NUKA, wanaisambaratisha zaidi. Wanasahau kutimiza matakwa ya wananchi waliowachagua na kuyapa kipaumbele masuala yaliyowavutia sana ya kujigawia mamlaka na vyeo. Hatima yake inakuwa kugawika kwa muungano wa BORA na uongozi wa vuta nikuvute.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Suala la utafiti tunaloshughulikia katika utafiti huu ni matumizi ya uchimuzi katika riwaya mpya ya Kiswahili. Licha ya kuwa riwaya mpya inajitambulisha kutokana na sifa nyingi, uchimuzi unajitokeza kama sifa inayopewa kipaumbele zaidi kuliko sifa hizo nyinginezo kwani ndio mhimili mkuu wa dhamira katika riwaya ya *Mafamba.*

Dhana ya uchimuzi haijashughulikiwa na wataalamu hasa katika riwaya mpya ya Kiswahili na kwa sababu hii, msukumo wetu ni kupiga hatua mbele ili kuishughulikia katika riwaya mpya ya *Mafamba*. Japo kuna tafiti kuhusu dhana ya uchimuzi mathalani wa Kadenge Kazungu (1982) aliyehakiki ukiushi na uchimuzi katika riwaya ya *Asali Chungu* ya Said, A. Mohamed, shairi la *Swifa ya Nguvumali* la Hassan bin Ali na tamthilia ya *Wakati Ukuta* ya Ebrahim Hussein, motisha yetu ni kuonyesha uchimuzi katika riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili kwa kuiangazia katika riwaya nzima. Sababu ni kuwa, riwaya inahusisha mpangilio au muundo wa elementi au sifa za kimsingi kama msuko, usimulizi, usababishi, wakati na migogoro.

Riwaya ya *Mafamba* imedhihirisha uchimuzi katika viwango kadhaa. Mathalani, katika kiwango cha wahusika, wasomaji wanawatambua wahusika kwa tabia na majina yao halisi katika michakato ya jamii ya kisiasa. Hawa ni binadamu waliopatikana (kwa kuwa waliishi) na wanaopatikana katika miji, makabila ya hapa nchini na aidha, tunaowasikia na kuwaona katika runinga nchini Kenya. Hata hivyo, kwa kuwa si sifa zote za muundo wa kazi ya kifasihi ambazo huweza kuchimuzwa, kwa kuwa uchimuzi huhusu kufanya sifa fulani zijitokeze wazi zaidi au zibainike zinapoangaziwa kwa usambamba na usuli wa sifa husika, tulionelea tuhakiki riwaya hii na tubainishe uchimuzi katika viwango vya wahusika na matumizi ya lugha.

Riwaya ya *Mafamba* inavuta nadhari ya msomaji kwa kuwa masuala ibuka yanahusu siasa katika jamii zetu na wanasiasa mbalimbali ambao wamehusishwa nazo miongoni mwa sakata kadhaa zilizoibuka nchini wakati wa utawala wa Maotad na mwisho wa kipindi cha utawala wake na aidha kipindi cha kwanza cha utawala wa LiMioe. Riwaya hii inampa mtafiti yeyote hamu ya kuyachanganua masuala kama ufisadi, utawala mbaya, tamaa, umaskini na ubinafsi yanayowasilishwa kwa kutumia mbinu tofauti. Lengo letu ni kuchunguza namna yanavyojitokeza katika kazi hii tofauti na yanavyodhihirika katika jamii tunamoishi. Aidha, ni muhimu kuwapa mwangaza wasomaji ambao hawakupata kuyaelewa haya wakati yalitendeka kwa kuwafungua macho na hasa wanapowachagua viongozi wapya nchini.

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

Dhamira ya utafiti huu ni kuonyesha nafasi ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio au riwaya mpya ya Kiswahili kama itakavyodhihirishwa katika riwaya ya *Mafamba.* Tutafanya hivi kwa kushikilia kwamba uchimuzi ni kigezo cha kimsingi katika uendelezaji wa mambo mengi katika riwaya ya kimajaribio, hii ikiwa ni pamoja na usawiri na uendelezaji wa wahusika, maudhui, mandhari, matukio na mitagusano ya aina nyingi. Uchimuzi huu mara nyingi unajibainisha katika misingi ya matumizi lugha na usimulizi.

Aidha tunalenga kuhakiki *Mafamba* kama riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili. Mwelekeo huu utatusaidia kubainisha tofauti iliyopo kati ya riwaya hii na za jadi katika uwasilishaji wa msuko, usimulizi na matumizi ya lugha.

Tunadhamiria kuonyesha kuwa utanzu wa riwaya ya Kiswahili unakua kila uchao na hivyo kuthibitisha madai ya Mlacha (1991:7) kuwa historia ya riwaya ya Kiswahili imepitia hatua tofauti na kukua kiasi kwamba, umaarufu wake umezidi ule wa tanzu nyingine kwa kiwango

kikubwa, yaani jinsi jamii inavyoendelea kubadilika kupitia mabadiliko tangu enzi za ukoloni, baada ya uhuru, enzi ya utawala mpya wa Kiafrika hadi sasa, ndivyo waandishi wa riwaya wanavyoendelea kuyasawiri matukio haya. Kwa njia hii, kumeibuka mitindo mipya inayohusishwa na riwaya ili kuyajadili masuala yanayosibu jamii na ujirani wetu ambayo hayawezi kuwasilishwa kwa njia ya kawaida, njia iliyohusisha utungaji wa fasihi kutokana na mazingira aliyopatikana mwanadamu kwa kutumia lugha rahisi iliyoeleweka bila shida yoyote.

Hali kadhalika, tunakusudia kuchunguza iwapo riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* ambayo ni ya kwanza ya Tom Olali inaafiki sifa za riwaya ya kimajaribio kama ndoto zinazoingiliana na ukweli wa mambo mbalimbali, mwingiliano wa matini na mchezo wa lugha, upya katika usanii na maudhui, miundo mipya inayojaribu kuasi kwa makusudi, uhalisia unaohusishwa na riwaya ya kawaida.

## 1.4 Nadharia tete

Utafiti wetu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

(i). Dhana ya uchimuzi imechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya ya *Mafamba.*

(ii). Dhana ya uchimuzi ndiyo mhimili mkuu wa dhamira katika uendelezaji wa riwaya ya *Mafamba.*

(iii). *Mafamba* ni riwaya inayoweza kuhakikiwa kama riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili mbali na kuwa inaweza kuhakikiwa kwa njia nyinginezo.

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Tumechagua mada hii kwa sababu kadha wa kadha. Kwanza, hakuna tafiti tunazozijua za kiuhakiki wa kitaaluma kuhusiana na riwaya mpya ya Kiswahili ya *Mafamba* (2008). Kazi

tuliyodurusu ya Olali (2010) ilihusu muundo na dhidi-muundo (anti-structure) katika riwaya mpya ya *Babu Alipofufuka* ya Mohamed (2001). Katika kazi hii, alibainisha muundo wa riwaya hii kimtindo. Kwa hivyo, tunatarajia kuchanganua *Mafamba* kwa kina huku tukimulika vipengele mbalimbali vinavyoibainisha kama riwaya mpya.

Pili, dhana ya uchimuzi katika riwaya hii haijawahi kushughulikiwa na haina tafiti nyingi na hivyo motisha wetu ni kuihakiki kazi hii na kujenga ufahamu wa awali. Hivyo tuliona haja kubwa ya kuhakiki *Mafamba* ili kubainisha ilivyochimuza katika viwango mbalimbali huku tukiongozwa na mwelekeo wa Urasimu. Sababu ni kuwa, kazi tuliyokumbana nayo ya Kazungu Kadenge (1982), ilihusu dhana ya ukiushi na uchimuzi katika riwaya ya *Asali Chungu* ya Mohammed, S. A, shairi la *Swifa ya Nguvumali* la Hassan bin Ismael na tamthilia ya *Wakati Ukuta* ya Ebrahim Hussein. Alibainisha kwamba, ingawa dhana hizi zina mipaka isiyo dhahiri, zinaweza kuchunguzwa bila kuhusishwa. Aidha, alifafanua kuwa, dhana hizi huwaathiri wasomaji wa kazi za kifasihi na kuwafanya wazielewe. Utafiti wake uliongozwa na mtindo wa kiuhakiki wa matini wa Leech (1969:37).

Hali kadhalika, tunalenga kuonyesha kuwa dhana ya uchimuzi iliyohusishwa sana na ushairi na iliyokuwa na athari za mwelekeo wa Urasimu wa Kirusi, ni muhimu katika fasihi kwa jumla kwa kuwa inaweza kushughulikiwa katika riwaya ya kimajaribio.

Tatu, masuala yaliyoshughulikiwa na mwandishi katika riwaya ya *Mafamba* hayahusu tu vitushi vya siasa nchini Kenya pekee bali pia yanadokeza jinsi hali zilivyo katika nchi nyingine hasa za Afrika kama Zimbabwe na kuwa mambo haya yanazikumba nchi, jamii na ulimwengu kwa jumla.

Nne, riwaya ya *Mafamba* ni riwaya ya kwanza ya Tom Olali na kwa hivyo, tunadhamiria kuchunguza iwapo mwandishi huyu amefaulu au amefeli katika usanii wake kwa misingi kuwa alianza uandishi wa riwaya kwa kuandika riwaya ya kimajaribio ambayo inasawiriwa na wengi kama 'ngumu' kuandika na kueleweka. Riwaya ya *Mafamba* ni riwaya inayosheheni matumizi ya sifa za kimajaribio kwa kiwango kikubwa na hasa yanayohusiana na usimulizi, msuko na uhusika.

## 1.6 Upeo na mipaka

Uhakiki huu unahusu nafasi ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba*. Mjadala utahusu uelezaji wa dhana za riwaya ya kimajaribio au riwaya mpya, uchimuzi, na viwango mbalimbali vya uchimuzi kama vinavyojitokeza katika riwaya ya *Mafamba*. Viwango hivi ni vipengele muhimu vya uchanganuzi wa uchimuzi katika riwaya ya kimajaribio. Hivi ni viwango vya matumizi ya lugha na usimulizi.

Tunatafiti kazi hii kwa kutumia mtazamo wa Urasimu wa Kirusi ambao unahusishwa sana na dhana ya uchimuzi. Tutajifunga katika kushughulikia riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* na kuonyesha uchimuzi wa viwango mbalimbali katika uendelezaji wa riwaya hii. Tutaonyesha uchimuzi katika kiwango cha wahusika kwa kuthibitisha kuwa usawiri wao hauzingatii misingi ya jadi ya kuwasawiri kama binadamu halisi hivi kwamba, hawaonekani kama viumbe wanaoweza kupatikana katika jamii. Aidha, tutadhihirisha kuwa matumizi ya lugha katika riwaya hii yanachimuzwa na kukiuka kaida za kawaida za matumizi ya lugha. Kwa namna hii, maudhui yanayosibu jamii, nchi na ulimwengu kwa jumla, yanachimuzwa na kusisitizwa kiasi kwamba, yanaelezea ukweli katika muktadha mpana ambao unavunja ukawaida uliozoeleka.

Tumerejelea riwaya nyingine za kimajaribio ili kubainisha kuwa riwaya ya *Mafamba,* inaafiki sifa kadhaa zinazohusishwa na riwaya hii. Sifa hizi zilituwezesha kuichagua riwaya hii ili kufanikisha malengo yetu.

## 1.7 Misingi ya nadharia

Uhakiki huu unaongozwa na Nadharia ya Urasimu wa Kirusi ambao unajulikana pia kama Urasimu au Umaumbo. Inaitwa Nadharia ya Urasimu wa Kirusi kwa sababu wahakiki wake walikuwa wasomi katika nchi ya Urusi. Mwasisi wa nadharia hii alikuwa Viktor Shklovsky ambaye aliandika makala *'Ufufuo wa Neno'*. Katika makala haya, alisisitiza umuhimu wa lugha katika kuelezea maana ya fasihi[4]. Mbatiah, (2001:86) anasema kuwa, hii ni nadharia iliyoibuka mjini Moscow katika miongo miwili ya kwanza ya karne ya ishirini na iliyokuwa na mwelekeo kwamba, fasihi ni matumizi ya kipekee ya lugha ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida na kuwa fasihi humwezesha msomaji kukiona kitu, jamii au tajriba fulani kwa mwanga mpya. Nadharia hii inahusishwa sana na dhana ya uchimuzi kwa kiwango kikubwa. Neno uchimuzi ni tafsiri ya neno la Kiingereza 'foregrounding'. Hata hivyo, Mbatiah (2001:100) anairejelea dhana hii kama 'uradiradi'. Anasema kuwa ni mbinu muhimu ya uandishi ambapo kwa kutumia uhuru wa kishairi, msanii anakiuka kimakusudi kaida za matumizi ya lugha na hivyo kuvifanya vipengele fulani vya mtindo wake vijitokeze. Kwa namna hii, ujumbe unawasilishwa kwa njia bora kwa kuvisisitiza vipengele hivyo.

Uchimuzi ni neno lililotokana na Garvin (1964), kama tafsiri ya Czech 'aktualisace'. Dhana iliyokuwa mashuhuri sana na mwanamuundo wa Prague, Jan Mukarovsky ambaye alilitumia kurejelea neno la Kiingereza 'actualization'. Yaani, hali ya kukifanya kitu halisi kuliko cha kweli. Ingawa neno uchimuzi liliundwa kwa njia hii na wanamuundo wa Prague, dhana yenyewe

sio uvumbuzi au ubunifu wao, bali mawazo yao yalikuwa tu ukuzaji wa kihistoria wa mawazo yaliyozalishwa na Wana-Urasimu mathalani Viktor Shklovsky anayehusishwa na mbinu ya ostranenia au uajinabishaji. Kulingana na Shklovsky, umuhimu wa sanaa ni kukifanya kitu kuonekana kama kisicho cha kawaida na kwa namna hii kusawiriwa kwa njia mpya. Huu ni ukweli unaobainika katika riwaya ya *Mafamba* ambapo msomaji yeyote wa hadithi hii anahisi kwamba, mambo yanayoelezewa kutokana na usawiri wa wahusika na usimulizi kama yasiyo ya kawaida lakini kwa hali halisi ni mambo yaliyowahi kutendeka katika jamii yetu ila tu yanawasilishwa kwa mtindo mpya. Hata ingawa dhana ya uchimuzi ilisisitizwa zaidi na Wana-Urasimu katika karne ya ishirini, ni dhana yenye asili kutokana na mawazo ya Aristotle katika kazi yake ya *'Poetics'*. Alisisitiza kwamba, matini za kifasihi huzingatia kanuni na kwa njia hii mbinu za ukiushi na usambamba huchukua nafasi kubwa. Kwa mujibu wa mawazo yake, uteuzi wa matumizi ya maneno katika kazi ya kifasihi lazima upambanuliwe (Finke, 1989:77 ). Ili kufanikisha athari hizi, matumizi ya maneno yasiyo ya kawaida, sitiari, maneno ya kiajabu na miundo mirefu ya sentensi au maneno hutumiwa.

Erlich, (1969:63-64) anasema kuwa, nadharia hii iliibuka nchini Urusi katika miaka ya 1915-16 na kuwa waasisi wake walikuwa wasomi chipukizi wengi wao wakiwa chini ya umri wa miaka ishirini. Wasomi hawa waliunda makundi madogo ya majadiliano nje ya vikwazo vilivyowekwa na mitalaa rasmi ya elimu. Hawa walikuwa wanafunzi wa fasihi na wana- filolojia kama Roman Jakobson, Boris Eichenbaum, Juri Tynjanov, Viktor Shklovsky miongoni mwa wengine, Selden (1995:11). Uhakiki wa nadharia hii ulifikia kilele miaka ya 1917-1930 ambapo makundi mawili yalihusika katika uendelezaji wa nadharia hii.

Kikundi cha kwanza kilibuniwa na wanafunzi wa chuo kikuu cha Moscow kilichoitwa **Chama cha Kiisimu cha Moscow** (Moscow Linguistic Circle) kilichoanzishwa mwaka wa 1915 na

wanachama waliohusika walikuwa Roman Jakobson, Petr Bogatryrev na Grigory Vinokuv. Kundi la pili lilikuwa **Chama cha Mtalaa wa Lugha ya Kishairi** (Society for the Study of Poetic Language) lililojulikana kama OPOJAZ. Lilianzishwa katika mji wa Petrogad (Petersberg) mwaka wa 1916 na lilikuwa na wahakiki kama Viktor Shklovsky, Boris Eikhenbaum, Yuri Tynyanov, Lev Jakubinskij na Sergej Bernstejn, Fokkema na Kunne-Ibsch (1979:2).

Makundi haya licha ya kuwa na uhusiano wa kirafiki, yalitofautiana kimawazo kwa kuwa yaliangazia suala la fasihi kwa kuzingatia mitazamo miwili. Kikundi cha kwanza kiliamini kuwa, ushairi ni lugha inayotenda kazi ya kiujumi na kuwa maendeleo ya kihistoria ya miundo ya kiujumi yalikuwa na misingi ya kisoshiolojia. Kundi la pili liliamini kuwa motifu ya kishairi kwa kila njia, hutegemea miundo, Selden (1995:11-12).

Kulingana na Erlich (1969:82), waasisi wa Urasimu waliegemea sana upande wa ushairi kwa kuwa kuanzia miaka ya 1915-21, utanzu wa ushairi ulitumiwa sana kwa sababu kinyume na riwaya, mashairi yalikuwa na wepesi wa kuwasilishwa mbele ya hadhira, njiani, mikahawani au hata katika mikutano ya wafanyakazi. Walielezea vipengele vya kiarudhi vya ushairi kama vile sauti, vina, mizani, na wizani. Aidha, walitoa maelezo ya kijumla kuhusu namna mashairi yanafaa kutungwa kwa ufundi na uhuru wa kutumia lugha. Kwa mantiki hii, walifafanua kuwa kilichokuwepo ni 'ushairi' na wala sio 'washairi' au msanii anayehusika, Wamitila (2003:189). Yaani, kilichokuwa na maana ni kazi maalum za kifasihi wala sio chimbuko wala athari zake kwa wasomaji. Lengo lao lilikuwa kuitazama fasihi kama sanaa ya maneno wala sio kubainisha mitazamo ya kijamii. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa uchimuzi wa kimakusudi wa lugha haujabanika tu katika ushairi. Baadaye, Wana-Urasimu walijihusisha na tanzu za kimasimulizi kama vile riwaya na wakaelezea jinsi vipengele vya fani vilivyooanishwa. Miongoni mwa mbinu

walizozishughulikia ni mazungumzo, mpangilio wa visa au hadithi walioirejelea kama 'fabula' na mpangilio wa matukio au msuko waliouita 'sjuzet'. Pia, unadhihirika katika kazi za kinathari kama ambavyo tunaushughulikia katika riwaya mpya ya *Mafamba* na katika hotuba za vichekesho na michezo ya watoto na hali kadhalika katika kazi za kifasihi zisizoandikwa kama vile futuhi.

Kwa mujibu wa Leech (1969:57), fasihi kama asemavyo mtaalamu wa Czech, Jan Mukarovsky inatambuliwa na sifa bainifu mbili; uthabiti na utaratibu wa uchimuzi. Uchimuzi katika matumizi ya lugha ya kawaida kama vile ya mazungumzo ama ya uandishi wa habari hutokea bila mpangilio ama utaratibu fulani lakini uchimuzi katika matini za kifasihi ni muundo: hufuata utaratibu na mfumo fulani, sifa sawa kama sitiari hujitokeza na seti moja ya sifa hutawala nyinginezo. Sifa hii inarejelewa na Jakobson kama "the dominant" (sifa tawala). Leech (k.h.j:57) anasema kuwa uchimuzi ni ukiushi wa kaida za kiisimu ama kijamii zinazokubalika. Kulingana naye, ukiushi wa kisanaa hujitokeza wazi ikilinganishwa na mazingira hivi kwamba katika ushairi au kazi za kinathari, ukiushi wa kiisimu hurejelea umbo lililokiushwa nayo mazingira yanayozaa umbo hilo huwa lugha. Kwa mfano, kama ambavyo jicho hunasa umbo kama elementi muhimu na ya maana katika eneo au uwanja fulani wenye mwanga, vivyo hivyo msomaji wa kazi ya kifasihi hunasa ukiushi wa kiisimu katika kirai kama sehemu muhimu ya ujumbe na inayovuta nadhari na baadaye kuifasili kwa kuihusisha na mazingira ya ruwaza tarajiwa kama ambavyo tutafanya katika kuihakiki riwaya ya Kiswahili ya *Mafamba.* Kwa jinsi hii, tutaangazia ukiushi wa kiisimu au uchimuzi katika kiwango cha wahusika na matumizi ya lugha kwa kuelezea ujumbe muhimu unaojitokeza katika viwango hivi kulingana na maelezo yaliyotolewa. Ingawa fafanuzi hii ya Leech na Mukarovsky kama tutakavyoona zinasawazisha dhana ya uchimuzi na ukiushi, tunakubaliana na Kazungu (1982) kuwa uchimuzi sio lazima

uhusishwe na ukiushi kwa sababu kuzihusisha dhana hizi mbili kama moja na zilizo sawa inamaanisha kuwa mhakiki anafaa achukulie sifa za ukiushi kama sifa pekee ambazo zinastahili kuchimuzwa. Kwa mtazamo wetu, uchimuzi ni matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha katika matini za kifasihi zenye kuibua athari fulani kwa msomaji na ambazo hujitokeza kwa uwazi zikilinganishwa na lugha ya kawaida.

Nadharia ya Urasimu ilipata mashiko baada ya mapinduzi ya Urusi ya mwaka 1917 na mwanzoni mwa miaka ya ishirini kwa kiasi kilichoiwezesha kupenya zaidi katika uwanja wa kiusomi. Licha ya hayo, kulianzishwa kitengo rasmi cha kushughulikia historia ya uhakiki katika taasisi ya kiserikali mjini Petrogad. Hapa wasomi kama vile Eichenbaum na Shklovsky waliendeleza mijadala pamoja na wanafunzi kuhusu masuala ya kimtindo, mbinu za utunzi, miundo ya mashairi na mbinu za utunzi wa kinathari, Erlich (1969:83).

Hata hivyo, nadharia hii ilipata upinzani kutoka kwa wafuasi wa nadharia ya Umaksi ambao walikuwa wanamapinduzi wa Urusi ya 1917. Wakati makundi tuliyoyataja yalikuwa yakiendelea na harakati za kuishughulikia fasihi, kulitokea mapinduzi Urusi yakiongozwa na Viladimir Lenin. Wanamapinduzi hawa waliongozwa na itikadi iliyokuwa na misingi ya Karl Marx. Mtazamo wa wanamapinduzi kuhusu fasihi ulitofautiana na mtazamo wa wataalamu wa makundi haya mawili. Wanamapinduzi walikuwa na mtazamo wa kijamii kwani walichukulia kuwa fasihi haiwezi kutenganishwa na jamii. Lenin na Trotsky walipinga juhudi za Wana-Urasimu za kuitenga fasihi na soshiolojia na historia. Walionelea kuwa fasihi hutangamana na nyanja nyingine kama elimujamii, historia, soshiolojia na utamaduni. Wataalamu wa makundi mawili walitetea upekee wa fasihi, walisema kuwa fasihi ilikuwa huru na haifai kuchanganywa na masuala ya kijamii[5].

Baada ya kifo cha Lenin mwaka wa 1924, Joseph Stalin alichukua usukani na aliyapinga makundi haya mawili kutokana na mawazo yao kuhusu fasihi. Alidai kwamba, yalikiuka sera rasmi ya serikali iliyojikita katika uhalisia wa kijamaa. Tukio hili liliwafanya baadhi ya wanachama wa makundi haya mawili kuhamia nchini Czechoslovakia ambapo walikikuta kikundi cha Isimu cha Prague (Prague Linguistic Circle) kilichoanzishwa mwaka 1926 na wakaungana kuiendeleza Nadharia ya Urasimu. Lenin na Trotsky walichukulia fasihi kama silaha katika mapambano ya kitabaka na nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa. Trotsky (1960:180) anadai kuwa ingawa njia za uhakiki wa kirasimu zinafaa, hazitoshelezi kwani bila ya kuhusisha kazi fulani ya kisanaa na mazingira, inatusaidia tu kuelewa muundo wa nje wa kazi hiyo na wala sio muundo wa ndani ambao ni muhimu.

Kufikia mwaka wa 1930, historia ya Urasimu ilikuwa imefifia kutokana na mwingiliano wake na siasa. Baada ya kifo cha Stalin mwaka wa 1953, shughuli za kiurasimu ambazo zilikuwa zimefifia zilikusanywa tena. Wana-Urasimu walipata mshawasha wa kutalii, kuchunguza upya na kuhifadhi tena mawazo ya Urasimu na maoni yao yanaendelea kuishi na ni sehemu muhimu ya nadharia ya uhakiki wa fasihi, Fokkema na Kunne- Ibsch (1979:1-2).

## 1.7.1 KANUNI KUU ZA WANA-URASIMU

### 1.7.1.1 Mtalaa wa kisayansi wa fasihi

Kanuni kuu ya Urasimu ilikuwa mtalaa wa kisayansi wa fasihi (Scientific Study of Literature). Shabaha ya wasomi hawa ya kijumla ilihusiana na mtalaa wa lugha na uamili wake katika kuipa maana kazi fulani ya kifasihi. Haja yao ilikuwa kubuni sayansi huru ya lugha ambayo ingezitalii kazi za kifasihi kwa misingi ya kiisimu. Ili kuitalii fasihi kisayansi, ililazimu Wana-Urasimu kutafuta sifa za kijumla au za kawaida za fasihi. Hivyo, Jakobson katika mwaka wa 1921

alionelea kuwa ufasihi uwe msingi wa sayansi ya fasihi badala ya kuiangalia kwa ujumla wake ama kwa kuzingatia kazi za kifasihi za watu binafsi, Fokkema na Kuune-Ibsch (1979:12). Ili kuweka msisitizo kwa mbinu za fasihi, Jakobson na Ejchenbaum waliamini kuwa vipengele vingine vyafaa kutolewa katika matini za kifasihi na kuchunguzwa kwa upekee kwa kuzingatia matini na muktadha (k.h.j, 1979:13). Aidha Wana-Urasimu walikubaliana na maoni ya Krucenych (1979:13) kuwa umbo jipya huzaa maudhui mapya na kuwa maudhui hutegemea umbo, hivyo basi, maumbo tofauti ya kazi ya kifasihi huwa na maana tofauti. Azma yao vilevile ilikuwa kuwawekea mipaka waandishi wa fasihi kutokana na mitagusano na taaluma nyingine kama vile saikolojia, soshiolojia, historia na filosofia[6]. Walisisitiza miundo bora ya mbinu za kisanaa katika uandishi wa kiubunifu na kwa njia hii kuipa fasihi uhuru wake bila ya kuihusisha na matini au mambo nje ya matini ya kifasihi. Erlich, (1969:71) anafananisha mwelekeo huu na askari ambao wakitumwa kumkamata mtu fulani, hukamata vilevile na mtu au kitu chochote wanachokipata nyumbani mwake wakiwemo wapita njia.

Katika uchunguzi wao wa fasihi, Wana-Urasimu walitilia maanani fasihi ama miundo ambayo inabainisha fasihi na amali za binadamu, kuwa fasihi inapaswa izingatie mielekeo ya fasihi. *Aidha, walisisitiza haja ya kuupa nafasi kuu 'ukweli wa fasihi' (literary facts) kutokana na masharti ya kimetafizikia katika uhakiki wa fasihi, ambayo yaweza kuwa ya kifilosofia, kiujumi* ama ya kisaikolojia. Ili kutimiza malengo haya, mitindo mbalimbali ilikuzwa. Juhudi yao ilihusisha ufafanuzi wa seti ya tabia zinazohusiana na lugha ya kishairi ambayo ni ya ushairi au ya kinathari inayotambulika kutokana na ufundi wa kisanaa. Kulingana na Peter Steiner, tabia hizi zilikuwa za aina tatu[7]. Kwanza, ni 'ufundi wa Urasimu' (mechanistic formalism). Kikundi cha OPOZAJ, kikiongozwa na Viktor Shklovsky, kilitilia maanani njia rasmi na iliyolenga kuzingatia ustadi wa kiufundi na mbinu. Kazi za kifasihi kulingana na mtindo huu,

zinashabihiana na mashine, Selden (1995:18). Huwa ni matokeo yanayosababishwa na utendakazi wa binadamu, kama ambavyo ufundi maalum unabadili malighafi hadi kuwa utaratibu changamano uwezao kutenda kazi maalum. Mtazamo huu huiondoa kazi iliyobuniwa ya fasihi kutoka kwa uhusiano wake na mwandishi, msomaji na usuli wa kihistoria[8]. Uchimuzi katika matini za kifasihi hutumiwa kwa makusudi na huwa na maana. Wakati ambapo msomaji anakumbana na miundo ya uchimuzi katika matini anayoisoma, mbali na kutambua miundo hii, humfanya atafakari motisha kuu ya matumizi ya mbinu hizo na mwandishi katika matini husika. Katika kujaribu kupata motisha, msomaji huweza kupata maana halisi ya ujumbe ambao umewasilishwa na mwandishi katika kazi ya kinathari au ushairi. Katika kuihakiki nafasi ya uchimuzi katika riwaya ya *Mafamba*, tutabainisha motisha kuu ya mbinu husika ili kubainisha dhamira kuu ya mwandishi. Kutokana na matumizi ya mbinu ainati na mwandishi wa *Mafamba* kama vile ukweli bunilizi, matukio yaliyoikumba jamii yetu miaka iliyopita yameelezewa kwa undani kwa kuzingatia ustadi wa kiufundi wa mbinu.

Pili, Wana-Urasimu wengine walizingatia mtindo wa kiviungo (organic model). Bernstejn (1927) alithibitisha kuwa sifa bainifu za kazi ya sanaa ni kuwa na ukamilifu kwa kiasi kwamba, haiwezi kugawika katika vijisehemu. Kazi ya sanaa haitokani na kuongezea elementi bali kwa vipengele ambavyo wakati wa kupanga nyenzo kwa ukamilifu huwa sehemu ya muundo wa kazi ya sanaa. Kwake, ingawa kazi ya kisanaa haiwezi kugawika katika elementi, kuna uwezekano wa kuchanganua muundo wake kisanaa (k.h.j, 1979:21). Walibainisha tofauti kati ya viungo vya kimwili na matukio ya fasihi kama idhihirikavyo katika kazi ya kibinafsi na tanzu za kifasihi. Fasihi kama vilivyo viungo vya kibiolojia, inao muundo uliokamilika. Sehemu zake zimefungamanishwa kwa kufuata mfumo fulani. Kwa mintarafu hii, ufafanuzi wa mbinu uliongezewa utendakazi katika matini.

Analojia kati ya biolojia na nadharia ya fasihi iliweka misingi ya urejelezi wa uchanganuzi wa tanzu na uhakiki wake. Kama vile viungo vya binadamu vinashirikiana katika utekelezaji wa mambo muhimu na kwa ambavyo aina mbalimbali ya wanyama au mimea inayofanana huwekwa katika jamii moja, vivyo hivyo kazi za kibinafsi ni sawa na kazi nyingine zenye muundo sawa wa kimaandishi na huwekwa katika utanzu mmoja, Selden (1995:19). Kwa mintarafu hii, uchimuzi katika kazi za kifasihi na hasa katika riwaya mpya au riwaya ya kimajaribio huweza kutokea katika viwango tofauti. Mathalani, kiwango cha kifonetiki, kiwango cha kimaana au kisemantiki ambapo maneno au vifungu tofauti hupewa maana kadhaa na pia kutumiwa kwa njia isiyozoeleka. Katika kiwango cha kisintaksia ambapo kuna ukiukaji wa miundo ya virai na vishazi na mwisho urudiaji unaochimuza na kufanya mofu, sauti, neno, sentensi au kishazi kujitokeza wazi.

Uchimuzi katika matini za kifasihi hutokana na nia ya mwandishi kutaka kuwasilisha ujumbe fulani kwa uzito na hivyo mwandishi mwenyewe hubainisha miundo mbalimbali ambayo atatumia ili kuchimuza sifa maalum katika kazi yake. Kwa njia hii, maana ya sifa za miundo ya uchimuzi hutegemea ufasili wa msomaji kupitia jitihada na taswira za usawiri wa sifa na matini anayosoma. Kwa mujibu wa Halliday kama alivyonukuliwa na Chatman (1971:339), sifa inayojitokeza huchimuzwa tu kwa misingi kuwa, inahusiana na maana ya matini kwa ujumla, uhusiano ambao hutenda kazi maalum au huwakilisha maana fulani. Aidha, kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa riwaya ya *Mafamba* ni mfano wa riwaya ya kimajaribio kutokana na muundo wake unaoafiki sifa za riwaya hizi tulizojadili hapo awali. Hali kadhalika, uchimuzi katika riwaya hii unajitokeza katika viwango tofauti vinavyowakilisha ujumbe wa mwandishi kutokana na miundo kadhaa ya lugha.

Tatu, ni mfumo wa Urasimu wa kimfumo (systematic formalism) ambao uliasisiwa na Yuri Tynyanov mwaka wa 1924 (k.h.j, 1995:20-21). Alisisitiza kwamba, mabadiliko ya fasihi ni mapambano kati ya elementi, mwigo wa kubeza (the method of parody) na upembuzi wa mbinu (the dialectic pray of devices). Kwake, kwa kuwa fasihi huhusisha masuala ya mifumo ya kitamaduni, upembuzi wa fasihi huhusika katika mabadiliko ya kitamaduni. Hivyo, fasihi inahusiana na amali za binadamu mathalani mawasiliano ya kiisimu ambayo hustawishwa na kanuni jenzi mpya. Kudhihirika kwa uchimuzi katika kazi ya kifasihi kwa mujibu wa Kazungu (1982:33) hutegemea mapenzi ya mwandishi ya kuutumia. Kwa mantiki hii, sio sifa zote hujitokeza kama kiwakilishi cha matini bali sifa ambazo zinaonekana kutoa ujumbe ndizo huchimuzwa. Katika riwaya ya *Mafamba* kwa mfano, herufi kubwa zimetumiwa katika matini ili kuchimuza maana kadha kama vile, kuashiria nguvu au upaaji, kuonyesha masuala mazito, ufikaji juu kwa jambo, kusisitiza jambo na kuonyesha kinachosemwa ni muhimu sana. Suala linalobainisha umuhimu wa sifa inayochimuzwa ni juhudi za msomaji zinazomwezesha kutafakari na kutafsiri uhusiano kati ya sifa husika na matini na kwa njia hii, kumpa usawiri mpya wa kazi hiyo.

Nne, ni Urasimu wa kiisimu (linguistic formalism). Jakobson alishikilia kwamba fasihi kamwe haipaswi kuhusishwa na hisia. Kwake, sifa bainifu za kihisia katika fasihi ni duni na zinafungamana na uhakika wa maneno ya kiisimu (verbal, linguistic facts). Anasisitiza 'ufasihi', yaani matumizi ya kipekee ya lugha kama msingi wa lugha ya fasihi badala ya kuangalia fasihi kwa ujumla au kwa kuzingatia kazi za watu binafsi. Kwa njia hii, Jan Mukarovsky, anafafanua dhana ya uchimuzi kuwa ukiukaji wa kaida za lugha ya kawaida kwa makusudi na uwezo wa kukiuka kaida ambazo hudhihirisha ufasihi, Freeman (1970:42). Uchimuzi huibua athari ya ostranenia, yaani kufanya ajabu ili kuondoa uzoevu. Hivyo, sababu mojawapo inayotufanya

tusichoshwe na kazi za kinathari ni matumizi ya miundo tofauti ya lugha isiyo ya kawaida inayotuwezesha kutambua ukweli unaowasilishwa kwa njia ya ajabu inayochimuza mambo kadha kama ilivyo katika riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* ambapo ukiukaji wa kaida za lugha kimakusudi unadhihirika. Kwa mfano kuhusisha vitu ambavyo havifai kuhusishwa, kueleza ujumbe kwa njia ya kihalisiaajabu, matumizi ya italiki katika uandishi wa aya nzima miongoni mwa mengine.

### 1.7.1.2 Ostraneniya/ Uajinabishaji au Uondoaji wa uzoevu

Dhana nyingine iliyoundwa na Wana-Urasimu na iliyohusishwa zaidi na Viktor Shklovsky mwaka wa 1917 ni uajinabishaji. Iliibuka kutokana na neno 'Ostranenie' yaani 'making strange' (kufanya ajabu). Istilahi hii kulingana na Wamitila (2003:237) inarejelea hali ya kukifanya kipengele fulani cha lugha ya fasihi kijitokeze wazi kikilinganishwa na lugha ya kawaida. Dhana hii huhusishwa na uchimuzi na humfanya msomaji wa kazi za kifasihi kutambua sifa za kipekee zinazohusishwa na mitindo ya uandishi. Wana-Urasimu Shklovsky, Tynyanov, Eikhenbaum na Tomashevsky walichukulia kazi ya uandishi kama muungano wa sehemu changamano[9]. Sehemu hizi zilichanganuliwa kwa kuzihusisha na zingine, zile ambazo zilijitokeza kwa uwazi zilichukuliwa kama ambazo zimechimuzwa.

Kulingana na Shklovsky, usawiri wa binadamu wa mambo huchangiwa na mahitaji yake ya kila siku. Alionelea kwamba, mtazamo wa William Wordsworth kuhusu mazingira ambayo yanahifadhi utukufu na upya wa ndoto sio hali halisi ya ufahamu wa binadamu. Alisisitiza kuwa, sanaa huturejeshea ufahamu wa mambo ambayo yamepoteza umuhimu wake hasa tunapoishi katika dunia hii. Riwaya ya *Mafamba* kwa jinsi hii inatoa ufahamu wa michakato ya kisiasa ya awali kisanaa kwa kujenga maarifa kwa msomaji hasa kuhusiana na siasa na tabia ya wanasiasa

nchini. Umuhimu wa sanaa basi ni kubadili njia zetu za kawaida za usawiri wa mambo kwa kuyasawiri kisanaa. Katika kazi yake *'Art as a Technique,'* (Sanaa kama ufundi) Shklovsky anajadili jinsi sanaa inavyofanya mambo kuwa yasiyozoeleka na aidha kupanua usawiri wetu, Usanii ni njia ya kupata tajriba ya kisanaa ya jambo; jambo husika haliwi muhimu bali njia ambayo inawasilishwa kwayo, Selden (1988:274). Mukarovsky alionelea uchimuzi kama njia moja ya kuwasilisha kazi ya kifasihi kwa njia mpya. Alisisitiza kwamba, uwezo huu wa kukiuka kaida ndio hujenga ufasihi ama usanii katika lugha. Kulingana naye, utaratibu unaoandamana na ukiukaji wa kaida za matumizi ya lugha ndiko hujenga kazi ya kifasihi.

Shklovsky kama alivyonukuliwa na Fokkema na Ibsch (1979:15) aliiona fasihi kama iliyokuwa na uwezo wa kuifanya hadhira kutazama ulimwengu inamoishi kwa njia tofauti na vile imezoeleka. Ili lugha iwe na maana ya kifasihi, lazima iajinabishwe na kufanywa kuwa ngeni na vilevile kwa kuitumia katika miktadha isiyo ya kawaida. Upekee wa fasihi hutokana na jinsi inavyobadilisha kategoria za lugha ya kawaida na kwa namna hii kuwafanya wasomaji kuliona suala fulani tofauti na walivyozoea kuliona kila siku. Mbinu hii ilitumika kuelezea kuwa sanaa au fasihi hutuchangamsha na kutukumbusha maisha na uzoevu wetu kwa njia ngeni. Hii ni sifa inayodhihirika katika *Mafamba* ambapo mwandishi anatudokezea mambo ambayo yamepitikia jamii zetu na kwa namna hii kutukumbusha sifa hasi za viongozi wetu na hali kadhalika kupambanua na kuangazia macho ya umma kwa kutumia mbinu kadha za lugha.

Kulingana na Shklovsky, kunazo njia kadha za kuonyesha mambo kuwa mageni ama kuondoa uzoevu. Athari ya mbinu kama usambamba, tashbihi, urudiaji, na balagha ni kukibadilisha kitu kutoka hali yake ya kawaida na kukifanya kipya hivi kwamba, maana mpya na ambayo haikuwepo nayo inajitokeza. Athari za matumizi ya mbinu kadha zimechimuzwa na kufanya maudhui, wahusika, lugha na usimulizi katika *Mafamba* kujitokeza kwa njia mpya katika

kuieleza hali halisi ya mambo yaliyokumba jamii zetu katika utawala wa Maotad na vilevile yanayotukumba kwa sasa.

Wana-Urasimu waliamini kuwa lugha ya kawaida huajinabishwa na baadhi ya maneno kupewa sifa zinazoyakuza na kuyachimuza yakawa waziwazi. Katika ushairi, mbinu tofauti za utunzi kama mizani na wizani hutumiwa na hutofautisha lugha ya kishairi na ya kawaida kwa kuyaunda maneno mapya. Athari ya uajinabishaji ya mbinu fulani hutegemea jukumu la mbinu hizo katika kazi husika. Dhana ya uajinabishaji ilipanuliwa na Jan Mukarovsky, mwanachama wa kikundi cha 'Prague Linguistic Circle' (Kikundi cha Kiisimu cha Prague) kuwa uchimuzi[10]. Wana-Prague kwa mujibu wa Leech na Short (2007:23), walibainisha jukumu la lugha ya kishairi au kifasihi kutokana na uchimuzi wa ishara za kiisimu. Hivi kwamba, matumizi ya kiujumi ya lugha huvutia wasomaji kwa njia mpya na yenye kuibua hisia katika lugha, suala linalochukuliwa kutokea bila mpangilio.

Boris Tomashevsky, mshirika mmoja wa Shklovsky alitoa mfano wa uajinabishaji kwa kutumia mbinu ya Jonathan Swift ya kuelezea njia za kibinadamu kupitia kwa hadithi yake *Gullivers Travel*[11] (Safari za Gulliver). Msimulizi hatumii tasfida katika kuelezea uozo na upumbavu wa mwanadamu na kwa njia hii, udhalimu wa kitabaka unadhihirishwa. Tunamwoma Gulliver kama mwanabaharia anayepotelea baharini baada ya chombo chake kuharibika. Baadaye, anajikuta katika nchi ya majitu ambapo yeye anakuwa mtu wa kimo kidogo sana. Hata hivyo, anapata uwezo wa kimaajabu wa kuviona vitu ambavyo majitu hayangeweza kuviona. Kwa namna hii, tunapata kuona ulimwengu mpya. Mwandishi anafanikiwa kuonyesha uozo katika jamii ambao haungetambulika kwa mtazamo wa kawaida. Katika *Babu Alipofufuka*, mwandishi anatumia Mzuka wa Babu yake K ili kuchimuza uozo wa kimaadili wa viongozi na kutowajibika kwao kunakojitokeza kupitia kwa K. Hivi ndivyo ilivyo katika mataifa ya kiafrika. Katika *Mafamba,*

mtunzi amebadilisha majina halisi ya wahusika na mahali ili kudhihirisha uozo wa kimaadili na kutowajibika kwa njia inayochimuza tabia zao na hali kadhalika kuifanya hadithi ya kuvutia kwa kubadilisha usawiri wa jamii zetu kwa njia mpya.

Leon Tolstoy katika hadithi yake fupi *'Kholstomer'* alitumia farasi kusimulia. Katika masimulizi yake, anatoa maelezo kuhusu tajriba yake anapoishi katika jamii ya binadamu. Hali hii ya kutumia farasi badala ya binadamu ndiyo inayoyafanya maudhui ya hadithi kuwa yasiyozoeleka, Selden (1988:275). Tolstoy anasisitiza kuwa fasihi ni chombo ambacho kinaweza kutumiwa kuleta mabadiliko katika jamii. Katika fasihi ya masimulizi, Wana-Urasimu walibainisha mbinu zilizotumiwa kuunda hadithi kama vile masimulizi, mazungumzo na wahusika. Wana-Urasimu hawakutilia uzito wowote kwenye maana ya kazi za kifasihi, walisisitiza umuhimu wa jinsi ya kuunda kazi ya sanaa na bali sio kazi zinazotokana na sanaa. Katika riwaya ya *Mafamba,* uchimuzi ni mbinu ya kisanaa inayojitokeza waziwazi na ni nguzo kuu iliyotumiwa na mwandishi kusisitiza mambo tofauti yanayobeba uzito na ya muhimu kupitia kwa matumizi ya lugha na usimulizi kwa njia inayozaa maudhui mapya yanayoathiri jamii na hata mataifa. Kwa mujibu wa Shklovsky, kazi zinazoundwa sio muhimu katika sanaa na kuwa maudhui ya kazi za kifasihi ni jumla ya mbinu zilizotumika. Kwa mujibu wa Rice na Waugh (1996), fani mpya huzaa maudhui mapya.

### 1.7.1.3 Dhana ya 'fabula' na 'sjuzet'

Wana-Urasimu walibainisha kati ya *sjuzet* (msuko au ploti) na *fabula* (hadithi) [12]. *Fabula* ni malighafi ya kuundia ploti au msuko na *sjuzet* ni mpangilio wa matukio. Hadithi ni utaratibu wa matukio kwa mfuatano ilhali msuko unaweza kutiririka bila kufuata utaratibu wowote. Mawazo yao yalikuwa kwamba, katika masimulizi, dhana ya msuko na hadithi zafaa zipambanuliwe.

Utofautishaji huu ulipendekezwa kwa mara ya kwanza na Aristotle katika sehemu ya sita ya *Poetics*, ambaye aliona ploti kama mpangilio wa mwandishi wa matukio ya hadithi. Matukio huweza kupangwa kisanaa kwa kutumia miundo ya urudiaji na usambamba. Methodolojia hii ya kiufundi hufanya fasihi kuwa ya aina mbalimbali na yenye muungano wa stadi na mbinu ambazo hazina elementi za kisaikolojia ama za kifilosofia. Ploti ilichukuliwa kuwa njia kuu ya kuwasilisha masimulizi kimaana kwa kuwa ina dhana ya umbo na maana ilhali fabula ni jambo la kidhahania. Kulingana na Wamitila (2003:191), uhusiano uliopo kati ya *fabula* na *sjuzet* unaweza kulinganishwa na ule uliopo kati ya lugha ya kimatumizi au ya kawaida na lugha ya kishairi. Msuko huunda athari ya kiajinabishaji kwenye *fabula* au hadithi. Mpangilio wa matukio katika riwaya za kimajaribio kama *Mafamba* unamwezesha msomaji wa riwaya hii aielewe na kuzingatia vitushi kiwakati. Vitushi ambavyo vimechimuzwa kwa njia ya uwazi ili kudhihirisha lengo mahususi katika mahali fulani kwenye matini na vyenye kuleta athari kwa msomaji kutokana na matumizi ya mbinu mbalimbali. Katika *Mafamba* kwa mfano, mbinu kama uhusishaji, uhalisiaajabu, ukwelikinzani, urudiaji miongoni mwa nyingine zimetumiwa kuchimuza masuala kadhaa.

#### 1.7.1.4 Matumizi ya lugha katika sanaa

Jakobson (1921) alibuni dhana ya 'ufasihi', alitilia mkazo kuwa nia ya usomaji wa kifasihi sio kujihusisha na fasihi kwa jumla bali ni kujihusisha na ufasihi. Istilahi hii inarejelea sifa za kifasihi zinazoifanya matini fulani kuchukuliwa kama fasihi, yaani matumizi ya kipekee ya lugha katika fasihi, Mbatiah (2001:86). Kwa Wana-Urasimu, matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha huipa fasihi upekee wake na kuitofautisha na aina nyingine za mawasiliano. Sifa za kifani zilipata athari kubwa katika kuipa maana kazi fulani ya kifasihi kutokana na dhana ya ufasihi. Uchimuzi katika matini za kifasihi huvutia wasomaji na kuvuta nadhari yao. Kwa njia hii,

wanazingatia matini kwa makini, kuzidisha athari ya mvuto wa matini, kuwawezesha kutathmini ujumi na kubadili usawiri wa ulimwengu kwao nje ya matini za kifasihi. Katika uhakiki wetu wa riwaya ya *Mafamba,* tutaangazia uchimuzi katika matumizi ya lugha na kuonyesha mbinu tofauti zilizotumika na zinazodhihirisha ufasihi.

### 1.7.1.5 Mbinu za uwasilishaji

Wana-Urasimu walisisitiza kwamba, uandishi wa kiubunifu huhusisha usemi au diskosi ya aina fulani inayotambulishwa na msisitizo wa njia za kiuwasilishaji, Wamitila (2003:190). Walipendekeza njia tofauti za kuitazama fasihi bila kuzingatia uzito wa kijamii wala ujumbe katika kazi ya fasihi. Haya yanatokana na hoja mojawapo ya Viktor Shklovsky katika makala yake *"Art as a Device"* (sanaa kama mbinu) [13]. Sanaa ni jumla ya mbinu za fasihi na za kisanaa ambazo msanii huzifinyanga ili kuwasilisha kazi yake kwa ustadi. Uchimuzi hufanya uwasilishaji wa maana ya fasihi kuwa tata na changamano tofauti na ilivyo katika lugha ya kawaida. Kwa mantiki hii, kazi ya mbinu za kimtindo ni zaidi ya kuwasilisha maana ya kawaida. Sura ya kazi za kifasihi sio kutufanya tuisawiri maana bali kujenga mtazamo maalum wa jambo. Inajenga usawiri wa jambo badala ya kuonekana kama njia ya kulijua au kulielewa. Lengo kuu la Shklovsky katika makala haya yake lilikuwa kutupilia mbali mawazo ya fasihi na uhakiki wa fasihi yaliyotawala nchi ya Urusi wakati huo.

Kwa kiwango kikubwa, fasihi ilichukuliwa kwa upande mmoja kama matokeo ya kijamii na kihistoria ambayo yalifasiriwa katika misingi ya kitamaduni ya mhakiki Belinsky. Yaani, fasihi kama sehemu muhimu ya kijamii na ya siasa za kihistoria. Kwa upande mwingine, fasihi ilichukuliwa kama njia ya mwandishi ya kujieleza kutokana na anavyoisawiri dunia kwa kutumia taswira na ishara. Kulingana na Shklovsky, sio taswira ambazo hubainisha mashairi na historia

yake bali kuibua mbinu mpya za kuwasilisha ujumbe. Kwa hivyo, kuna mbinu nyingi kama takriri, jazanda, usambamba na kadhalika zinazochimuza katika riwaya za kimajaribio kwa namna ambayo inabainisha mafunzo tofauti katika riwaya husika. Kutokana na mitazamo hii miwili ya Belinsky[14], fasihi inatathminiwa kama inayoeleza usuli wa kijamii na kihistoria ama usuli wa kisaikolojia usio dhahiri. Hivyo basi, lengo la Shklovsky lilikuwa kutenga na kufafanua jambo muhimu la fasihi ama lugha ya kishairi: mbinu ambazo zinaifanya fasihi kuwa stadi. Mawazo haya ya Shklovsky yatatufaa katika kuchunguza uchimuzi wa viwango mbalimbali katika *Mafamba* unaobainika kufuatia mbinu za uwasilishaji zinazowezesha msomaji kujenga mtazamo maalum wa ujumbe.

Hata ingawa Wana-Urasimu hawakukubaliana hasa kuhusu mbinu ni nini, ama jinsi mbinu hizi zinavyotumika ama zinavyoweza kuchanganuliwa, wazo la kimsingi lilikuwa la kijumla: lugha ya kishairi au fasihi humiliki sifa maalum ambazo zinaweza kuchanganuliwa. Hivyo basi, Wana-Urasimu waliamini kuwa lugha ya kishairi au fasihi ni tofauti na lugha ya kawaida kutokana na matumizi yake ya mbinu mbalimbali.

Kwa muhtasari, mihimili mikuu ya Nadharia ya Urasimu ni kuwa fasihi ni matumizi ya kipekee ya lugha katika uwasilishaji wa fani na maudhui ambayo ni tofauti na lugha za kawaida na kuwa fasihi humwezesha msomaji kukiona kitu, jamii au tajriba fulani kwa mwanga mpya. Katika uwasilishaji wa kazi ya kifasihi, sehemu fulani hufanywa zichimuze kutokana na jinsi mtunzi anavyobadili kwa makusudi elementi za lugha.

Pili, ni kuwa ufasihi ni msingi wa kazi ya kisanaa kwa kuwa unaifanya kazi fulani itambulike kama kazi ya kifasihi badala ya kuimulika kwa ujumla wake ama kwa kuzingatia kazi za waandishi binafsi. Kwa njia hii, riwaya itatambuliwa kutokana na masimulizi ya kinathari,

msuko unaoonyesha vitushi mbalimbali na wahusika walioendelezwa kwa kina. Katika riwaya za kimajaribio tulizodurusu, mbinu ya uchimuzi imetumika na watunzi ili kutubainishia falsafa, tajriba na mienendo ya watu mbalimbali katika jamii zetu inayotuathiri kwa njia moja au nyingine katika uwasilishaji wa fani na maudhui.

Tatu, kazi ya kisanaa inapaswa kuelezwa kwa kuzingatia kanuni za kisanaa pekee ili iweze kuwa huru. Kwa njia hii, fasihi haipaswi kuhusishwa na masomo mengine kama vile soshiolojia, historia ama saikolojia. Ingawa haya yalikuwa maoni yao Wana- Urasimu, kwa maoni yetu, fasihi inaweza kuhusishwa na masomo mengine kama ambavyo tunaihusisha riwaya ya *Mafamba* na historia ya Kenya.

Nne, ni kuwa kazi ya kifasihi inafaa ifinyangwe kwa kutumia mbinu tofauti za kipekee na za kisanii katika uandishi wa kiubunifu kwa kutumia sanaa ya maneno. Dhima ya mbinu hizi ni kufanikisha uelewa wa masimulizi. Mathalani, matumizi ya uhalisia mazingaombwe yanayochimuzwa katika riwaya za kimajaribio kama *Nagona, Babu Alipofufuka na Mafamba* unaonyesha kuwa matukio husika hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa mwelekeo huu waweza kutumiwa kuchanganua riwaya bali sio mashairi pekee kwa kumulika uchimuzi, fani na ujenzi wa ploti. Tutahakiki *Mafamba* kwa kutumia mwelekeo huu, huku tukiongozwa na mihimili tuliyojadili ili tuweze kufanikisha utafiti wetu.

## 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Dhana ya uchimuzi ni dhana ambayo imeibuka kuwa moja ya sifa bainishi za riwaya ya kimajaribio katika fasihi ya Kiswahili. Hii inatokana na ukweli kwamba, katika riwaya zilizojitokeza tangu miaka ya 1990 ambazo zinahesabiwa kama za kimajaribio, uchimuzi

unajitokeza kwa uwazi. Uchimuzi kwa njia hii unaweza kuangaliwa kama ufundi wa kiutunzi, ufundi ulio na uamili mkubwa katika utunzi wa fasihi. Lakini, hata kama huo ndio ukweli wa kiutunzi kuhusiana na riwaya ya kimajaribio, usomi na utafiti unaohusiana na matumizi ya mbinu hii haujajitokeza kwa kiasi sawia na cha utunzi. Miongoni mwa tafiti za mwanzo zilizojishughulisha na suala la uchimuzi ni kazi ya Kadenge Kazungu (1982) katika tasnifu yake ya uzamili. Alichunguza ukiushi na uchimuzi katika riwaya ya *Asali Chungu* ya Mohammed, S.A, shairi la *Swifa ya Nguvumali* la Hassan bin Ismael na tamthilia ya *Wakati Ukuta* ya Ebrahim Hussein. Katika utafiti wake, alifafanua dhana ya ukiushi na uchimuzi kwa kuzingatia kaida za lugha. Alionyesha jinsi ukiushi na uchimuzi unavyowaathiri wasomaji kwa kuwafanya wazielewe kazi za kifasihi. Utafiti wake ulitilia mkazo kwamba, sifa muhimu za ukiushi na uchimuzi zinapotumika na mwandishi zinamwezesha msomaji kupata maana ya ndani ya kazi husika na kwa namna hii kumfanya aisawiri kwa njia bora.

Vilevile, alisisitiza kuwa dhana hizi zina jukumu la kimawasiliano na hivyo zinastahili kuchukuliwa kama mbinu atumiazo mwandishi kuwasilisha ujumbe kwa msomaji. Kwake, dhana hizi zinatumika kama daraja baina ya umbo na maudhui katika kazi ya kifasihi. Alifafanua kuwa, kila wakati ambapo mwandishi anatumia mbinu hizi, huwa katika nafasi ya kuueleza ujumbe wake kwa msomaji kwa njia ifaayo na yenye maana. Madai haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa tunanuia kuonyesha kwamba, katika riwaya ya *Mafamba* mtunzi ametumia mitindo tofauti ya lugha inayoyachimuza mambo na kuyafanya yaonekane wazi katika uwasilishaji wa fani na maudhui kwa njia yenye kuathiri.

Alibainisha kwamba, ingawa dhana hizi huchukuliwa kama zisizo na mipaka wazi kwa kuwa ukiushi ni tabia moja ya uchimuzi kwani kuna uwezekano kwa mfano uchimuzi kuchukuliwa kama ukiushi ama dhana zinazohusiana kwa kiwango kikubwa, pia zinaweza kuchunguzwa kwa

upekee wao. Alishikilia kuwa, miundo ya uchimuzi sio lazima iwe imekiushwa kwa sababu kuhusisha dhana hizi mbili kama moja na sawa italazimu mhakiki kuzichukulia sifa pekee za ukiushi kama ambazo zinastahili kuchimuzwa. Alithibitisha haya kulingana na mawazo ya Cluysenaar (1976:57) katika uhakiki wake wa shairi la *Flying Crooked* ambapo alionyesha kuwa uchimuzi pia waweza kushughulikiwa katika misingi ifaayo ya kisemantiki ili kuonyesha maana zifaazo. Aidha, kutokana na uhakiki wa Halliday wa *Inheritors,* Chatman (1971:330-363). Madai haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tunachunguza uchimuzi pekee katika riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba.*

Utafiti wake uliongozwa na mtindo wa kiuhakiki wa matini wa Leech (1969:37) ambao una kanuni tatu za kuchunguza mtindo. Yaani, kiwango cha utambuzi kinachohusisha jinsi miundo ya lugha inavyotamkwa ama kuandikwa, kiwango cha umbo kinachorejelea msamiati unaotumika katika kuunda sentensi (kwa kufuata kanuni teule) na kinachohusisha masuala ya kisarufi na kileksika na aidha kiwango cha semantiki ambacho kinahusika na maana. Alizingatia viwango vya kiisimu vya kifonolojia au grafolojia, kileksika, kisarufi na kisemantiki ili kuonyesha athari na azma ya mtunzi ya kutumia ukiushi na uchimuzi katika matini. Hata hivyo, uchunguzi wetu unalenga kuonyesha nafasi ya uchimuzi katika riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* ili kubainisha unavyoathiri usimulizi na matumizi ya lugha.

Katika utafiti huu, tuliteua mwelekeo wa kihakiki wa Urasimu wa Kirusi ili kudhihirisha kuwa mtazamo huu una madai muhimu yawezayo kutumiwa kuhakiki fasihi kwa ujumla kutokana na mtazamo wake wa matumizi ya kipekee ya lugha yanayoondoa uzoevu ikilinganishwa na uandishi wa riwaya za kimapokeo katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui.

upekee wao. Alishikilia kuwa, miundo ya uchimuzi sio lazima iwe imekiushwa kwa sababu kuhusisha dhana hizi mbili kama moja na sawa italazimu mhakiki kuzichukulia sifa pekee za ukiushi kama ambazo zinastahili kuchimuzwa. Alithibitisha haya kulingana na mawazo ya Cluysenaar (1976:57) katika uhakiki wake wa shairi la *Flying Crooked* ambapo alionyesha kuwa uchimuzi pia waweza kushughulikiwa katika misingi ifaayo ya kisemantiki ili kuonyesha maana zifaazo. Aidha, kutokana na uhakiki wa Halliday wa *Inheritors,* Chatman (1971:330-363). Madai haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tunachunguza uchimuzi pekee katika riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba.*

Utafiti wake uliongozwa na mtindo wa kiuhakiki wa matini wa Leech (1969:37) ambao una kanuni tatu za kuchunguza mtindo. Yaani, kiwango cha utambuzi kinachohusisha jinsi miundo ya lugha inavyotamkwa ama kuandikwa, kiwango cha umbo kinachorejelea msamiati unaotumika katika kuunda sentensi (kwa kufuata kanuni teule) na kinachohusisha masuala ya kisarufi na kileksika na aidha kiwango cha semantiki ambacho kinahusika na maana. Alizingatia viwango vya kiisimu vya kifonolojia au grafolojia, kileksika, kisarufi na kisemantiki ili kuonyesha athari na azma ya mtunzi ya kutumia ukiushi na uchimuzi katika matini. Hata hivyo, uchunguzi wetu unalenga kuonyesha nafasi ya uchimuzi katika riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* ili kubainisha unavyoathiri usimulizi na matumizi ya lugha.

Katika utafiti huu, tuliteua mwelekeo wa kihakiki wa Urasimu wa Kirusi ili kudhihirisha kuwa mtazamo huu una madai muhimu yawezayo kutumiwa kuhakiki fasihi kwa ujumla kutokana na mtazamo wake wa matumizi ya kipekee ya lugha yanayoondoa uzoevu ikilinganishwa na uandishi wa riwaya za kimapokeo katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui.

Kuhusu riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili, hakuna utafiti wa kitaalamu wa riwaya ya *Mafamba* (2008) uliofanywa. Tafiti zilizofanywa ni za riwaya mpya za awali kama *Babu Alipofufuka* (2001) ambapo Olali alishughulikia muundo na dhidi-muundo wa riwaya hii katika *Jarida la Isimu la Chuo Kikuu cha Nairobi* (2010). Alidhihirisha kuwa muundo na mtindo katika riwaya za kimajaribio zinatofautiana kwa kiwango kikubwa na kazi za kihalisia. Muundo ni ruwaza au umbo katika kazi za kifasihi na inayohusiana na elementi za kazi hizi na zinazopangwa kwa uthabiti ili kukamilishana. Mtindo ni uteuzi wa vipengele vya lugha katika uandishi wa kazi za kisanaa.

Kuhusu riwaya ya kimajaribio, Olali (2010:82-98) anathibitisha kuwa, riwaya kadha za Kiswahili zilizoandikwa tangu miaka ya 1990 hadi leo zinadhihirisha muundo usio wa kawaida zikilinganishwa na miundo ya riwaya za kihalisia. Alionyesha kuwa, katika riwaya za Kiswahili kuna ukiushi wa kisarufi ambao husababisha tofauti katika utaratibu uliozoeleka hadi kwa ule usiozoeleka. Kwake, dhidi-muundo katika riwaya za Kiswahili za kimajaribio uhusisha uandishi usio wa kawaida kwa mfano wa sentensi, neno au sura ambayo inakiuka kaida za riwaya ya kihalisia.

Alionyesha dhidi-muundo katika *Babu Alipofufuka* ambao ni mtindo katika riwaya za kimajaribio unaoingiliana na mambo ya kifantansia, kiajabu, na kiubadausasa na wenye mitindo mipya ya uandishi wa kimajaribio ambao unajaliza katika masuala nyeti ya kimaudhui kama ya utandawazi, dini, filosofia na siasa za kimataifa. Msisitizo wake wa sifa za riwaya hizi ni uandishi unaokiuka kaida za kiitikadi, utathmini wa ujumi kwa ndani na uvunjaji kaida za lugha kwa namna inayompa mwandishi uhuru zaidi.

Anakiri kuwa msuko wa riwaya hizi ni changamano na hudhihirisha mbinu rejeshi kwa kiwango kikubwa. Kulingana naye, msuko wa riwaya hii upo katika vitengo viwili, yaani wa mhusika mkuu K na wa Mzuka wa Babu yake. Pindi Mzuka wa Babu yake uanzapo kufuatia maisha ya K, mambo ya kiajabu yanaanza kutendeka kama vile kupotea kwa chakula cha mbwa wake, 'Doggy', kuendesha na aidha kusumbuliwa na mzuka uliomtawala mara kwa mara. Licha ya hayo, mizuka ya watu ambao alitendea mabaya hapo awali ilimrudiarudia, hawa walikuwa watu halisi ambao yeye pekee ndiye aliyewaona. Mohammed, kama asemavyo Olali, alimuumba mhusika 'Mzuka wa Babu' kudhihirisha ukweli kwa wasomaji na K kuhusu mienendo mibaya ya K ya kuuhasi utamaduni na kutowajibika kama kiongozi.

Anadai kuwa, K anapouliwa na Mzuka wa Babu yake ili amwezeshe kuzuru dunia nyingine kwa mafunzo zaidi anawekwa kwa majaribio kwa kupotosha maisha ya watu wengi, kuwadharau na kutumia muda vibaya. Safari ifikapo mwisho na kurejeshwa katika dunia halisi, anapata kuwa hana chochote ila mbwa wake 'Doggy'. Anabadilisha maisha yake kutokana na mafunzo aliyoyapata kupitia kwa Mzuka wa Babu yake. Kazi hii itatufaa katika utafiti wetu kwa kuwa inadhihirisha njia mpya ya uwasilishaji wa maudhui kwa njia isiyo ya kawaida inayoyafanya yachimuze waziwazi ili jamii iweze kuyafahamu, jambo ambalo pia tutadhihirisha katika *Mafamba* kwa kuonyesha uchimuzi katika ngazi ya wahusika.

Dhidi-muundo katika riwaya hizi unakiuka kaida za riwaya ya Kiswahili kimofolojia, kisintaksia, na kifonolojia. Mathalani, kulingana na Olali, (2010:83) Mohamed ametumia mbinu ya uhuru wa kishairi na kuzipuuza au akaziacha mbinu za zamani za uteuzi wa matumizi ya maneno, sarufi na maudhui. Katika utunzi wake, ameunda, kurefusha, kugeuza na kuingiza maneno, jambo ambalo limefanya uandishi wake tofauti na riwaya za kihalisia. Amejipa uhuru

juu ya kaida kama kuweka viunganishi mwanzoni mwa sentensi kama ilivyo katika ukurasa wa 163.

> Na ndipo tena K alikuja kubebwa kitikiti; mzimamzimza na kubebwa nje. Na hayo hayakutosha......Na huko akaliona limonsin la Bw, Tajuri limeegeshwa bustanini....Na amri ni moja tu nchi hii.

Katika utafiti wake, Olali alibainisha dhidi-muundo katika matumizi ya mbinu za uhalisiaajabu kwa mfano unaodhihirika nyumbani mwa K, katika *Limonsin* yake na anapokuwa Neo-Casino, sintaksia yenye nyufa, matumizi ya italiki na wino mzito, uhusishaji, taswira, wakati na mahali, mbinu rejeshi, uzungumzi nafsi, tasfida, ukwelikinzani, urudiaji, usambamba, kinaya na ufasahaneno. Ameonyesha jinsi katika kuwasilisha uhalisiaajabu, mwandishi anayagawa maneno katika silabi kama idhihirikavyo katika ushairi. Anadai kwamba, matumizi ya mtindo huu hulenga kuonyesha kuwa matukio kama haya hutendeka katika ulimwengu na kosmolojia ya Kiswahili. Yaani, uhalisia huu unasawiri jamii ama sayansi kuhusu ulimwengu na hivyo matukio yanayoonekana kama ya kiajabu, kwa hakika ni ya kawaida katika uhalisia wa Kiswahili.

Aidha, anaonyesha kuwa matumizi ya italiki na wino mzito yanayotilia ujumbe mkazo, ni njia ya ukiukaji wa kaida na hali ya kuonyesha dunia iliyopasuka. Matumizi ya uhusishaji anayachukulia kumaanisha kuwa katika jamii tunamoishi, binadamu ana utegemezi kwa kiwango kikubwa katika vyombo vya kiteknolojia kwa kiasi kwamba, hawezi kuyatekeleza mambo kadha bila kuvitumia. Nayo matumizi ya taswira anayahusisha na mgawiko wa kitabaka katika jamii, kuwa kuna kutoelewana kati ya tabaka la juu na la chini. Uchanganuzi wa mbinu hizi ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu baadhi ya mbinu hizi zinadhihirika katika riwaya ya *Mafamba* na tutazifafanua tutakapojadili uchimuzi katika ngazi ya matumizi ya lugha na athari zake katika kuelewa ujumbe.

Aidha, tulidurusu pia kuhusu drama ya kimajaribio. Utafiti ambao ulihusu uhakiki wa *Sigana* kama drama ya kimajaribio, Atisiaya (2002). Utafiti wake ulitilia maanani vipengele vya kimuundo vinavyojenga drama ya *Sigana* kwa kuonyesha umuhimu wake katika kuijenga kazi yenyewe. Aidha, alitathmini mchango wa viambajengo hivi katika ujenzi wa drama ya *Sigana* kwa kuizungumzia sanaa hii ya kimajaribio ambao ni mtindo mpya wa drama iliyoibuka katika miaka ya tisini ya karne ya ishirini (wakati mmoja na riwaya ya kimajaribio). Utafiti huu unatufaa kwa kuwa mojawapo ya madhumuni yetu ni kuthibitisha kwamba, lugha ya Kiswahili ambayo inakua kwa kiwango cha kasi kutokana na kuzuka kwa mitindo mipya ya kisanaa, inachochea vionjo vya wasomi ambao hutaka kuvipigia darubini. Lengo letu ni kuwa utafiti wetu utachangia katika hazina ya uhakiki wa riwaya za kimajaribio na wa fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

## 1.9 Njia za utafiti

Utafiti huu ni wa maktabani. Ili kufanikisha utafiti huu hatutakuwa na budi bali kujihusisha na mbinu mbalimbali ili kutimiza madhumuni yetu. Mosi, tutasoma riwaya ya *Mafamba* kwa ufasaha na makini ili kuielewa kwa undani kwa lengo la kuichanganua vilivyo.

Pili, tutasoma riwaya nyingine za kimajaribio zilizoandikwa na waandishi mbalimbali ili kutathmini sifa za riwaya ya kimajaribio.

Tatu, tutasoma kuhusu yaliyoandikwa kuhusu riwaya ya kimajaribio au mpya na kuhusu uchimuzi ili kujua pengo lililoachwa. Somasoma zetu zilituwezesha kuchagua mada hii kwani hakukuwa na utafiti wa kitaaluma uliofanywa kuhusiana nayo.

Nne, tutasoma yaliyoandikwa kuhusiana na mwelekeo wa kihakiki wa Urasimu wa Kirusi katika vitabu na makala mbalimbali. Maandishi haya yatatuwezesha kuielewa nadharia hii kwa

kuangazia jinsi misingi ya madai yake inavyotumiwa katika uhakiki wa fasihi na kwa njia hiyo, kufanikisha ufahamu wetu na utafiti wetu.

Mwisho, tutaufumbata ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu, wahadhiri mbalimbali wakiwemo wanafasihi na wanaisimu na aidha, wasomi wa isimu.

## 1.10 Tanbihi

1. Khamis, S.A M. *"Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai.* http:www.ajol.info/index.phd

2. Khamis, S.A M. *Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili.* http:www.ajol.info/index.phd

3. Ibid

4. *http://210.4697.80/zonghe/book/30=unit 1-Russian-Formalism-htm*

5. Formalism (Literature) *http://en.wikipedia.org/wiki/formalism*

6. Everard's J. February 12,th 2007 http:// lostbiro.com/blog

7. Formalism (Literature) *http://en.wikipedia.org/wiki/formalism*

8. Ibid

9. Everard's J. February 12,th 2007 http:// lostbiro.com/blog

10. Surdulescu,R.July,2002http://ebooks.unibuc.ro/us/RaduSurdulescu-Formstructuality/capitolul.l.htm

11. Ibid

12. Literary theory: *The characteristics of Russian Formalism* Sep21, 2010. http://Maureencutajar.suite101.com/literary-theory-the-characteristics-of-russian-formalism

13. Formalism (Literature) *http://en.wikipedia.org/wiki/formalism*

14. Ibid

# SURA YA PILI

# USUKAJI WA RIWAYA YA *MAFAMBA*

## 2.0 UTANGULIZI

Sura hii inadhamiria kuuwekea msingi mjadala wa utafiti wetu. Usukaji wa riwaya hii utatuwezesha kujua njia mwafaka ya kuchambua maswali nyeti yanayohusiana na uchimuzi. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:175), usukaji ni dhana inayorejelea hali ya kuyachukua matukio au matendo ya kihistoria na kuyafanya sehemu ya msuko wa hadithi au kazi ya kifasihi. Katika hali hii, mtindo wa usukaji huwa umefichika bila kuwa dhahiri ambapo mwandishi huweza kuyatumia matukio ya kihistoria au wahusika. Hivi ndivyo ilivyo katika *Mafamba* ambapo mwandishi ameeleza matukio ya kihistoria ya nchi ya Kenya katika riwaya ya *Mafamba* kwa njia ambayo haidhihiriki kwa uwazi kwa kuwafinyanga wahusika, mandhari na matukio kifasihi.

## 2.1 USUKAJI WA RIWAYA YA *MAFAMBA*

Mwandishi anaanza hadithi kwa kutuchorea taswira halisi ya mtaa wa Bikerani-Msiige ambapo umaskini umekita mizizi. Mkabala wa mtaa huu, hali ni tofauti ambapo wakazi wake wanaishi maisha ya kifahari na ni matajiri kwelikweli, hali ambayo inamkera sana Arijojo ambaye ni mkazi na mwakilishi wa wakazi wa Bikerani-Msiige. Wakazi wa Bikerani-Msiige wamejaa uchungu mioyoni mwao kwa sababu wamenyimwa haki zao ambapo hawatimiziwi matakwa yao na hali kadhalika hawahusishwi katika utekelezaji wa maendeleo nchini.

Maotad, ambaye jina lake maarufu la kimajazi ni Aende lililoibuka kutokana na tabia ya wakazi wa Bikerani-Msiige kumwamurisha aende anasawiriwa kama kiumbe wa ajabu mwenye miaka 720 na anayesababisha dhuluma zote zinazowakumba wakazi hawa. Maotad ni kiongozi wa

sayari ya NUKA, sayari ya zamani sana iliyoumbwa yapata miaka mingi iliyopita wakati ambapo muumba aliumba Karifa (uk 7). Alipendwa sana na watu ambao haja zao zilikidhiwa na kutimizwa na kuchukiwa na watu kama Arijojo ambao haja zao kamwe hazikutambuliwa.

Katika hatua za mwanzo za kuleta mapinduzi ya ukombozi, Arijojo anaungwa mkono na Amrao, mwanasayari wa DiPieLi ambaye nia yake kuu ilikuwa kwamba, Maotad aende ili aghalabu apate kukikalia 'kiti cha enzi' ambacho kingemwezesha kuyaonja maji matamu. Licha ya juhudi zao na za LiMioe, mwanasayari wa PiDi aliyekuwa pia na uchu wa kuzileta sayari zote pamoja ili kuzitawala, Maotad alikataa katakata kubanduka uongozini na kupelekea hali yake kubadilika kiasi cha kuwa kiumbe wa kutisha. Hali hii yake ya kutisha haikuwa na mipaka, kila binadamu ambaye alimkosea aliona cha mtema kuni. Hata washauri wake wakuu kama Shanata na Nikiabi walipokea dhuluma za mara kwa mara kutoka kwake kwa sababu ya ujeuri wake walipotenda kinyume na matakwa yake.

Amrao, mwanasayari wa DiPieLi aliyekuwa na mamlaka makubwa katika sayari hii, anabainika kama mwenye matamshi ambayo hayakusikika. Alikuwa kigugumizi na alipozungumza, mazungumzo yake yalikuwa mchanganyo wa vitendawili, mafumbo na nahau. Alipendwa na kundi moja lililomwelewa na kuchukiwa na kundi lingine kama la Maotad. Nia yake ya kutaka kukitia kitumbua mchanga inasababisha awekwe kizuizini na Maotad kwa miaka 30. Hata hivyo, kwa bahati nzuri anaepuka kitanzi ambacho kilikuwa adhabu kwa yeyote aliyedhubutu kosa kama hilo ikizingatiwa kuwa, sayari ya NUKA tofauti na ya DUNIA haikuwaruhusu watu kujitetea na kwa ajili hii, haki za binadamu hazikuheshimiwa wala kuzingatiwa. Licha ya dhuluma hizi, watu wengi waliamini kwamba, sayari ya DUNIA haikutoweka na kwa hivyo itaonekana tena ambapo matunda yake yataendelea kuonjwa kama ilivyokuwa hapo zamani (uk 26).

Uhasama kati ya Maotad na Amrao uliendelea kuzidi na kila mara waliwindana usiku na mchana. Malengo ya Amrao yanabainika katika wimbo anaotunga akiwa kizuizini wa kutimiza haki za wakazi wa sayari zote pindi tu atokapo kizuizini. Ingawa hivyo, Maotad alikuwa na wimbo wake uliodhihirisha azma yake ya kuendeleza mafamba milele. Tunadhihirishiwa kwamba, sayari zote zilikuwa na miundo ya lugha ambayo ilizingatiwa. Miundo hiyo ilihusisha vokali na konsonanti zilizochukiwa mno na zingine kupendwa zaidi. Mathalani, katika sayari ya NUKA, herufi M, A, F na B zilipendwa kwa sababu hazikusababisha ufukara wala kumwalika ziraili nyakati za magharibi. Ni herufi zilizowakilisha dhana ya mafamba na kwa hivyo zilipendwa kwa dhati. Maradhi haya ya NUKA yalienea katika sayari nyinginezo jirani kama hospitalini na kanisani na kusambaa kati ya madaktari na wagonjwa, makasisi na waumini.

Nia ya Maotad ya kuiokoa sayari ya NUKA dhidi ya mahasidi wa sayari nyinginezo kama LiMioe, Boyi, Fadhila, Mastanji na Sinya inatambuliwa. Ingawa hivyo, alionyesha wasiwasi uliompelekea atake uhusiano na Amrao ili aweze kuwakabili. Ili kuwakomesha baadhi ya mahasidi hawa, alitoa amri katili dhidi yao ya kuwapeleka Mkanyangeni, makazi ambayo hayakufahamika kilichokuwa kikiendelea huko na wanasayari wengi wa NUKA na aidha na wanasayari wengine. Hili lilikuwa jumba la orofa 77 lililokuwa na sifa mbaya na lililokuwa limetengwa hasa kwa wale waliojaribu kumzaba makofi Maotad (uk 77). Waliopata kudhulumiwa katika jumba hili ni Mastanji na Charo miongoni mwa wengine.

Kiwewe cha Maotad kuhusiana na kung'atuka mamlakani na azma ya Amrao ya kugombania uongozi ni mambo yaliyozidi kujibainisha. Amrao aitwapo sebuleni mwa Maotad, anampata Shanata na kama ilivyokuwa kawaida ya sheria za NUKA, anamkaribisha kitini lakini Amrao anakataa kuvikalia viti vyote vya wageni na kusisitiza kwamba alitaka kukikalia kiti cha Maotad (uk 50-51). Hata hivyo, kwa kuwa Maotad pekee ndiye aliyepaswa kukikalia kile kiti, ilimbidi

Amrao asimame. Sio kwa sababu kilikuwa na swichi iliyounganishwa na nyaya za stima ili kuwaangamiza waliokosa kusalimu amri za Maotad bali ilidhihirisha nia na tamaa ya Amrao ya uongozi. Hivyo, Amrao aliamua kumuomba Maotad mwenyewe ruhusa ya kukikalia kiti hicho kwa sababu hakuridhika na jawabu la Shanata. Maotad alipoingia huku akiimba wimbo wake alioupenda wa kutukuza mafamba na uliochukiwa sana na Amrao anampata Amrao akiwa amesimama. Anamfokea Shanata kwa kuvunja sheria za sayari tukufu ya NUKA ila anatambua kwamba yalikuwa mapenzi yake Amrao kusimama. Katika hali halisi, Amrao alikuwa anamjulisha Shanata azimio lake kuu la kuwania kiti cha urais na alipokosa kumpa matumaini ya ushindi, aliamua kumwambia Maotad malengo yake.

Maotad hatimaye anamjulisha Amrao nia yake ya kutaka waungane ili waweze kukabiliana na mahasidi wao Fadhila, Boyi na LiMioe. Licha ya wao kuungana, Maotad anasumbuka ndani kwa ndani kwani sheria za haki ya sayari ya NUKA zilibainisha kuwa muda wake wa kujiuzulu ulikuwa umefika. Aidha, wanajamii na wanasayari wa nje walimtaka anga'tuke mamlakani. Ingawa alijiamini katika mchezo wa karata, yaani kuiba kura, ndoto ya kijinamizi iliyomjia mara kwa mara ilimtia wasiwasi kwani licha ya mahasidi wake kudhihirika katika ndoto hiyo, alimtambua Amrao pia katika ndoto hiyo mbali na wao kuwa wameshirikiana tayari akiwa na sumu na akiwa katika mstari wa mbele akiwaongoza akina LiMioe. Mwandishi anatubainishia kiwewe, tamaa na ubinafsi wa Maotad, alitaka kuwa kinara wa NUKA daima.

Maotad anapoungana na Amrao, watu mbalimbali wanakereka kutokana na jambo hili kwa kuwa waliamini kwamba, Amrao hakuwa na nia njema. Kajo ambaye alikuwa maarufu katika kumpaka Maotad mafuta kwa mgogo wa chupa, yaani kumpa sifa asizostahili, alikuwa mmoja wao (uk 66-67). Hata hivyo, Maotad alitupilia mbali mawazo ya Kajo na wenzake nia yake ikiwa kumtumia Amrao kukabiliana na Boyi na kundi lake ili kutosheleza haja yake ya kuendelea

kukikalia kiti cha 'enzi.' Maotad anabainika kama binadamu ambaye hakujali, hakutambua kamwe maslahi ya wakazi wa Bikerani-Msiige waliokuwa maskini hohehahe mbali na kubarizi katika sebule yake mkabala wao. Kutokana na hofu iliyozidi kumwandama popote hasa alipoimbiwa nyimbo za kumfukuza mamlakani, anaamua kuwaita Kamu, U, Avadi na Kanga ili awaambie siri. Siri iliyohusu uamuzi wake wa kujiuzulu na mtu aliyekuwa amechagua kuwakilisha NUKA. La kushangaza ni kuwa, wote waliambiwa siri moja kuhusu kutunukizwa kiti cha 'enzi,' kiti ambacho hakingeweza kukaliwa na zaidi ya mtu mmoja (uk 74-6). Azma ya LiMioe, Fadhila na Boyi ilikuwa kiti kiki hiki ambacho hawakujua jinsi ya kukifikia. Vilevile, walikumbwa na tatizo moja kuu la kutofahamu mwakilishi shupavu zaidi kati yao ambaye alifaa kukikalia kiti hiki akiwa wa kwanza. Tatizo hili lilitokana na ukweli kwamba, wote waliamini kwamba walikuwa na uwezo wa kuivusha meli hadi ngambo ya pili, yaani kuongoza.

Maotad anakutana na wakazi wa NUKA, U, Avadi, Kamu, Kanga, Amrao, Nikiabi, Kajo na Shanata ili awape faili. Faili zilizoidhinisha wajibu wa mmoja katika utawala wa NUKA. Faili za U, Avadi, Kamu na Kanga zilifanana kwa kila sura, nayo ya Amrao licha ya kuwa tofauti na ya akina U alifurahia. Hata hivyo, baadhi kama Kajo walikosa faili kwa sababu hazikutosha. Kajo alipata pigo kubwa kwa mara ya kwanza maishani mwake kwa sababu Amrao alipewa faili aliyotarajia kuipata, kazi ilimponyoka mikononi. Mbali na juhudi zake za awali za kumshawishi Maotad aukate uhusiano wake na Amrao, hakufaulu. Ni kama kwamba alikuwa ameonyeshwa katika ndoto. Kweli, dalili ya mvua ni mawingu, Kajo aliathirika na msukosuko ambao alitarajia Amrao aulete katika NUKA (uk 85). Licha ya kuahidi kuwa angesalimu amri ya karata na kutii wakazi wa Bikerani –Msiige, Maotad alibakia na faili iliyokuwa kubwa lakini baadaye alisalimu amri na kumchagua U kama kiongozi wa kuendeleza sera za NUKA.

Maotad pamoja na U na wafuasi wao walijizatiti kukabiliana na Amrao na kundi lake kwa kuwasilisha sera zao katika sayari nyingi za sayari ya NUKA kwa lengo la kuhakikisha kwamba Amrao haendi popote. Walijihami vilivyo wakiwa na imani kwamba ushindi utakuwa wao. Uadui wa Maotad na Amrao ulizidi licha ya wao kushirikiana hapo awali, wakawa maadui ambao hawangeweza kupaliana hata moto. Hata hivyo, Shanata na Nikiabi waliendelea kumsaidia kwa kuwa waliamini atawapa mambo mema kama vile mafamba. Ingawa watu wengi akiwemo Amrao walipinga vikali msimamo wa Maotad wa kumchagua U kuwa kiongozi baada yake, Maotad hakutishika bali alishikilia msimano wake.

Amrao kwa kuwa aliamini malengo yake kisiasa yalielekea kugonga mwamba, ilimbidi ajiondoe kwa kundi la U na Maotad. Kwa sababu hii, alianza mikutano katika mkahawa wa Hakuna Uma pamoja na Saigeo kwa madhumuni ya kuleta ukombozi kwa waliodhulumiwa. Mbali na ushirikiano walioudumisha katika mikutano yao hasa unaobainika katika unywaji wao wa damu ya nungumaria, ni dhahiri kuwa kila mmoja alikuwa na matumaini yake ya kisiasa yaliyodhihirishwa na ladha tofauti za vyakula walivyoagiza. Huu ulikuwa wakati ambapo kundi la BORA, la akina Boyi, LiMioe na Fadhila lilikuwa limepiga hatua kadha mbele ili kujitambulisha kwa wanasayari wote. Watu wengi walielekeza matumaini yao kwa kundi hili kwa kuwa waliamini lilikuwa bora na kwa kuwa walionelea kwamba sera zao zilikuwa bora na za kuigwa (uk 101). Ingawa wafuasi wa BORA walikuwa na matamanio tofauti, ushirikiano ulikuwa ngao yao iliyowaweka pamoja. Ingawa ni kundi lililotatizika mara kwa mara kuhusiana na atakayekuwa kiongozi wa merikebu yao, waliamua kwanza kuiabiri wakiwa kama abiria na dereva ili waweze kujipanga na halafu baadaye waamue.

Maotad aliendeleza kampeni zake mahali tofauti huku akisaidiwa na Kanje, U, Shanata, na Nikiabi. Katika mikutano yao, alikashifu vikali kundi la BORA ila tu juhudi zake ziliendelea

kuzimia kwani kila mara alipomtaja U kama chaguo la kuendeleza sayari ya NUKA aliungwa mkono na watu wachache. Hakuna makofi yaliyosikika kumshangilia na waliojibu maswali yake walikuwa wachache, ishara kwamba U hakupendwa hata kidogo. Aidha, majibu aliyopata Maotad yalikuwa mchanganyiko wa ndio na hapana ila hakuamini kwamba zile hapana zilitoka kwa wakazi wa Bikerani-Msiige. Wakati wa kampeni hizi, U hakupewa nafasi ya kuzungumza ila tu aliipungia hadhira mkono kama kwamba kufanya hivyo kulitosha (uk 131-132).

Kutokana na maingiliano ya NUKA na tamaduni mbalimbali, kulizuka mabadiliko ya kimaisha ya mara kwa mara kwa wanasayari kadha. Kwa muda mrefu, wakazi wa Bikerani-Msiige walikuwa washirika katika unywaji wa *rumkis malt,* kinywaji alichokienzi sana Maotad na kilichokuwa maarufu alikozaliwa. Yaani, watu wengi waliendelea kumuunga mkono kwa kipindi kirefu licha ya kuwa na asili tata kwani walitoka maeneo tofauti. Ingawa hivyo, walianza kukinaishwa na nyendo za Maotad na mwelekeo wao ukaanza kubadilika, walikuwa wamepata mwamko mpya. Hata kama wengi walikuwa wamejaribu kupambana kwa nia ya kubadilisha hali ilivyokuwa kama vile Bwana Kachuoheze, LiMioe, Amrao, Mastanji na Bwana $O_2$ na wakaambulia patupu, kundi la BORA lilikuwa na imani ya kupata ushindi baada ya Nuhu kuyapatanisha makundi ya akina Boyi na Amrao kwa lengo la kukabiliana vilivyo na Maotad.

Akina LiMioe waliendeleza mikutano yao Haponaseremwige mbali na kutatizika katika uteuzi wa kinara mkuu. Ni wadhifa uliohitaji mtu mmoja, kama ambavyo fahali wawili hawawezi kukaa katika zizi moja. Ni suala lililohitaji masikizano na uelewano, Boyi alikuwa wa kwanza kumpendekeza LiMioe kuwa kinara kwa sababu alikuwa mzee. Alikuwa radhi kufanya hivyo kwa masharti. Kwanza ingawa wangeshinda, alitaka kuwa makamu wa LiMioe. Pili, LiMioe aushike uongozi kwa kipindi kimoja tu, na kipindi cha pili ang’atuke na kumwachia yeye. Tatu, alitaka masharti haya yaandikwe chini, kutiwe sahihi baina yao kwa kuchanjana chale kwa

kutumia damu (uk 142-143). Kulitokea kutoelewana ambapo LiMioe alidai kuwa watumie kalamu nyekundu badala ya damu katika kutia sahihi na kuwa kipindi cha kwanza kilikuwa kifupi na hivyo alipendelea akubaliwe kuendelea kidogo, jambo ambalo lilikataliwa vikali na Boyi na Fadhila. Ili kufaulisha masikizano kati yao, Nuhu, mpatanishi wao aliwahimiza wawe na stakabadhi ambayo ingekuwa shahidi kuwa wote wamekubaliana na ndiposa wakaafikiana watumie kalamu nyekundu badala ya damu kutia sahihi mkataba wao.

Ili kukabiliana vilivyo na Maotad, Amrao na wenzake walikubali kujiunga na kundi la BORA kwa masharti kuwa watapewa majukumu yaliyo sawa na wala sio nafasi duni. Kwa ufupi, walitaka madaraka yagawanywe katikati ili kuwepo na usawa kwa kila jambo. Licha ya vuta nikuvute za hapa na pale, walikubaliana kuwa wakishinda, LiMioe awe kinara mkuu wa kundi, Boyi awe naibu wa kinara, Amrao awe msaidizi mkuu wa kinara, Fadhila awe naibu wa msaidizi mkuu wa kinara naye Kamu awe naibu wa pili wa kinara. Iwapo sheria za NUKA kulingana na katiba ya wakati huo hazikukubaliana na mamlaka ya Amrao, Fadhila na Kamu, LiMioe aliwahakikishia kuwa mamlaka hayo yangeidhinishwa katika muda wa siku moja mara kumi na kumi, yaani miezi mitatu na siku kumi hivi.

Kila jambo waliloafikiana walilipiga msasa wenyewe, hata baada ya maafikiano fulani wengi hawakutosheka, walitilia shaka lolote lile waliloonelea kutokuwa na imani nalo. Mathalani, baadhi kama Amrao walikerwa na Azimio hilo kwa kuwa maneno husika yalikuwa na vyanzo vya NI na TU na kwa sababu hiyo, walihisi kuwa Azimio hilo lilirejelea mtu mmoja. Hata hivyo, Azimio lilitiwa katika sefu na kufungiwa baada ya kukubaliana na maoni ya LiMioe kuwa yale yalikuwa makosa ya uchapishaji na kuwa hawakuwa na muda wa kuyarekebisha. Muungano huu uliibua chuki kati ya Maotad na wale walioasi NUKA kama Avadi kwa kujiunga na BORA. Kwa ajili hii, Maotad alimtisha vikali Avadi huku akimtaka aasi BORA na ajiunge na NUKA mara

moja la sivyo aende jongomeo. Alimshurutisha pia alipe deni la shilingi bilioni saba alilolipata kutokana na mafamba na kumuahidi nafasi ya makamu akikubali kuasi BORA, cheo alichotunukizwa pindi tu alipoitikia hewala kwa masharti ya Maotad ili kusalimisha maisha yake (uk 147-157).

Makundi yote yaliendelea kujisifu kwa ubora wao huku yakishutumiana na kuchafuliana jina katika tafuta tafuta zao za 'chakula' kwa wakazi mbalimbali. Maotad kama ilivyokuwa kawaida yake aliendelea kumwombea 'chakula' U na kuwahimiza wakazi kupuuza propaganda za kundi la BORA. LiMioe alionekana na kundi la NUKA kama mzee tofauti na U aliyekuwa kijana barobaro naye Amrao alionekana kama mtu ambaye alibadilishabadilisha uaminifu wake. Kundi la BORA nalo lilidai U alikuwa ni mwanagenzi katika masuala yaliyohusu wakazi wa Bikerani-Msiige, walisema kuwa babake U, Jokaga alishiriki mafamba na hivyo damu yake U ilitiririka mafamba. Waliamini kwamba, Maotad alimsukumia U kuwa kinara wa NUKA ili amhami kutokana na tuhuma za kushiriki sera ya mafamba, uk 167-8.

Ghasia zilitapakaa kila mahali, mara utulivu mara shamrashamra na mara ajali. Ajali iliyomkumba LiMioe na iliyoibua hisia za huruma kwa LiMioe na chuki kwa Maotad ni ajali iliyotokea wakati kundi la BORA lilikuwa limetoka kuomba 'chakula' katika makutano ya barabara ya kuelekea Kar Pir Mang'ich kutoka Nzambani, mahali kulikokuwa na chakula adimu (uk 168). Baada ya ajali hii, LiMioe aliendelea kuumia na maumivu makali hospitalini huku kundi la U likifurahi sana. Ingawa nia yao kuu ilikuwa ziraili amalize kadhia na LiMioe haikufanyika hivyo. U basi hakuwa na budi ila kukabiliana na LiMioe, mapambano ambayo yalingojewa na kila mtu akiwemo ziraili. LiMioe alishindwa kuendelea na shughuli ya kutafuta 'chakula', akiwa hospitalini, Amrao, Saigeo, Kajo, Fadhila, Boyi, Damisi, Kamu na wengine katika kundi lao waliendelea kukutana na wakazi huku wakieneza siri ya sumu ya NUKA kwa

sababu hakuweza kutoka pale kitandani alikolazwa kwa maumivu, mambo yalikuwa yamemwendea mrama.

Makundi yote yalitembelea wenye mamlaka na wanaoishi katika madongoporomoka, walivuka milima na mabonde, walitumia magari yao katika njia zilizosonga. Makundi yote yaliwashirikisha watu mbalimbali kama vile wahubiri na wanamuziki. Ni vita vilivyoendelea baina ya magazeti na vyombo vya habari. Kundi la BORA lilikuwa na lengo la kuzika mafamba na kuwaweka hadharani watu walionyakua makaburi, mashamba, mito, maziwa, nyumba, barabara na misitu. Mathalani, walinda usalama usiku walisemekana kushiriki na wahalifu kuwaua watu usiku kuvunja mabenki, kuiba magari, uendelezaji wa biashara haramu ya mbao, unajisi wa wanawake na wasichana wadogo na ubakaji wa watu wakati wa mchana (uk 171-173). Siku ya mwisho ya mkutano wa kundi la BORA, uwanja ulikuwa umefurika furifuri kiasi cha kutokuwa na nafasi hata ya kutema mate ama ya kutua sindano. Mkutano ulikuwa na sampuli yote ya viumbe wenye uhai, watu kutoka ngambo na mijini walifika, kuna waliokaa chini, juu ya mabodi ya magari na wengine kwenye miti. Ingawa kulikuwa na kundi la wenye nia mbaya na nzuri, wenye kutaka kujenga na kuimarisha imara hali za maisha, dalili ya kuzaliwa kitoto kipya, yaani kupatikana kwa kiongozi mpya ilibainika waziwazi (uk 176-180).

Tarehe 12/27/2200, tarehe iliyotengewa siku muhimu ya kuamua nani kati ya U na LiMioe ilifika. Watu walipeleka 'vyakula' vyao katika vituo vya kuvikusanya, kulikuwepo na wageni kutoka sayari nyingine waliokuja kushuhudia siku hii. Sababu ni kuwa katika miaka ya awali, waliopata 'chakula' kidogo walisemekana kupata kingi na wenye kukipata kingi walisemekana kupata kidogo sababu ya mafamba. Hivi kwamba, aliyekuwa ameshindwa alishinda na aliyekuwa ameshinda alishindwa na kuwa aliyedhubutu kukata rufani, rufani hiyo ilitokea kuwa kifo. Mafamba ilibatilisha ndiyo kuwa hapana na hapana kuwa ndiyo (uk 180-181). Baada ya

'treya' kuhesabiwa, LiMioe alikuwa amepata ushindi mkubwa na Boyi akawa makamu wake. Taarifa hii ilipokelewa na U kwa unyenyekevu mkubwa huku akiirejelea shughuli yenyewe kuwa ya haki na huru na akaahidi kushirikiana na utawala mpya wa LiMioe. Ni ushindi uliopokelewa na wengi kwa furaha, shangwe na nderemo, yalikuwa matokeo yaliyohamasisha makundi ya wanyonge katika sehemu nyingi za Karifa kwani hakuna aliyeamini Maotad angesalimu amri bila tetesi yoyote. LiMioe aliwakikishia wanasayari kuwa mafamba yangezikwa na kuwa utawala wake ungekuwa tofauti kabisa na uliotangulia.

Hata hivyo, baada ya muda mchache, tetesi kwamba viongozi walikuwa wameteuliwa kinyume na ahadi ya kundi la BORA zilianza, kulisemekana kuwa watu kutoka eneo moja la sayari ya BORA walipata nyadhifa nzito na muhimu. Huu ulikuwa wakati ambapo Boyi alikuwa akipoteza nguvu mara kwa mara kutokana na ugonjwa wa figo uliopelekea aende katika sayari moja ya nje kwa matibabu ambapo ziraili alimwandama na akaenda zake jongomeo, jambo lililosababisha huzuni tele kwani alifahamika kama sauti ya wenye dhiki. Kwa hivyo, Damisi aliteuliwa mahali pake, tendo lililozua tetesi zaidi kwa sababu LiMioe hakukumbuka maagano ya kundi la BORA la kutoa nafasi kuu kwa waasisi wake. Vilevile, LiMioe hakufaulu kuwapa wanasayari wote karatasi muhimu, yaani katiba kwa siku kumi mara kumi kama alivyoahidi licha ya wakazi kutoa mapendekezo yao kuhusiana na mambo kadha waliyotaka yafanyiwe marekebisho kama dini, ardhi, uhuru wa wanawake, mamlaka ya kinara wa BORA na wasaidizi wake na uenezi wa utawala mashinani.

Hata hivyo, mawazo haya yalikusanywa na kuwekwa pamoja kama stakabadhi iliyojulikna kama Azimio la nyumba. Kwa kuwa kundi lililopinga lilliliona Azimio hilo kuwa na walakini kwani hawakuridhika na maamuzi yaliyoafikiwa, ukarabati zaidi uliendelea na ukasababisha kuzuka kwa uhasama kati ya makundi haya mawili. Wenye kupinga walidai kuwa mamlaka ya kinara wa

BORA yalikuwa mengi zaidi na kuwa baadhi ya mamlaka yapewe msaidizi mkuu wa kinara. Hawa walituhumiwa na kundi lililounga kwa kutaka kuanzisha utawala wa kiimla na kutwaa madaraka kwa njia zisizo halali. Tofauti katika stakabadhi ya Azimio la nyumba ilivunja umoja wa sayari ya BORA na juhudi za wengi za kuzisuruhisha hazikufua dafu. Wivu, chuki, stihizai, njama, maandamano, matusi, mikutano ya siri, tandabelua, utanguaji sheria, ghasia, zilijenga kuta baina ya viongozi na watawaliwa. Ikawa ni mizozano na kizungumkuti cha kila siku katika sayari ya BORA iliyosababishwa na kutopewa kwa Amrao kile alichoahidiwa. Kamati nyingi zilivunjwa baada ya pande zote mbili kukosa kuafikiana, viongozi wa kidini pia walitoa mapendekezo yao ambayo pia yaliambulia patupu. Marekebisho mengi yalifanyiwa Azimio la nyumba na kuibua Stakabadhi mpya ya Siri ya Mbuyu iliyompa kinara wa BORA mamlaka mapya na mengi zaidi. Tendo hili lilisababisha maasi makubwa miongoni mwa viongozi ambao walianza kumpinga hadharani LiMioe na kumtusi pasi na kujali kuachishwa kazi na kwa njia hii sayari ya BORA ikapasuka katikati (uk 85-9).

Kuzaliwa kwa BORA kuliua mafamba, ufisadi, ulanguzi na maovu mengine mengi ila tu muda mrefu haukupita kama mambo haya hayazaliwa tena. Wananchi walianza kuingiwa na wasiwasi lakini nyoyo zao zilitulizwa na Mzee Twajua, mwanakijiji wa Tuga Amor. Aliwaelimisha na kuwahamasisha kuhusiana na maovu yaliyotekelezwa na viongozi wa NUKA kama mafamba ya mfuko wa vito yaliyohusishwa na Bwana Paka na yaliyojitokeza kwa sura mpya ya Angolalasting iliyohusishwa na Engineer katika sayari ya BORA. Alitumia muda mwingi kuwaomba watumie kura zao vizuri wakati wa uchaguzi kwani hiyo ndiyo iliyokuwa silaha pekee ya kuwang'oa viongozi kama hao mamlakani. Licha ya kuwepo kwa viongozi wapenda maendeleo na uwazi kama Jogi, afisa mkuu aliyeteuliwa na LiMioe ili kuzima mafamba, mwandishi anatudhihirishia jinsi juhudi zao watu kama hawa hugonga mwamba kutokana na

utawala mbaya na kwa namna hii wengi hutorokea sayari za mbali ili kuokoa maisha yao kutokana na chuki inayoelekezwa kwao. Kwa mintarafu hii, ingawa Jogi alijaribu kufichua maovu ya Engineer, jitihada zake ziliambulia patupu kwani aliogopa ukatili wa viongozi wakuu na hivyo ili kusalimisha maisha yake, akatorokea sayari za mbali. Licha ya matumaini mengi ya wanasayari, machafuko yaliendelea kuzidi kama vile umaskini, kukosekana kwa dawa hospitalini, barabara mbovu na kadhalika. Ni mambo yaliyowatia uchungu moyoni mwao kwani hawakupata mabadiliko waliyotarajia baada ya kuutimua utawala wa NUKA.

Wakati wa kupigia debe Azimio la Siri ya Mbuyu, kundi la LiMioe lililotumia ishara ya mumbi lilishindwa na kundi la Amrao lililokuwa na ishara ya njiwa. Hali hii ilisababisha uhasama na chuki baina ya viongozi wa BORA huku athari za matokeo haya zikiwa kupigwa kalamu kwa baadhi ya viongozi na kudhoofika kwa kiwango cha maendeleo kiuchumi, kielimu na usalama, huku uharibifu wa mali na ufisadi ukikita mizizi. Kutoelewana na kutosikizana kati ya viongozi wa BORA kuliendelea hadi mwisho wa kipindi cha uongozi cha LiMioe ambapo, uamuzi wa wananchi kupitia kwa debe kulibainisha waliopendwa na wasiopendwa. Shughuli hii iliyotengewa tarehe 12/27/2700 ilikuwa na athari mbaya na nzuri katika historia ya wanajamii. Ni mapinduzi yaliyobainisha kukombolewa kwa wanajamii ambapo vigogo wengi waliondolewa mamlakani. Aidha, kulizuka vurugu katika baadhi ya sehemu nchini kwani haikujulikana kama aliyeshinda alikuwa LiMioe au Amrao. Machafuko ya aina yote yalitokea, mathalani mapigano yaliyosababisha maafa ya wengi, kuchomwa kwa nyumba, mashamba na mali taslimu, mali ya nchi ikaharibiwa, damu ikamwagwa, chuki na uhasama ukaenea baina ya makabila. Mafarakano haya yalichukua muda kuisha hadi pale LiMioe na Amrao walipokubali kugawana madaraka, maafikiano yaliyofaulishwa na juhudi za mwanasayari wa nje na mkataba ukatiwa sahihi na kushuhudiwa na sayari zote tarehe 2/28/2800. Kufikia tarehe 4/13/2800, sayari ya BORA

ilizaliwa upya na viongozi wapya na mipango yote ya ukombozi ikafanyika Haponaseremwige. Baada ya mapatanisho haya, jukumu la wanajamii likawa ni kuomba Mungu ili maafikiano hayo yadumu milele.

## 2.2 Hitimisho

Katika sura hii, tumeelezea msuko wa riwaya ya *Mafamba*. Kwa kufanya hivyo, tumeweka msingi wa uelewa kuhusiana na kisa chenyewe, tendo ambalo litatuwezesha kuchambua nafasi ya uchimuzi katika kiwango cha wahusika na matumizi ya lugha. Kutokana na mtindo wa uwasilishaji, ni dhahiri kuwa hii ni riwaya ya kimajaribio au mpya.

Ni hadithi inayohusu historia ya Kenya katika kipindi cha mwisho cha utawala wa Moi na madhila mbalimbali waliyopokea wananchi wakati chama kikuu tawala cha KANU kilienziwa na wengi kwa takriban miaka 40 kabla ya chama cha upinzani kupata ushindi. Aidha, ni hadithi inayoelezea kipindi cha utawala wa Kibaki wakati chama cha NARC RAINBOW kilipata ushindi mkubwa dhidi ya chama cha KANU. Huu ni wakati ambapo wananchi walitarajia mageuzi makubwa katika uongozi lakini matamanio yao yaligonga mwamba baada ya hali ya uongozi kubadilika muda mfupi tu baada ya Kibaki kuingia ofisini. Hali kadhalika, mwandishi anagusia mwanzo wa kipindi cha utawala wa serikali ya muungano kati ya Kibaki na Raila baada ya kutokea kwa machafuko makali nchini. Masuala na maudhui yanayojitokeza katika kisa hiki yanabainika sio tu hapa nchini bali katika mataifa mengine.

# SURA YA TATU

# UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA WAHUSIKA

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ya tatu, tunahakiki nafasi ya uchimuzi katika kiwango cha wahusika. Huu ni uchimuzi unaodhihirika katika kiwango cha maana au cha kisemantiki. Kulingana na Baldic (2001:70), neno wahusika lilitokana na kazi ya Theophratus, *'The Characters,'* katika karne ya tatu kabla ya Kristo. Wahusika kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:45) hubuniwa kutokana na mazingira anamoishi msanii ambayo huweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, wanaotambulishwa na mhusika au msimulizi na huwakilisha sifa tofauti zinazobainika kupitia kwa matendo yao. Kwa mintarafu hii, iwapo wahusika ni viumbe au watu, wao huakisi sifa na tabia za kibinadamu katika jamii husika kwa namna wanavyotumia lugha kulingana na tajriba yao na hivyo, kuwafanya wenye msimamo thabiti na wa kuaminika. Dhima kuu ya wahusika katika kazi ya kifasihi ni kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa kushirikisha matendo yao, hisia, mazungumzo na mawazo yao. Wao hudhihirisha wasifu wa binadamu katika hali halisi kwa kuwa wanawakilisha binadamu wa kawaida. Pia, wao huwa nguzo kuu ya kusukuma hadithi mbele.

Katika kuangazia uchimuzi wa wahusika katika kiwango hiki, tutabainisha jinsi wahusika mbalimbali walivyosawiriwa kiasi cha kubatilisha dhana nzima ya wahusika hata ingawa matendo yao na wasifu wao unachukuana na hali ya kisasa ya maisha ya jamii. Haya kwa

kawaida ni maisha yanayobadilika kila uchao na yanayooana na malengo na matumaini ya wanajamii. Kupitia kwa migogoro ya kisiasa katika riwaya ya *Mafamba*, maendeleo ya wahusika kisaikolojia, mitagusano na wahusika wengine, tutabainisha upekee na umuhimu wao katika uendelezaji wa riwaya hii kwa kuonyesha sifa bainifu zinazojitokeza au kuchimuzwa. Katika maingiliano yao na wanajamii, wanabainika kama wanadamu walio na uwezo wa kuyapokea, kuyakubali au kuyakataa mawazo ya watu mbalimbali kuzingatia viwango vyao vya uelewa na mwamko na kutegemea uzito na wepesi wa ujumbe husika. Uhusika wa jadi ulijengeka kwenye uhalisi wa kijamii ambapo wahusika walikaribiana na wanadamu katika ulimwengu halisi. Mathalani, wahusika wakuu walikuwa na ujasiri na nguvu za kiajabu na walitambuliwa kwa urahisi kutokana na sifa za kiadilifu, hamu ya kutimiza malengo yao bila kufa moyo, nguvu za kiungu na majaribu ya ajabu kama alivyokuwa Fumo Liyongo.

## 3.1 WAHUSIKA WAKUU

Wahusika hawa wanatawala kazi ya kifasihi, wanahusika katika utendaji wa matukio muhimu na wanawakilisha dhamira na maudhui ya kazi husika. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:41), wahusika hawa huwa na dhima ya kuisukuma riwaya mbele kwa sababu migogoro na matendo yote muhimu inawahusu. Wao hushiriki katika matendo na migogoro muhimu katika kazi kwa njia inayothibiti msuko wa matukio makuu na visa au vitushi huzunguka maisha yao. Katika kiwango hiki kuna wahusika sita wakuu, Maotad, LiMioe, Amrao, U, wakazi wa Bikerani-Msiige na Mzee Twajua. Ndio nguzo kuu ya riwaya hii kwani matendo na migogoro muhimu inawahusu. Mwandishi aliwaumba wahusika hawa ili kuchimuza ukweli kwa wasomaji kuhusu mienendo yao.

### 3.1.1 MAOTAD

Maotad alikuwa kiongozi wa sayari ya NUKA, sayari ya zamani sana iliyoumbwa yapata miaka 4000 iliyopita wakati muumba aliumba Karifa. Hii ilikuwa sayari maarufu kuzidi nyingine zote kutokana na vitu vingi vyenye kuvutia kama vile matapishi, hewa mbaya, mbwedu, dondandugu, uvimbe na zaidi mafamba. Sifa bainifu za sayari hii zinachimuzwa kwa lengo la mtunzi kutupa ithibati tosha kwa uwazi kuhusu sayari hii ambayo iliongozwa na Maotad. Kutokana na ufafanuzi huu, uozo katika sayari hii unadhihirishwa, ni uozo unaoandamana moja kwa moja na tabia za Maotad kama itakavyobainika.

Jina lake maarufu lilikuwa Aende na liliibuka kutokana na tabia ya wakazi wa Bikerani-Msiige ya kumwamrisha aende kila mara. Alipendwa sana na alikuwa maarufu kwa wale ambao haja zao zilitimizwa na kukidhiwa tofauti na ilivyokuwa kwa wakazi wa Bikerani-Msiige waliomchukia kwa kuwa mahitaji yao hayakutimizwa. Alikuwa na umri wa miaka 720 ambapo alikuwa ametawala kwa miaka 400 na wala hakutishika wala kuliona kama jambo zito, kwake ilikuwa tu kawaida (uk 5-6). Tunajuzwa kwamba alipotakikana aende, alijihisi kijana wa miaka 720 tu kwani kuna wengine katika sayari nyingine walioishi takribani miaka 1440, nusu ya miaka yake. Kwa namna hii, mwandishi anachimuza kwa wasomaji jinsi Maotad alivyokuwa hapendwi na watawaliwa kiasi cha kumbandika jina la kimajazi lililoashiria kukinaishwa kwao naye. Aidha, tunapata kuelewa alivyokuwa na miaka mingi na alivyokuwa ametawala kwa muda mrefu sana ingawa yeye aliliona kama suala la kawaida akijilinganisha na watawala wengine aliowafahamu.

Maotad alikuwa kama shetani na aidha kama mnyama wa futi saba na aliyesifika katika sayari zote kwa sifa ya ugeugeu. Alipotazamwa, alionekana kana kwamba ni kiumbe mmoja ila kwa

kumchunguza kwa ufasaha, alibainika kama kiumbe tofauti hasa katika kuwapokea wageni mbalimbali. Alionekana kuwa kiumbe mzuri mwenye kuyajali maslahi ya watu ila alikuwa tofauti katika kuwapokea wenye dhiki, wenye haja na wenye kunywa maji matamu. Hali kadhalika, sifa yake ya ugeugeu inachimuzwa kwa jinsi alivyoyakana maneno aliyoyazungumza hata baada ya kuyasema kwa muda mfupi. Angesema alinukuliwa vibaya na mashetani waliojizatiti kumchafulia jina na ambao aliwaona kama ibilisi waliojifanya binadamu, hawa walikuwa LiMioe, Boyi, Sinya na Fadhila (uk 89).

Maotad alikuwa kiumbe aliyebadilika na kuwa kiumbe wa kutisha hasa alipopokea changamoto kutoka kwa wapinzani. Alikataa kutoka 'chumbani' pindi tu LiMioe, mwanasayari wa PiDi alipotaka kuyanywa maji matamu kwa kuwa alikuwa na uchu wa kuzileta sayari zote pamoja bila ya ruhusa ya Maotad. Hili lilimfanya Maotad abadilike na kuwa kiumbe wa kutisha, mabadiliko ambayo yalichukua miaka 200 (uk 6). Hata hivyo, tunajuzwa kuwa katika miaka ya mwanzo 100, Maotad alikuwa na uhusiano bora na Arijojo, Amrao na hata LiMioe. Katika kipindi hicho, hata wakazi wa sayari ya NUKA walimpa sifa teletele kwa utawala wake mzuri uliofanya sayari hii kunukia kabla ya kuanza kukorofishana na binadamu mbalimbali. Tamaa ya Maotad inachimuzwa, yeye kamwe hakutaka kuyaacha 'maji matamu' au matunda yaliyoandamana na uongozi wa nchi, nia yake ilikuwa kuyanywa milele na milele bila kuwajali wengine waliokuwa na ndoto ya kuyaonja. Atambuapo kuwa watu kama LiMioe walinuia kuyaonja, tabia yake inabadilika ili kuubana uhusiano wa karibu nao kwa lengo la kuficha na kuzuia siri zake kufahamika.

Aidha, Maotad alikuwa kiumbe wa kutisha na kuogofya kwa namna ambavyo macho yake yalikuwa makali, meusi na yaliyofanana na miale ya jua kwa uangavu. Iliaminika kuwa macho haya yake yalikuwa na uwezo wa kumulika na hali kadhalika kupenya mbavu za mwathiriwa

yeyote yule. Hali hii yake ya kuogofya na kutisha iliaminika miongoni mwa wakazi wa Bikerani-Msiige kuwa ndiyo iliyomwangamiza Rojoo, mkazi mmoja wa sayari ya NUKA hadi akakata roho. Licha ya Rojoo kuwa mashuhuri, asiyetisha kwa namna yoyote ile na kuwa binadamu aliyemtii Maotad na sheria zote katika sayari ya NUKA, jambo lililotisha ni jinsi kifo chake kilivyotokea. Ilisemekana kwamba alikata kamba baada ya kula chapati moja na vipande saba vya nyama ya ng'ombe ambavyo kamwe havikutiwa sumu. La kushangaza ni kuwa Maotad alishikilia kwamba chakula hicho kingekuwa na sumu Rojoo hangekufa. Hali hii inachimuza uozo wa kimaadili na unafiki unaowaandama viongozi barani Afrika kutokana na tamaa yao ya kutaka kuendeleza daima mafamba. Ingawa Maotad alidai kwamba mahasidi wa NUKA kama Amrao ndio waliosababisha kifo hiki wakati alipoulizwa, baadaye vifo vingi vilitokea vya namna hiyo hiyo na jibu lake kama kawaida likawa chapati moja na vipande saba vya nyama ya ng'ombe visivyotiwa sumu (uk 7). Mwandishi anatudhihirishia hali ilivyo kwa uwazi, badala ya viongozi kuwa mfano mwema kwa watawaliwa, wanakuwa vikwazo katika uendelezaji wa taifa kwa kuwaangamiza wananchi chipukizi ambao wamejaa imani na matumaini ya kubadilisha sura za jamii zetu. Maotad ni mfano wa kiongozi barani Afrika aliyejaa ukatili, aliyewaangamiza wananchi ambao nia yao ilikuwa kuleta mabadiliko na aidha tunatambua jinsi uchunguzi wa maangamizo yao hugonga mwamba kutokana na utawala mbaya.

Wakati wa mjadala juu ya mafamba, Maotad anasemwa kuwa kwa niaba ya wenyeji alicheka kicheko kirefu, kicheko kilichosababisha wajitapikie ovyo na hali kadhalika kufanya matapishi yao kuvichafua viatu vya wageni waliozuru NUKA. Wakereketwa wake kwa sababu ya imani yao juu ya mafamba, walimtungia wimbo wa kuwajuza wakazi wa Bikerani-Msiige, Amrao, Arijojo na LiMioe kuwa sera ya mafamba ingedumu daima. Huu ni wimbo alioupenda sana Maotad na aliojua kuuimba kwa ufasaha. Kwa mujibu wa Maotad, mafamba ilikuwa hali ya

maisha, aina ya dhehebu na iliendeleza maendeleo katika sayari ya NUKA kama ujenzi wa barabara na kusababisha mvua kunyesha. Sera ya NUKA chini ya Maotad iliongozwa na mafamba iliyohusishwa na mnyama, yaani ndumakuwili mkubwa aliyekuwa takriban na urefu wa futi 400. Mbali na sera ya mafamba kuendelea kushamiri na hata kuenea katika sayari mojawapo ya kusini mwa Afrika, NUZAPIFU, wakazi wa Bikerani-Msiige, wanasayari ya DiPieLi, PiDi na DiPieNi walishikana mikono kuikashifu. Kwa namna hii, tabia ya Maotad ya kuabudu mafamba inajichimuza, tabia ambayo aliambukiza hata wageni waliomzuru na kwa sababu hii, hawakupata kuuweka ukweli wazi kwa wananchi kuhusu mienendo yake potovu kwa kuwa pia wao walivutiwa na kunufaika kutokana na mafamba.

Maotad alipenda kucheka sana hasa sera ya mafamba ilipotetewa kuwa nzuri na yenye kuleta mabadiliko, kwa mara nyingine anaangua kicheko kilichoendelea kwa miezi minne (uk 90). Hali inayochimuza uozo uliokita mizizi katika utawala wa Maotad, aliamini kuwa alikuwa na uwezo wa kuendeleza mafamba licha ya juhudi za kundi la BORA aliloliona kama lisilokamilika, lisilokuwa na uwezo, lililojaa watu wasiokuwa wazalendo na wenye kubadilisha misimamo kama lumbwi.

Maotad alikuwa mwepesi wa kutambua sauti, za hatari na zisizo za hatari. King'ora kinapotoa sauti, anaitambua kuwa ya hatari, hatari ambayo haikuashiria mahitaji ya wenyeji wa NUKA. Kwa mintarafu hii, alitaka kuwaalika wenyeji wa sayari nyingine ili aweze kuikabili hatari iliyomwandama. Sababu ni kuwa, sayari ndogo ambazo hazikuwa na watu wengi zilinuia kuungana ili kuipinga sera ya mafamba. Kwa kuwa tafrija za baada ya miaka 500 zilikuwa zimekaribia, maombi yake yalikuwa kuwa mwingine apate kukabiliana nazo kwa kuwa rabsha za aina hiyo zilikuwa zimemchosha. Ingawa mwepesi wa kutambua mahasidi wake, tabia yake ya kuwa na woga inachimuza kwani hata baada ya kuungana na Amrao aliogopa kung'olewa

mamlakani. Ndoto ya kijinamizi inayompata, inamfanya atishike, aathirike mwili na kufikia mwishoni mwa ndoto anatokwa na jasho jingi licha ya kuwepo pangaboi mle ndani. Kwa jinsi hii, sakafu ililoa maji, ikaota kijito chembamba kilichotoweka kupitia kwa ufa ukutani, moyo wake pia uligonga mara saba zaidi ya kawaida kwa kumuona Amrao ndotoni akiwaongoza akina LiMioe na akiwa na sumu licha ya wao kushirikiana (uk 62-63).

Sifa ya Maotad ya ubinafsi inachimuzwa, yeye ndiye aliyekuwa na ufunguo wa kukifungua chumba cha Shashamame kilichokuwa na kiti muhimu na ambao alikuwa ameumeza miaka 40 iliyopita. Juhudi za madaktari kutoka Biandi hazikufua dafu licha ya harakati zao za kujaribu kuutoa tumboni mwake kwa kumfanyia upasuaji. Mbali na kujizatiti mara kadha kwa kutumia nguvu ili angaa wapate kuuchukua huo ufunguo, walishindwa. Aidha, ubinafsi wake unabainika kwa jinsi alivyojipenda na kulimbikiza vitu mbalimbali vilivyomfurahisha katika sebule yake bila kuwajali wakazi wa Bikerani-Msiige ambao hawakuwa na chochote. Sebuleni palipokuwa na kiti cha enzi alipokaa palikuwa na vitu vingi vilivyotokana na mafamba kama vile zulia, mishumaa, kalamu, mafaili, viti, tarakilishi, chopasa na hali kadhalika harufu nzuri ya kuvutia. Nzi, yaani watu waliopatikana mle ndani waliimba wimbo wa mafamba na walihakikisha kwamba sera ya mafamba ilihalalishwa katika sayari ya NUKA. Kwa mintarafu hii, vigogo wafuasi wa Maotad walikuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba mali ya umma yalitumiwa kwa njia ambayo ilimfanya ajihisi mtukufu na mwenye enzi katika ufalme wa Karifa bila kukosa chochote kilichokuwa na thamani. Ni hali ya viongozi barani Afrika ambao huongozwa na tamaa ya kujilimbikizia mali ili watambulike kama matajiri badala ya kugawa baadhi ya mali hiyo kwa maskini kwa kuwasaidia kufungua biashara ama kuanzisha miradi ambayo inaweza kuwafaa maishani na kuinua hali yao ya maisha.

Maotad alikuwa mwenye hamaki na mshurutishaji, sifa inayochimuza katika uk 154-156. Avadi anaposita kuyajibu maswali yake kama vile sababu ya kuasi BORA, ingawa angekubali kuwa makamu wake baada ya kurudi NUKA na iwapo alikuwa radhi kulipa deni la shilingi bilioni saba, Maotad anaitisha askari wake bastola ili amuue. Anahesabu moja hadi saba kumpa nafasi ya kujibu kwa masharti kuwa kama hakujibu maswali yake basi aifyatue risasi. Sababu ya mori, anampiga mateke kadha yaliyoiharibu sura yake. Moja lilimpata kitovuni na kumwangusha katika kona ya sebule walimokuwa, la pili lilimfanya aangukie kalafati iliyokuwa katika kona nyingine ya sebule ile. Ghadhabu hazikuisha, alimkimbilia, akamnyanyua na kumpiga kidevu kwa goti lake mara tatu na damu ikaanza kumtiririka. Aidha, alichukua chupa ya *rumkis malt* akamgonga nayo kwa nguvu hadi akatokwa na damu mdomoni. Hili lilimfanya Avadi alie kwa kite na akubali masharti yote na kwa hivyo Maotad akamteua kuwa makamu wake.

Alikuwa mtawala mbaya kwa kuwa katika kipindi chake cha uongozi, aliweza kuwadhulumu wengi waliotoa hotuba zao katika Come-K, mahali pa kisirani kulikopelekea yeyote aliyetoa hotuba huko kupelekwa Mkanyageni (uk 124). Walioingizwa huko walitoka wakiwa maiti ama nusu maiti kwa sababu walikabiliana na hatari za aina nyingi kama vile mbwa koko, gesi ya sumu na risasi. Hawa walikuwa Mastanji, Charu, Bwana $O_2$, Jokaga, Tojombo, Kuka, Pange, Freku, Onachi na Bika.

Maotad hakuwa na msimamo, mara angesema anaunga mkono Azimio la siri ya Mwaujua Mbuyu, yaani kundi la mumbi na mara nyingine angekana na kusema aliunga mkono kundi la njiwa. Mara nyingine angejitetea kwamba kung'atuka mamlakani kama mtawala hakukuwa tikiti ya kumfanya asitoe maoni yake kuhusiana na msimano wake (uk 222). Alikuwa kiumbe wa ajabu ambaye angelisema kitu yapata saa mbili zilizopita na kukikana kwa dhati zote huku

Maotad alikuwa mwenye hamaki na mshurutishaji, sifa inayochimuza katika uk 154-156. Avadi anaposita kuyajibu maswali yake kama vile sababu ya kuasi BORA, ingawa angekubali kuwa makamu wake baada ya kurudi NUKA na iwapo alikuwa radhi kulipa deni la shilingi bilioni saba, Maotad anaitisha askari wake bastola ili amuue. Anahesabu moja hadi saba kumpa nafasi ya kujibu kwa masharti kuwa kama hakujibu maswali yake basi aifyatue risasi. Sababu ya mori, anampiga mateke kadha yaliyoiharibu sura yake. Moja lilimpata kitovuni na kumwangusha katika kona ya sebule walimokuwa, la pili lilimfanya aangukie kalafati iliyokuwa katika kona nyingine ya sebule ile. Ghadhabu hazikuisha, alimkimbilia, akamnyanyua na kumpiga kidevu kwa goti lake mara tatu na damu ikaanza kumtiririka. Aidha, alichukua chupa ya *rumkis malt* akamgonga nayo kwa nguvu hadi akatokwa na damu mdomoni. Hili lilimfanya Avadi alie kwa kite na akubali masharti yote na kwa hivyo Maotad akamteua kuwa makamu wake.

Alikuwa mtawala mbaya kwa kuwa katika kipindi chake cha uongozi, aliweza kuwadhulumu wengi waliotoa hotuba zao katika Come-K, mahali pa kisirani kulikopelekea yeyote aliyetoa hotuba huko kupelekwa Mkanyageni (uk 124). Walioingizwa huko walitoka wakiwa maiti ama nusu maiti kwa sababu walikabiliana na hatari za aina nyingi kama vile mbwa koko, gesi ya sumu na risasi. Hawa walikuwa Mastanji, Charu, Bwana $O_2$, Jokaga, Tojombo, Kuka, Pange, Freku, Onachi na Bika.

Maotad hakuwa na msimamo, mara angesema anaunga mkono Azimio la siri ya Mwaujua Mbuyu, yaani kundi la mumbi na mara nyingine angekana na kusema aliunga mkono kundi la njiwa. Mara nyingine angejitetea kwamba kung'atuka mamlakani kama mtawala hakukuwa tikiti ya kumfanya asitoe maoni yake kuhusiana na msimano wake (uk 222). Alikuwa kiumbe wa ajabu ambaye angelisema kitu yapata saa mbili zilizopita na kukikana kwa dhati zote huku

akisema alinukuliwa vibaya na mashetani. Hawa walikuwa LiMioe, Boyi, Sinya na Fadhila aliowaona kama ibilisi waliojifanya binadamu na aliamini walimchafulia jina (uk 89).

### 3.1.2 LiMioe

Alitoka katika jamii ya QiQu, alikuwa msahaulifu kwani alipoambiwa na Boyi kwamba asimrejelee Fadhila kama Chakangi Seconds, bado alimwita vivyo hivyo. Aidha alimdunisha kwani alimwona kama mtu ambaye hangeweza kusaidia kwa sababu alikuwa mwanamke, alimchukulia kama mama ambaye hangeweza kuchangia katika miradi yoyote (uk 34). Vilevile hakuwa na msimamo, sifa iliyofanya wengi wambandike jina la kimajazi, Tiara. Alikuwa ni kama tiara iliyokwenda huku na kule majira ya upepo. Hata hivyo, tofauti na tiara inayotegemea upepo, LiMioe alikuwa tiara ambayo ilienda kinyume na kunapotokea upepo, upepo ulipovuma kutoka kusini, yeye LiMioe angelielekea kaskazini. Yeye alikwenda dhidi na upepo tofauti na tiara na alikabiliana na mawimbi yenyewe bila kuogopa, hata ingawa yalikuwa makali kiasi gani. Sababu ya kufanya hivyo haikuwa kwamba alikuwa shujaa bali hakujua kama hali hizo zilikuwa hatari, yeye alijikakamua tu bila kutishika, alingoja dhoruba hizo kali ambazo zilimvunjavunja. Licha ya hivyo, hakukata tamaa bali alijipa matumaini kwamba siku moja angeibuka mshindi. Haya ni maelezo yanayochimuza harakati za LiMioe za kupigania uongozi dhidi ya Maotad, ushujaa, juhudi na matumaini aliyokuwa nayo tangu zamani ya kuwa angelimshinda Maotad siku moja.

Alikuwa na matumaini kuwa atamshinda U na hivyo hakuogopa kumkabili kwa kuwa alifahamu kuwa dawa ya moto ni moto. Alifanikiwa kupata ushindi katika tikiti ya BORA baada ya kushinda NUKA kwa asilimia kubwa. Hata hivyo, baada ya miaka michache tangu achukue usukani, alibadilika kama ilivyo viongozi wengi wa Afrika na kuendeleza utawala mbaya. Suala

linalochimuka katika uk 191. Tunajuzwa kuwa, baada ya baadhi ya wakazi wa Tuga Amor kuchapa mtindi uliowaletea madhara kadha, aliyehusika alikamatwa mara saba na kila wakati aliachiliwa huru kwa sababu ya sera ya nopro.

Ni kiongozi ambaye mara kwa mara alionyesha kutowajibika na kutojali. Ingawa alifahamu vizuri kuwa Azimio la Siri ya Mbuyu au la Mwaujua Mbuyu lilikuwa na walakini, aliwaambia viongozi wenzake walioiunga mkono watangaze uzuri wa sehemu za stakabadhi hizo zilizokuwa nzuri na kuwahimiza kutupilia mbali propaganda za wapinzani (uk 221). Hali kadhalika, aliidhinisha utumizi wa magari ya umma katika kampeni hii kwa kuwa ndiye aliyekuwa kiongozi kwa kusema kuwa ni magari rasmi ya BORA na kuwa hakukuwa na tashwishi yoyote wakitumia rasilimali za sayari (uk 218). Alisisitiza kwamba sehemu zilizojitokeza kama makosa zilitokea kwa sababu ya makosa ya kihijai na kutoeleweka kutokana na fasili tofauti.

Hakuwa mwangalifu, sifa inayochimuza katika uk 226. Anampa Amrao kanda ya maswali aliyoulizwa na Ngwena wakati wa mkutano wao wa siri kuhusiana na Azimio badala ya kumpa kanda yenye masuala ya ardhi na udongo na hivyo kuwezesha kundi la Amrao kufahamu walakini katika Azimio hilo.

LiMioe anadhihirika kama mtawala mbaya, ukweli unaochimuza wakati wa kupigia debe Azimio la Siri ya Mwaujua Mbuyu kwa jinsi alivyofuja mali ya umma kwa njia isiyofaa huku akipendelea zaidi waliounga mkono Azimio hilo. Katika uk 227-228 tunajuzwa jinsi wanajamii wa BORA walivyozawadiwa vitafunaji mbalimbali na viongozi wa kundi la LiMioe waliokuwa wanatafuta 'treya za vyakula' kutoka kwao. Yaani, waliokuwa maskini walipewa zawadi nono zilizowafanya kuwa matajiri huku wengine wakiahidiwa mambo tofauti ili waunge mkono mumbi tarehe 11/12/2500. Mathalani, eneo la Ma lilizawadiwa ardhi, la Ai likapewa kiwanda

cha nyama, la Fa likajinyakulia hifadhi kubwa ya wanyama nalo la Ao likalipiwa madeni yote. Watu wa Me waliahidiwa uwanja wa F-16, wa Ba nasari kubwa kuliko za wilaya mbili. Viongozi waliomsaidia LiMioe katika utawala wa mashinani waliokuwa na mamlaka ya chini kabisa katika utawala wake wakaongezewa mapato yao maradufu. Aidha kwa mara ya kwanza, watu walianza kumiminika na kuzuru makao rasmi ya BORA na kushauriana na LiMioe, nyendo ambazo zilikuwa maarufu katika utawala wa Jokaga na Maotad.

Kulingana na nyendo hizi, utawala wa LiMioe ukawa mbaya kupindukia licha ya dalili za maendeleo zilizokuwa zimeanza kubainika, hivi kwamba ulishabihiana kwa kiwango kikubwa na utawala wa NUKA. Ikawa ni vigumu kuweka mpaka kati ya utawala huu mpya na wa awali, mambo yaliyokuwa yakishutumiwa katika utawala wa NUKA yakajitokeza upya kwa sura ile ile katika utawala wa BORA. Kwa mujibu wa maelezo haya, ni wazi kuwa, viongozi katika Afrika wanapopata fursa ya kuongoza, wao hujizatiti kutekeleza wajibu wao katika miaka ya kwanza ya utawala wao na baadaye husahau sera zote walizokuwa watekeleze kwa minajii ya wananchi na maendeleo ya nchi. Wengi huingilia nyendo chafu kama za watawala wa awali wanaong'olewa mamlakani kwa kusababisha kuzorota kwa uchumi, elimu, afya na miradi tofauti ya uimarishaji wa nchi kutokana na ufisadi.

Hali kadhalika, alikuwa mwenye ghadhabu aliyefanya kazi kwa kuzingatia hisia zake za ndani, sifa inayochimuza katika uk 236-239. Mwelekeo huu wake wa kitabia ukawa chanzo cha kusambaratika kwa matumaini ya jamii kulikoandamana na matatizo chungu nzima. Neno kuwajibika likawa jipya katika orodha yake ya msamiati, akawa hajali tena, maisha ya wanajamii yakawa ni kutegemea kudura za Mwenyezi Mungu. Wanajamii walipokosa kuliunga mkono Azimio la Siri ya Mwaujua Mbuyu, alikasirishwa na matokeo haya yaliyolipa kundi la Amrao ushindi na kuwaachisha kazi wasaidizi wake wote ikiwemo waliounga mkono mumbi na njiwa

isipokuwa Damisi. Hawa walikuwa Amrao, Kamu, Saigeo, Sinya, Engineer, Fadhila, Bi. Zaraa, Kanje na wengineo. Kutokana na shughuli hii, alikivunja kikao cha jumba la mdahalo, yaani bunge kwa muda, muda uliopita akitafuta mawaidha kwa watu mbalimbali akiwemo Maotad. Aliwapiga kalamu Amrao, Kamu, Bi. Zaraa, na wengineo waliokuwa katika kundi la njiwa na aidha Engineer pekee wa kundi la mumbi bila kuzingatia ukweli kuwa baadhi yao ndio waliomsaidia kupanda katika wadhifa wa kinara wa BORA. Waliobahatika kuwa katika orodha mpya kama Fadhila, kiongozi wa KEFO na wengine walikataa nyadhifa zao kwa madai kwamba malatifu wao hawakupewa haki zao. La kushangaza ni kuwa kiwango cha elimu cha wasaidizi wapya hakikuzidi masomo ya shule ya chekechea, yaani hawakuwa wamesoma sana. Utawala wa LiMioe ulianza kuyumbayumba kutokana na fitina za watu mbalimbali wakiwemo viongozi kutoka maeneo alikozaliwa. Matatizo mengi yalianza kuikumba sayari ya BORA kama vile ukame uliosababisha sayari hii iagize chakula cha msaada na hali kadhalika mafamba. Matumaini ya BORA *yalianza kudidimia huku kejeli tele zikitoka kwa sayari ndogondogo*, huzuni ilijaa kila pembe ya jamii na wala LiMioe hakuongea, alinyamaza tu bila juhudi za utatuzi wa shida hizo.

Alikuwa mpenda maendeleo, suala linalochimuza katika uk 229. Licha ya maasi mengi yaliyodhihirika katika utawala wa LiMioe kama ilivyokuwa utawala wa Jokaga na Maotad, kuna pia mambo mbalimbali yaliyotia fora. Mathalani, masomo ya bila malipo katika shule za msingi yalifanya sayari ya BORA kuwa na wanafunzi wengi zaidi katika shule za msingi ikilinganishwa na sayari nyingine. Jambo hili liliwawezesha waliokosa elimu katika utawala wa Jokaga na Maotad kupata fursa ya kuendelea na masomo yao katika enzi za LiMioe na kwa namna hii kwa mara ya kwanza, kukawa na wanafunzi wazee sana katika shule za msingi. Vilevile, ushuru uliweza kukusanywa na serikali ya BORA kwa uzuri ingawa watu kadha walikataa kulipa kama

vile ajuza wa Tuga Amor. Ingawa hivi, maendeleo machache yaliweza kuonekana wazi mbali na mivutano ya hapa na pale.

LiMioe alikuwa mbinafsi, alishikilia kwamba mkataba baina yake, Boyi na Fadhila uandikwe kwa wino mwekundu na wala sio damu kwani kulingana na hekima yake, damu ni nyepesi kuliko wino mwekundu na kuwa mkataba wa damu ungetibuka nao wa wino mwekundu ungesimama imara. Ni kana kwamba alijua atavunja maafikiano yao na kuwa hakuwa tayari kuandamwa na athari kali za kuchanjana kwa damu baada ya kuvunja mkataba wao, alionelea afadhali watumie kalamu na karatasi ambazo zingeibua athari ya kushutumiwa tu kwa kutotimiza maagano.

### 3.1.3 AMRAO

Alikuwa mwanasayari wa DiPieLi aliyekuwa na uchu mkubwa wa kuongoza ingawa baadaye alijiunga na kundi la BORA. Kutajika kwa Amrao wakati wa ushirikiano wa karibu na Maotad unachimuzwa katika uk 90, baada ya wote wawili kuzileta sayari za DiPieNi na NUKA pamoja. Amrao alisifika sana na kuwa kama mti au maua mazuri yapendezayo na kunukia, alikuwa kama mpambauke kwenye jua la asubuhi au kama waridi nyakati za asubuhi, alijiona kama mganga aliyepata jawabu la kitu fulani kilichomtatiza mteja yeyote aliyekwenda kwake kupiga ramli na hali kadhalika aliamini alikuwa na manufaa kama mti wa msegese.

Kwa sababu alitamani sana kuachiwa uongozi na Maotad, ilimbidi Amrao atafute njama za kumzima, hivyo aliibuka na mipango kadha. Mipango hii inachimuza jinsi wanasiasa wengi huchanganyikiwa wakati wa kampeni, jambo linalowafanya wafikiri mambo tofauti yatakayowawezesha kupata ushindi. Baada ya matumaini yake kugonga mwamba kwa kuwa alitumai Maotad angempendekeza awe mwakilishi wake wa kuendeleza sayari ya NUKA,

Amrao aliibuka na mipango saba, mipango ambayo hangeweza kuitekeleza kwa wakati mmoja. Kwanza, alifikiria kumuunga mkono U, chaguo lake Maotad na halafu atulie tuli kwa matumaini ya kupata kipande chochote cha mnofu ambacho angetunukizwa. Pili, alifikiria kumuunga mkono U mradi tu awe makamu wake. Tatu, aliwaza kuhusu kumuasi U na Maotad akiwa na lengo la kujiunga na wanasayari wengine. Nne, alionelea avimeze vipande vya wembe na anywe sumu afie mbali na kwa njia hii azikwe na asahaulike. Tano, alikuwa na njama ya kumzima U kwa namna aliyoifahamu yeye. Sita, ni kuwaomba karatasi muhimu waliyoifadhi wakazi wa Bikerani-Msiige, karatasi ambayo ingebadilisha maisha yake kwa miaka mitano kwa kuking'ang'ania kiti kitukufu akiwa peke yake. Mwisho, ni kujiunga na LiMioe, Boyi, na Fadhila kwa azma ya kuzisaka karatasi muhimu dhidi ya karatasi za U (uk 100). Kwa namna hii, kuchanganyikiwa kwa Amrao baada ya kuondoka katika merikebu walioiabiri U na Maotad inachimuka. Hii ni hali inayowakumba wanasiasa wengi ambapo kwa sababu ya pupa yao, wao huungana na vyama tofauti na baada ya siku chache wanakorofishana kwa sababu matumaini waliyokuwa nayo hayatimizwi hasa katika ugawaji wa vyeo. Wanapojiondoa katika miungano hiyo, wengi wao huwa na njama za kuwadhuru wengine, kuwashambulia kwa matusi, kuwadharau hadharani na vilevile kutafuta mbinu za kushindana nao.

Amrao alikuwa mpenda makuu na makubwa kwelikweli, ukweli unaochimuka na kudhihirika kwa uwazi katika uk 101-102. Tunaambiwa kuwa Amrao alipenda mandhari mazuri, safi, yenye kupendeza ambayo yalitembelewa sana na watu kutoka sayari za nje, watu waliozungumza lugha tofauti na wakazi wa pale. Watu hawa walikuwa na ngozi za kijanikiwiti, macho ya rangi ya samawati na waliobeba misahafu na mikuki mikali kushinda mikuki yote walipokuja katika sayari ya NUKA. Alikuwa tofauti na Maotad aliyeshiriki mikutano yake katika mkahawa mkubwa wa Tortoise-Ram Court uliokuwa tu na ukuta mkubwa wa kuwahami wageni waliozuru

mahali pale na wenye mandhari sawia na ya Haponaseremwige. Aidha, alikuwa tofauti na akina Boyi, Fadhila na LiMioe walioendeleza mikutano yao Haponaseremwige ndani ya chumba. Amrao na Saigeo walikutana sanasana katika mkahawa wa Hakuna Uma kutokana na mandhari yake ya kuvutia, walipenda kukaa chini ya miti ya aina nyingi, mitobwa, mitomoko, mitondoo, mitonga, mitokwe, mitomondo, mitongonya, mitopetope, mitoria na mitongotongo iliyokuwa imepandwa kwa safu na kupafanya pahali hapo kuwa na mastakimu ya kustarehesha.

Amrao hakuchelewa katika mikutano, alifika mapema na alipochelewa ilikuwa ni kwa dakika chache. Hii ilikuwa tabia yake, kutangulia mikutanoni kabla ya yeyote kuwasili, sifa inayochimuza katika uk 110. Baada ya kuagana kukutana na Saigeo katika mkahawa wa Hakuna Uma mwendo wa saa saba za mchana, Amrao alifika saa sita naye Saigeo akafika saa saba kasorobo.

Alikuwa na utaratibu hasa katika kuendeleza kampeni za kupigia debe Azimio la Mwaujua Mbuyu. Aliwapa viongozi wenzake utaratibu ambao wangeufuata ili kujipatia ushindi. Kwanza, aliwajulisha kuwa mhubiri kutoka sayari za nje angekuja kuwaombea yeye na U ili Mungu alikubali dua lao kwamba njiwa angepata ushindi dhidi ya mumbi. Aliwaongoza kuhusiana na nguo, bakora, magari, baiskeli, mikutano na hotuba zao. Aliwaeleza kuwa walitakiwa kutumia nguo na bakora za rangi nyeupe na magari ya kibinafsi na wala sio ya utawala wa BORA. Pia aliwaeleza kwamba baiskeli zifuatane na magari huku zikihinikiza mchanganyiko wa kengele na honi huku wenyewe wakibeba mifano ya njiwa na majani ya miti. Hawa walikuwa washtumu mumbi kwa kutumia maneno yasiyoweza kupigwa chapa magazetini. Aliwaeleza kuwa makao yao makuu yangekuwa Kar Pi Mang'ich, kuwa wimbo wao ungekuwa mapambano dhidi ya mafamba, mikutano yao ingegawanywa katika makundi madogo madogo na kuwa hotuba ingetolewa na kila mmoja kwa kuzingatia kitu alichoambiwa. Aidha, aliwataka wachague

kutumia maswali ya balagha kuwakejeli wapinzani wao au kwa kutumia dhihaka. Aliwataka wawe na fomula funguzi ili wasiwakanganye wafuasi wao. Mwisho, aliwahimiza waingize futuhi ya kitashtiti na kicheshi katika hotuba zao ili wawe na hadhira tendi, watumie lugha nyepesi na wawe na mantiki.

Alipenda kutumia sana vitendawili, mathalani katika uk 225 anapoelezea kundi lake kuhusu Azimio, anawatolea kitendawili cha jinsi mtu anaweza kumpikia mgeni wake chakula kitamu na halafu kumpakulia huku akimtukana. Kwa namna hii, aliwafafanulia kuwa mgeni huyo hawezi kuwa na raha wala hawezi kukila chakula hicho. Hata hivyo, aliwaeleza kuwa iwapo mgeni ataonyesha furaha na aendelee kukila chakula hicho atakuwa hataki kumuudhi mwenyeji lakini katika nafsi yake atakuwa ameudhika ajabu na malengo yake yatakuwa kungoja siku ya kulipiza kisasi. Huu ni ujumbe uliokuwa muhimu sana katika kipindi hicho, ili kulishinda kundi la mumbi, wafuasi wa njiwa walihitajika kutumia mbinu mwafaka za kuwanasa wakazi katika upande wao kwa kuonyesha sababu murwa za kuwafanya wapinge Azimio la Mwaujua Mbuyu.

### 3.1.4 U

Babake alikuwa Jokaga na walitoka katika jamii ya QiQu. Alikuwa mdogo kati ya mazimwi wengine kama vile Avadi, Kamu, na Kanga waliokuwa wameahidiwa uongozi wa NUKA na Maotad. Utajiri uliomzunguka kutokana na kulelewa katika familia ya kifahari unachimuzwa kwa uwazi (uk 72). Mwandishi anatujuza kuwa U alikuwa mtoto wa watu aliyetoka katika familia ya watu. Kasri alimozaliwa na kulelewa lilijaliwa nyota ya jaha, lilinukia vizuri na ardhi yake ilikuwa imepakwa rangi ya biti marembo. Sebuleni, mlikuwa na mirasho iliyowekwa kuchangia hewa safi iliyokuwamo mle, nayo dari iliyopakwa rangi ya magnolia ilikuwa na mataa

ya thurea yaliyoning'inia. Katika upande wa pili kulikuwa na chetezo iliyoagizwa kutoka sayari za mbali. Kandoni mwa sebule la wageni, kulikuwa na mtawangu wa bei ghali.

Kasri lenyewe lilikuwa limejengwa kwa kuzingatia mtindo mojawapo wa jamii moja katika sayari ya NUKA na lilikuwa na vidaka vilivyobeba vito vya thamana. Vidaka hivi vilitunzwa vizuri ili kuwapa raha wageni waliokuja kutembelea babake U. Ndani mwa sebule, kulikuwa na viti ainati, vya mpingo, vya enzi, karasi, mdodoki na viti vya jeuri. Meza nayo ilikuwa na sinia ya shaba iliyobebea vyakula kadha. Vilevile, kulikuwa na chango cha wageni cha kutundika koti lililokuwa katika msana wa kati. U aliishi maisha ya raha, hakujua shida kama wakazi wa Bikerani- Msiige, yeye hata alilalia pavilao na samadari. Wakazi hawa walikuwa wamekata tamaa maishani, waliishi maisha ya umaskini, hawakuwa na lolote wala chochote, vitoto vyao havikuwa hata na mavazi, vililalia mararu ya mashati na mabaki ya suruali.

U alikuwa na maumbile yaliyomtofautisha na kiumbe yeyote yule. Maumbile haya yamechimuzwa hivi kwamba, walioishi nyakati hizo wanaweza kumtambua kwa kuzisoma sifa hizi zake. Mbali na kuwa mdogo kati ya mazimwi, Avadi, Kamu na Kanga, mwili wake haukuwa mkubwa, alikuwa amekondeana licha ya kuwa mtoto yai aliyedekezwa na kubembelezwa. Hali kadhalika, ingawa alikuwa na nywele za kipilipili, hakuzitunza na mara nyingi zilikuwa timtim. Macho yake hayakuwa ya kawaida, yalikuwa ya kikombe na mekundu sana kama damu. Midomo yake ilikuwa na rangi tofauti ikilinganishwa na rangi ya ngozi yake iliyokuwa nyeusi, hali iliyomfanya akibebe kibatari utosini mwake ili apate kutambua alipoenda na alipokuwa.

Ingawa Maotad alimpenda sana U na alimpa kipaumbele kwa kila jambo ikiwemo chakula, nguo na rumkis malt, mwandishi anatuchimuzia kwa uwazi kwamba ingawa hivi, U hakupendwa hata

kidogo na wakazi wa Bikerani-Msiige kwa kuwa alikuwa hafahamu siasa na haswa shida zilizowakumba wakazi hawa. Kwao, U hangewasaidia katika utatuzi wa madhila yaliyokuwa yamewaandama kwa miaka mingi na kwa hivyo, walimtaka mtu ambaye alielewa shida walizokuwa wanazipitia na hali kadhalika atakayewasaidia katika kuinua hali yao ya maisha iliyoelekea kuzorota siku baada ya siku kutokana na kunyanyaswa na kudharauliwa. Kwa namna hii tunajuzwa kwamba, U alikuwa kiumbe dhaifu ambaye hakujulikana ingawa alishirikiana na Maotad katika unywaji wa *rumkis malt*. Sababu ni kuwa, U alikuwa kitoto kichanga ambacho kilikuwa kinaanza kujifunza kusimama dede na wala hakikujua kutembea kwa kuwa hata alipoanguka alimwita mamake kwa usaidizi.

Katika ukurasa wa tisini na moja, kutokomaa kwa U kisiasa kunachimuzwa. Baada ya Maotad kuamua kutii sheria iliyomtaka ajiuzulu kama mmoja wa kuwania uongozi mwaka wa 2200, alianza kuzuru sehemu nyingi za sayari ya NUKA kwa lengo la kuwapasha wakazi ujumbe kuwa, U alikuwa chaguo lake na alikuwa radhi kumwachia uongozi wa sayari ya NUKA. Tunajuzwa kuwa U alikuwa mtoto mchanga sana ambaye bado alikuwa yuanyonya. Mbali na kuwa mtoto asiyekuwa na uwezo wa kusimama dede wala kutambaa, alipewa nafasi hii muhimu na Maotad iliyomezewa mate na wengi. Alikuwa mtoto mchanga sana ambaye hakuwa na nguvu za kutafuna ‘cerelac’ wala kunywa uji. Aidha, alipoitwa “wee mtoto wee” badala ya kuangalia aliyemwita, U alidhani kaimbiwa wimbo wa kumbembeleza ili alale na kwa namna hii alifunga macho yake na kulala. Hata angeulizwa jina lake alijibu “maa- maa- maa”, alikuwa mtoto asiyeweza kuandika herufi O wala kujua tofauti kati ya moja na sufuri. Hii ni hali iliyoweka wazi imani ya wengi kuhusiana na hatua ya Maotad ya kumchagua U wakati huo, kwamba hakuwa na uwezo wa kuongoza na maarifa ya kuinua hali ya maisha ya wakazi wa Bikerani-Msiige na uchumi uliokuwa umesambaratika.

Wakazi wa Bikerani-Msiige vilevile hawakumwamini. Kwa jinsi hii, tunajulishwa kwamba kitovu chake kilikuwa bado na unyevunyevu kwani hakuwa ametenganishwa na kiwiliwili cha mamake kwa muda mrefu. Kwa mintarafu hii, hakujulikana kama alikuwa anafanana na babake, mamake, shangaziye au labda Maotad, ilikuwa mapema sana kwa yeyote yule kutoa uamuzi. Hii ndiyo sababu mwandishi anaeleza katika uk 91 kuwa ni mamake alimyejua babake. Hivyo, U peke yake alijijua, alitambua msimamo uliomvutia zaidi, kama alikuwa azingatie nyayo za baba yake katika uongozi ama za Maotad na kuendeleza mafamba. Maana inayojichimuza ni kuwa, U aliogopwa na wakazi wa Bikerani-Msiige kutokana na uhusiano wake na Maotad na kamwe hawakumwamini, waliogopa U aisaliti imani yao ya kuleta mapinduzi ya uzalendo katika jamii.

Macho yake aliyafunga kila baada ya sekunde saba wala haikufahamika sababu yake. Vilevile, alikuwa mtoto wa ajabu kwa sababu hakulia, alipomwona paka alimshika kwa sababu alifikiria ni mwanaserere. Paka hawakumdhuru walipocheza naye kwa kuwa walimpenda kweli kweli, ni paka waliokuwa wanene na walizuia yeyote kumkaribia U, walicheza naye usiku mchezo wa *waltz* na hali kadhalika kumwimbia nyimbo za watoto ili apate kulala (uk 92). Kwa mintarafu hii, ni dhahiri kuwa U alihusiana vizuri na wanasayari wa NUKA waliokuwa mashuhuri bila kuwaogopa licha ya kuwa mdogo asiyefahamu vilivyo mambo yalivyoendelezwa katika sayari ile. Alihusika nao katika shughuli mbalimbali na wala hawakuonyesha chuki kwa sababu waliutii uamuzi wa Maotad na walifahamu matokeo na athari za kutotii kwao.

U alikuwa chaguo la Maotad na alihitajika kuchukua mahali pake, jambo lililosababisha uhasama kati yake na kundi la Amrao. Kutokana na ukweli huu, walianza kushambuliana kwa matusi mazito, hali iliyopelekea U kuanza dhuluma dhidi yao. Kundi lake lilianza kutumia mapepo na majini yaliyoishi katika sayari ya NUKA, kweli mtoto wa nyoka ni nyoka. U aliamua kufuata nyayo za Maotad ili kufanikisha mradi wao. Mapepo haya na majini yaliungana na

mashetani ili kusababisha umwagikaji wa damu kwa wakazi wa Bikerani-Msiige, damu ambayo haikuonekana kwa sababu matone yote yalirambwa na mazimwi na mapepo kwa kutumia ndimi zao pindi tu ilipomwagika. Dhuluma zilizowaandama wakazi wa Bikerani-Msiige zimechimuzwa kwa uwazi katika uk 99. Tunaambiwa kwamba walinda usalama walitoa propaganda kwa wakazi wa Bikerani-Msiige kuwa umwagikaji damu uliotuhumiwa wafuasi wa U ulikuwa propaganda za Amrao. Hata baada ya hotuba hii ya kutetea kundi la U, majini na mapepo yalikuja wakati wa magharibi na kuangamiza makao rasmi ya wafuasi wa Amrao na kutoroka. Ithibati kwamba, walinda usalama walishirikiana na utawala katika kuwatesa wakazi. Ukatili ulioandama U na wafuasi wake unachimuzwa, baada ya kughadhabishwa na watu waliomshutumu, wafuasi wa U walimvamia mzee mmoja na kumkatakata vipande vipande pamoja na wanawe kwa sababu ya kutoungana naye. Aidha, ndimi za wafuasi wa Amrao zilikatwa na sehemu zao za siri kuchopolewa na kukaangwa jambo lililomkasirisha sana Amrao na kumfanya atafute njia ya kumzima.

### 3.1.5 WAKAZI WA BIKERANI-MSIIGE

Hawa waliwakilisha wananchi ambao jukumu lao muhimu lilionekana na viongozi kama kupiga kura pekee ambapo baadaye walisahaulika kwa kipindi cha miaka mitano pale shughuli ya aina hiyo ilitarajiwa kufanyika tena. Maingiliano yao na viongozi wa sayari kadha yalisababisha umaskini, chuki na uhasama kati yao. Ni watu ambao asili yao haikujulikana vyema, ilikuwa tata, hawakujulikana kama walizaliwa pale ama walikuwa wametoka mahali tofauti na kuguria hapo. Kulingana na viongozi wa NUKA, hawa walikuwa wanadamu kutoka makabila tofauti na kwa hivyo walitilia shaka kuwepo kwa kabila la wenyeji halisi wa Bikerani-Msiige. Waliokuwa na imani tofauti walishikilia kuwa wakazi halisi wa Bikerani-Msiige walikuwa Masuriama wenye asili ya watu wenye rangi ya kijani kibichi kutoka sayari ya mbali yenye joto jingi na pea,

pea ambaye haijulikani alipopatana na watu hawa wa rangi ya kijani kibichi. Kwa mujibu wa wengine, wakazi wa Bikerani-Msiige walikuwa kundi la watu walioishi katika sayari ya NUKA toka zamani. Kulingana na hadithi simulizi ya wakazi hawa, asili yao ilikuwa sehemu ya kisasili cha sayari ya NUKA. Wakazi hawa walikuwa na imani kuwa walikuja na kukaa sehemu ya Bikerani-Msiige kutoka mahali palipojulikana kama twatokawapi, mahali pa asili kukaliwa na wakazi hawa na palipoaminika kuwa kati ya mpaka wa NUKA na PiDiEli. Wakazi hawa walijiweka katika kundi la watu wenye maumbile kama ya pea ambao mahame yao ya kiasili yalikuwa mbali na Bikerani-Msiige. Kulingana na kisakale, kundi hili lilihamia katika makao yao ya kiasili kutokana na sababu mbalimbali kama vile ongezeko la idadi ya watu, azma ya uzururaji, uvamizi kutoka kwa majirani, kutoroka mapigano ya kijamii, ukame, magonjwa na uvumbuzi wa kiufundi kama vile ufuaji wa vyuma.

Kuhama kwao hakukuwa kwa ghafla, ni watu waliohama kwa utaratibu na baadaye kusambaa katika eneo kubwa la NUKA, uk 132-133. Maelezo haya yanachimuza ukweli kwamba, wakazi hawa ambao wengi wao walizifuata sera za NUKA hawakutoka katika makabila sawa ya jamii zetu bali tofauti na kuwa asilimia kubwa ilitoka sehemu alikozaliwa Maotad. Vilevile, tunapata maana kuwa wengi wao walishinikizwa kubadilisha msimamo wao kuhusu kuendelea kuzifuata sera za NUKA na hivyo wakahamia sayari nyinginezo kutokana na sababu kadha kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Kwa mintarafu hii, walihama kwa kuwa kulikuwepo na watu wengi katika NUKA na hivyo wengine walihamia katika sayari zilizokuwa zinaibuka labda kwa kukosa imani nayo. Pili, iliwabidi wahame kutokana na mapenzi ya kuonja vinywaji na vyakula vilivyopikwa kwingineko, yaani azma ya kutaka kujua kama sayari nyinginezo zilikuwa sawa ama tofauti na NUKA. Tatu, kuibuka kwa sayari zilizoelekea kuwa na misimamo thabiti zaidi na zenye mwelekeo mwema. Nne, shutuma, kunyanyaswa, dhuluma, kutoshirikiana na chuki baina

ya wanachama wa NUKA. Tano, kutoshughulikiwa kwa wakazi wa Bikerani-Msiige kulikosababisha shida ainati kwao. Sita ni mafamba na mwisho ni uvumbuzi wa njia mwafaka ambazo zingewaletea manufaa kama ushirikiano ambao haukunawiri katika NUKA. Sababu hizi labda ndizo zilizowafanya kuhama na kujitenga na kundi kubwa la BORA lililokuwa na wafuasi maarufu kama LiMioe, Maotad, Amrao, Fadhila, Boyi na Mastanji.

Baadhi ya wakazi hawa walizungumza lugha ya Dhochi iliyowaleta pamoja na yenye vitendawili ambavyo havikueleweka, msemaji alisikika kana kwamba anamumunya maneno. Ingawa hivyo, ni msamiati uliopanuka kufuatia maingiliano yao ya miaka mingi na wafuasi wa NUKA, NUZAPIFU, PEFO, PiDi na wengineo. Pia waliegemea dini ya Bora pek na kwa njia hii, haikuwa rahisi kurejelea utamaduni wao bila kuwahusisha na dini hii. Kuja kwa Bora pek kulisababisha wafuasi sugu wa Maotad kuasi kushiriki unywaji wa *rumkis malt*.

Mateso ya aina tofauti yaliwaandama siku baada ya siku na kuzidi mwaka baada ya mwaka, wao walijitambulisha na utamaduni uliojaa umaskini wa kupindukia kama kutokuwa na barabara, hospitali, shule, usalama, nguo, chakula, vyoo, maji na umeme miongoni mwa vitu vingine. Hivyo, umaskini uliimarika, ukakithiri na kuathiri miundo ya wakazi hawa na utamaduni wao. Nyumba za madongoporomoka, chakula chenye sumu, mavazi yenye kupigwa viraka na ubezaji wa uongozi wa NUKA ndiyo iliyokuwa hali yao ya maisha. Walipokea dhuluma kadha kutokana na utawala wa Maotad, mtu aliyewakera, kuwachafua roho na hali kadhalika kuwatia kichaa. Ingawa walichangia kwa kiwango kikubwa katika juhudi za ujenzi wa taifa, hawakupewa fursa ya kutoa ushauri wao kuhusiana na maendeleo ya jamii.

Hawa ni wanadamu waliotegemea kudura ya Mungu, waliishi maisha ya umaskini tofauti na viongozi wao walioishi raha mstarehe. Katika uk 1, hali hii inachimuza kutokana na maelezo ya

mwandishi. Hapa ni mahali palipokuwa na vijumba vya madongoporomoka vilivyoelekezana milango ya mabati na kupeana migongo ili kuhimizana, yaani vilikuwa vimekaribiana sana kiasi cha kutokuwa nafasi ya kutema mate ama kutua nzi. Aidha, milango ya vyoo vyake ilikuwa magunia matupu ya sukari yaliyofanya juhudi kubwa kuchukua pasipo haya nafasi ya milango iliyokuwa imeanguka kwa namna iliyokinga jicho la wapita njia kuwaona. Hata hivyo, milango hiyo kwa hakika haikuzuia chochote kwa kuwa aliyekuwa nje aliweza kumwona aliyekuwa ndani. Hii ni taswira iliyokuwa tofauti kabisa na hali iliyokuwa mkabala na mtaa huu. Mkabala na mtaa wa Bikerani-Msiige, kasri la kifahari lilisimama tisti bila haya. Lilikuwa na dari iliyovuta nakshi kwa mpingo na yenye mataa maridadi ya thurea yaliyoning'inia darini. Sakafu yake ilikuwa safi na yenye jiwe la marmar katika pembe zake saba. Upande mmoja ulisheheni mirahatillayl na mikilua, miti iliyochangia kivuli kizuri kilichowaneemesha wakazi wa kasri lile walimoishi wanadamu wenyewe.

Umaskini ulikuwa umekithiri na kudhihirishwa sio tu na vyumba vibofu bali pia, mavazi na maisha ya watoto waliozaliwa huko yaliweka dhahiri ukweli huu. Hali inayochimuka katika uk 125-126 ambapo tunajulishwa kuwa waliohudhuria mikutano ya Maotad walikuwa watoto labda kwa azma ya kupewa pesa ili angalau waweze kujinunulia chakula. Sababu ni kuwa, walionekana dhaifu huku vitumbo vyao vikipasua funguo za mashati waliyoyavaa kama kwamba walikuwa na utapiamlo kwa kukosha lishe bora. Aidha, vitumbo vyao vilionyesha alama iliyoachwa na 'mto'au michirizi ya mchuzi uliokuwa kitoweo juzi. Pia, mavazi yao yalibainisha umaskini uliowazunguka kwani wengi wao hawakuwa na nguo ila suruali zilizokuwa zimepigwa viraka miaka nenda miaka rudi na ambazo iwapo zingepasuka kwa mara nyingine, sindano haingefanya kazi kwa kuwa hazingeshoneka. Labda kama asemavyo mwandishi, misumari ya

inchi nne ingetumiwa kupenyezea matambara ya nguo hizo zilizokuwa zimeshonwa mara kadha ili kufunika uchi wao. La sivyo, ingekuwa kazi bure kujaribu kuzishona tena.

Ni shida zilizowakumba wadogo kwa wakubwa, kuna wengi waliotembea uchi bila nguo na wengine walivalia debwani. Watoto walivalia vidochi viunoni mwao, wanawake na wanawali walivalia vipande virefu vya nguo walivyovifunga viunoni ambapo ncha zake mbili zilishikanishwa kisha kupitishwa juu ya bega moja kama kaniki huku wakiwa wamevaa barakowa na ukaya, nao wanaume walivaa visibau vyenye rangi kukiwemo makubadhi. La ajabu ni kuwa, Maotad aliendelea kuwapuuza na kulingana na nafsi yake, alionelea watoto hao wajaliwe ikiwezekana ama wakamatwe na walishwe simba marara. Yaani, wapate usaidizi kutoka kwa wafadhili wengine ama waangamie kwa njia mbalimbali, ni watoto ambao hawakubahatika kupata fola tangu walipofungua macho kwa mara yao kwanza.

Katika uk 69, mateso ya aina mbalimbali waliyoyapata wakazi hawa wakati wa utawala wa Maotad yanachimuzwa kwa uwazi. Tunaambiwa kwamba, mbali na vyoo vya ajabu vilivyokuwa huko, walipewa na Maotad chakula sawia na kilichokuwa kikipewa waliofikishwa mkanyageni, jumba la orofa 77 lililokuwa na sifa mbaya. Chakula kilichopikwa huko ni panya wa kukaangwa, msongareli wa kukaushwa, sindano za kuchemshwa, miiba ya kuchomwa na miguu ya kombamwiko iliyokauka, chakula walichojaribu kukila ili kutunza siha yao lakini hawakuongeza uzani wowote. Licha ya juhudi zao za kukabiliana na madhila haya, hawakufaulu kwa sababu ya mafamba, kushuka kwa thamani ya shilingi, ufisadi uliotekelezwa na vigogo wakubwa serikalini, kutoa na kupokea mlungula kwa waliopewa kandarasi za kuendesha, uuzaji wa mashamba yaliyotengewa miradi ya kunufaisha umma kama ya kustawisha misitu ama kujenga shule na aidha uanachama katika kampuni ya mfuko wa vito kwa jina maarufu 'goldenbag' iliyofilisisha

jamii kwa kiwango kikubwa wakati huo na kusababisha athari kwa vitoto ambavyo bado havikuwa vimezaliwa.

Vilevile, tunajuzwa kuwa wakazi hawa walikuwa na mazoea ya kunusa sumu ya tumbo na wala sio hewa safi waliyoifurahia kwa mujibu wa Maotad, hata watoto wao waliifurahia sumu ya tumbo kwa kuwa waliipinga hewa safi. Maana inayochimuka ni kuwa, wakazi hawa walizaliwa katika mazingira mabaya, wakakuzwa kwa shida na chakula kibaya, wakavishwa mararu ya mashati na mabaki ya suruali na kwa namna hii wakakua bila kutambua haki zao kwa kudhani hayo ndiyo yaliyokuwa maisha mema, maisha waliyoumbwa kuishi na muumba ila tu hawakufahamu kuwa huo ulikuwa msiba uliosababishwa na utawala mbaya wa Maotad.

Wakazi hawa walikuwa nyenzo kuu ya ukuzaji na uimarishaji wa vigogo wakuu wa NUKA kama vile Maotad, Nikiabi, Saigeo, Kanje na U. Ingawa hivyo, jambo hili halikuwa rahisi kwani wengi walitumia mbinu mbalimbali kufikia malengo haya, hali inayochimuka katika uk 135. 'Biashara' katika eneo la Kar Pi Mangi'ch ilikuwa changamano, iliyobadilika na iliyohusu mahusiano ya kiuchumi kati ya vigogo hawa na wakazi wa Bikerani-Msiige. Tunajuzwa kuwa wakazi hawa walishikilia usukani katika shughuli za kibiashara kati ya Karifa, NUKA na sayari nyinginezo kwa karne nyingi. Ni wazi kuwa ingawa wakazi hawa walikuwa tegemeo la walionuia kuwa viongozi kwa kuwa ni wao pekee walioamua kupitia kwa debe, ilibidi waliohusika wajikakamue kwa sababu kuchaguliwa kwao hakukuwa suala la kawaida. Ni shughuli iliyokuwa changamano na iliyohitaji ujuzi wa hali ya juu kwa kuwa uamuzi wao ndio uliokuwa wa mwisho. Waliohisi hawatatoboa katika mkondo huo wa utaratibu, walijihami kwa kutumia mchezo maarufu wa wazee kama alivyozoea Maotad, mchezo wa karata, yaani kuiba karatasi za kura na kuziongeza katika debe.

### 3.1.6 MZEE TWAJUA

Hili ni jina la kimajazi lenye maana ya kufahamu mengi. Ni mzee aliyefahamika sana katika kijiji cha Tuga Amor, kijiji kilichokuwa mkabala na Bikerani-Msiige. Wengi wao walikuwa washiriki wa ulevi, waliokunywa vileo vya bei nafuu kwa sababu ya umaskini. Siku moja walilewa kupindukia kwa kileo ambacho chanzo chake hakikufahamika, hali iliyowafanya waathiriwa kupofuka macho, waliokosa kuwa vipofu walipoteza uwezo wa kuongea na waliojaribu kuongea kiwango cha juu cha matamshi yao kilikuwa ni kupiga kithembe. Ni watu walioathirika sana kutokana na hali mbaya ya maisha. Baadhi yao walikuwa na vichwa vya koroma, mengi ya mambo yao yaliwaendea mvange kwa sababu walishinda mchana kutwa wakilaza damu, wanawake na wanaume walilaumiana, wanaume walidai kuwa wake wao walikuwa tasa nao wanaume walishikilia kuwa wanaume wao walikuwa hanithi. Ingawa ni kijiji kilichokuwa na watu wachache na chenye sifa mbaya, Mzee Twajua aliyetambua mengi, alipata kuzaliwa pale.

Alikuwa na hekima ya hali ya juu, alijulikana kwa weledi na usafi, mambo yaliyomfanya aheshimike kwa kuwa aliwakilisha maoni ya wengi katika Tuga Amor (uk 191-196). Aliwazidua kutokana na maneno yake ya hekima pale ambapo walionekana kukosa matumaini sababu ya shida zilizowakumba mara kwa mara. Kitambo kidogo baada ya BORA kuchukua usukani, kulikuwa na amani na ushirikiano katika kijiji hicho ambapo wenye mapenzi ya michezo ya pumbao kama vile bao la komwe na kete walicheza kwa pamoja. Nao wapenzi wa dumma, dama, shatranji na karata walicheza pia kwa pamoja, uchechefu wa watu wazima waliokaa pale kushuhudia michezo hii haukupungua. Vitoto vinyangarika navyo mara kwa mara vilikimbizana chini ya mkungu vikicheza foliti, hata hivyo ni furaha ambayo haikuzidi miaka miwili.

### 3.1.6 MZEE TWAJUA

Hili ni jina la kimajazi lenye maana ya kufahamu mengi. Ni mzee aliyefahamika sana katika kijiji cha Tuga Amor, kijiji kilichokuwa mkabala na Bikerani-Msiige. Wengi wao walikuwa washiriki wa ulevi, waliokunywa vileo vya bei nafuu kwa sababu ya umaskini. Siku moja walilewa kupindukia kwa kileo ambacho chanzo chake hakikufahamika, hali iliyowafanya waathiriwa kupofuka macho, waliokosa kuwa vipofu walipoteza uwezo wa kuongea na waliojaribu kuongea kiwango cha juu cha matamshi yao kilikuwa ni kupiga kithembe. Ni watu walioathirika sana kutokana na hali mbaya ya maisha. Baadhi yao walikuwa na vichwa vya koroma, mengi ya mambo yao yaliwaendea mvange kwa sababu walishinda mchana kutwa wakilaza damu, wanawake na wanaume walilaumiana, wanaume walidai kuwa wake wao walikuwa tasa nao wanaume walishikilia kuwa wanaume wao walikuwa hanithi. Ingawa ni kijiji kilichokuwa na watu wachache na chenye sifa mbaya, Mzee Twajua aliyetambua mengi, alipata kuzaliwa pale.

Alikuwa na hekima ya hali ya juu, alijulikana kwa weledi na usafi, mambo yaliyomfanya aheshimike kwa kuwa aliwakilisha maoni ya wengi katika Tuga Amor (uk 191-196). Aliwazidua kutokana na maneno yake ya hekima pale ambapo walionekana kukosa matumaini sababu ya shida zilizowakumba mara kwa mara. Kitambo kidogo baada ya BORA kuchukua usukani, kulikuwa na amani na ushirikiano katika kijiji hicho ambapo wenye mapenzi ya michezo ya pumbao kama vile bao la komwe na kete walicheza kwa pamoja. Nao wapenzi wa dumma, dama, shatranji na karata walicheza pia kwa pamoja, uchechefu wa watu wazima waliokaa pale kushuhudia michezo hii haukupungua. Vitoto vinyangarika navyo mara kwa mara vilikimbizana chini ya mkungu vikicheza foliti, hata hivyo ni furaha ambayo haikuzidi miaka miwili.

Mzee Twajua na wakazi hawa hawakuamini kwamba hali ingebadilika na kuwa kama ya zamani, mafamba yalizinduliwa tena pamoja na mlinzi wake maarufu nopro yaani 'no prosecution'. Matumaini ya kuwafichua waliotekeleza nyendo mbovu katika utawala wa NUKA yalififia kwa sababu ya mafamba, mathalani mafamba ya mfuko wa vito. Walioshiriki walienda zao kwa kuwa nopro haikuwapata na hatia. Ingawa mfuko wa vito ulikuwa umesababisha umaskini na hivyo haja ya kuwafungulia mashtaka waliohusika, uongozi wa LiMioe ulibainisha kuwa yaliyopita sio ndwele na kusisitiza umuhimu wa kuganga yajayo, ambayo pia hayakuweza kugangika kwa sababu ya mafamba. Hakuna aliyeamini kwamba BORA ingeshiriki mafamba kama vile NUKA kwa sababu azimio lao kuu lilikuwa kuzika milele mafamba. Kwa namna hii, jukumu maalum la Mzee Twajua likawa ni kuwahamasisha wakazi hawa kwa kuwafungua macho huku akiwategulia kitendawili cha mafamba na nopro kilichowafanya wahusika wa kashfa ya mfuko wa vito kuwekwa huru.

Aliwafahamisha kuwa mafamba hayakuwa tu katika mfuko wa vito ambapo kesi ilibatilishwa baada ya mashauriano na hakimu bali pia yaliendelezwa katika sekta mbalimbali ambapo wenye kutenda mema na maovu walishiriki. Kwa namna hii, aliwahamasisha kuwa uchafu wowote uliohusiana na ufisadi, ulungula, ukabila, ubinafsi, chuki, uuaji, ubwanyenye, unajisi na uungu ulikuwa dalili ya mafamba. Funzo lake kwa wakazi hawa lilikuwa kwamba, ni mwiko kutenda mambo haya. Aliwaelimisha kuwa, sababu ya kuteseka kwao ilichangiwa na uvunjaji wa miiko hii na kutozingatia sheria kwa wanaohusika wakati wa kutoa hukumu. Pale ambapo, wanaovunja miiko hii hushikwa na baada ya kupatikana na ithibati ya kuivunja, wao hupelekwa mahakamani, hupewa hukumu kali, hukatiwa rufani, huachiliwa na kuwekwa huru na baada ya muda mfupi wanarudia makosa yale yale tena.

Aliwafafanulia maana halisi ya nopro, sera chafu inayowaachilia huru watendaji wa nyendo chafu na shetani mwovu aliyezaliwa na mafamba. Kwa mujibu wa Mzee Twajua, nopro huwarejeshea wauaji, wabakaji na wezi uhuru mpya wa kuendeleza matendo haya. Ndiyo iliyofanya kashfa ya mfuko wa vito kuzikwa kwenye kaburi la sahau, ikafanya kijiji chao cha Tuga Amor kushindwa kuzika kileo kilichosababisha wengi kukosa kuona na kuzima matendo ya ndoa na vilevile kusababisha wauaji wa watu mashuhuri kama Rojoo kuwa huru hadi wa leo. Aliwaelezea sababu ya kufanikiwa kwa nopro, kuwa wanaohukumu na wanaokata rufani huwa na sifa bainifu zinazoshabihiana na kuwatambulisha kama vile matumbo makubwa, majumba makubwa ya kifahari, mabenzi meusi yenye kukupwa mafuta na uanachama katika hoteli za *seven star* yanayopatikana baada ya wenye kuhukumiwa kufanikiwa kukata rufani na kuachiliwa huru kwa kutopatikana na hatia.

Hali kadhalika, Mzee Twajua alikuwa mtoboa siri, hakuwaficha wanakijiji wenzake lolote lililoelekea kuathiri hali ya maisha yao. Ukweli unaochimuza katika uk 197-208. Aliwasimulia kisa kimoja cha mhandisi mfisadi katika soko la Tuga Amor lililojulikana kwa mema na mabaya, yaani kwa biashara halali na haramu. Lilikuwa soko maarufu lililokuwa na takriban vitu vyote vyenye uhai na visivyo na uhai kama vile uuzaji na ununuzi wa binadamu mfu au hai, magari ya aina yoyote ile, matunda, vyakula miongoni mwa vitu vingine. Ingawa hili lilikuwa soko la wakazi hawa, wao kwa uhakika hawakuwa wanabiashara kwani hawakuuza ila tu kununua bidhaa zilizopatikana pale sokoni. Jambo lililosababishwa na kupanda kwa gharama ya uzalishaji mali ikilinganishwa na mapato waliyopata baada ya kuuza bidhaa zao, kushuka kwa bei ya bidhaa na vilevile kulaza damu katika shughuli za kilimo baada ya kujiingiza katika unywaji pombe wa kupindukia. Ni wazi kwamba, wanaojiingiza katika unywaji na utengenezaji wa pombe haramu huwa wamekata tamaa maishani baada ya njia zao za uzalishaji mali

kunyakuliwa na vigogo wanaojishindia mashamba makubwa kwa kuwa katika jamii zetu wengi hutegemea mapato ya kilimo.

Mzee Twajua alikuwa ndiye akili na mtambo wa kuendeshea vuguvugu la kuleta mabadiliko katika sayari ya BORA, aliwakilisha sauti za wanasayari walionyanyaswa kupitia kwa mawazo yake yaliyoyeyusha aina zote za mushkil na vizingiti katika maisha yao. Wakati wa kujitayarisha kwa wakati mwingine kufanya shughuli za baada ya miaka mitano zilizotengewa tarehe 12/27/2700, aliwakumbusha jinsi walivyouma meno kwa miaka mingi na kuvumilia dhuluma kochokocho chini ya uongozi katika sayari ya BORA uliowaenzi wezi na kuabudu mafamba. Kwa ujasiri wake, aliwaongoza wanajamii kutambua kwamba lilikuwa jukumu lao kuu kuwaajiri au kuwapiga kalamu viongozi wote kulingana na mamlaka ya katiba. Aliwaeleza jinsi viongozi walivyoabudu mafamba na kusababisha wao kuwa nyuma kama koti katika hali mbalimbali za maisha na hivyo kuwahimiza washikilie na waitumie vyema silaha muhimu ya ukombozi wao. Yaani, debe ili waweze kuwazika kwenye kaburi la sahau wanasiasa sampuli hiyo kwa kuwa ulikuwa mkakati kabambe wa kuwanasa. Aliwapa imani na matumaini ya ushindi kwa kuwaondosha viongozi hao iwapo hawangebadilisha misimamo yao kuhusiana na kuwachagua viongozi walioelekea kuonyesha dalili za kuleta mabadiliko katika jamii. Ingawa kulikuwa na vyama vingi vilivyokuwa chanzo cha kukwamiza mapinduzi na kueneza usaliti, aliwatia moyo kutozingatia vyama hivi bali kufuata mkakati wa amani bila kupendelea upande wowote.

Aliwahimiza wasitumie silaha hatari kama vile visu, bastola bali watumie kura, yaani kinachotupwa ndani ya debe kwa njia ya siri kwa imani kuwa kidole kimoja hakivunji chawa. Aliwatangazia mkakati wa ushirikiano kwa kuwa kwenda kwa debe ndiko kungekuwa alfa na omega ya mateso yao. Aliwatahadharisha dhidi ya viongozi ambao hunyonya jasho lao miaka nenda miaka rudi kwa kuwajia katika ngozi mbalimbali kwa matao ya chini na kuwapunja kwa

kutumia mkakati wa kifaurongo. Mawaidha haya yalikuwa ya muhimu kwani wanasayari walipata kujanjaruka kutokana na juhudi za Mzee Twajua. Asilimia kubwa ya viongozi walitimuliwa akiwemo Damisi aliyekuwa naibu wa LiMioe huku vigogo wengine wakiangushwa kwa vishindo vikuu na kupata somo ambalo hawakuwahi kulipata maishani. Haya yalikuwa mapinduzi yaliyodhihirisha ukweli kwamba, mjinga akierevuka mwerevu huwa mashakani.

## 3.2 WAHUSIKA WADOGO AU WASAIDIZI

Hawa ni wahusika ambao hawachukui nafasi kubwa katika kazi ya kifasihi bali huwa mihimili ya kujenga dhamira na kusaidia katika ujenzi wa wahusika wakuu. Mwandishi amewasawiri kama wahusika wa kisiasa katika jamii yetu kimatendo, kitabia na kimaumbile.

### 3.2.1 BOYI

Alikuwa mmoja wa kundi la BORA aliyekuwa mashuhuri sana katika usemi na aliyefahamika kama sauti ya wenye dhiki. Alizungumza kwa king'ong'o na maneno yenye vitendawili katika hotuba zake. Alipendwa na watu wa Bikerani-Msiige kutokana na hekima yake na aidha walipenda kumsikiza sana. Katika uk 105, hekima yake ya kuwasilisha mambo hadharani kwa ufasaha inachimuka. Ujumbe unaodhihirika katika hotuba yake ni kuhama kwa Amrao kutoka kundi la U na Maotad na kujiunga kwake na kundi la BORA. Katika ujumbe huu, alieleza jinsi baba (Maotad) na mwana (Amrao) walikuwa wamekosana kwa sababu ya urithi, yaani azma ya mwana kutaka kiti cha bei ghali kinyume na mapenzi ya babake, jambo ambalo linamfanya mtoto amwasi babake na kutorokea kwa mahasidi wake. Alieleza kuwa hata baada ya mwana kuasi alikaribishwa kwa shangwe na nderemo na kufuatwa na wafuasi wengi kila mara alipopita.

Aidha, alipenda kuyaweka mambo kwa uwazi, dhana aliyoisisitiza kwa wenzake wa BORA. Jambo hili linachimuka katika uk 103 ambapo alimtaka LiMioe aseme kinagaubaga msimamo

wao bila kuficha hata jambo moja kwa kuwa wakati ulikuwa unaendelea kuyoyoma. Hii ilikuwa kawaida ya LiMioe, alipenda sana kunyamaza na kudhihirisha msimamo wake kwa vitendo. Kusema tu kwa LiMioe katika kampeni zao kwamba wao walikuwa kundi la BORA hakukutosha. Kwa mujibu wa Boyi, alihitajika aitishe 'kifungua kinywa', yaani kura walizohitaji kutoka kwa wakazi ili wapate ushindi.

Alikuwa mtambuzi wa mambo, kama inavyodhihirika wazi katika uk 142. Alifahamu kuwa vinara watatu yaani yeye, LiMioe na Fadhila hawangeweza kukikalia kiti kimoja kama ambavyo fahali wawili hawawezi kukaa katika zizi moja. Alikuwa wa kwanza kupendekeza kwamba wamwachie LiMioe kiti hicho kwa kuwa alikuwa amewazidi kwa umri na pia kutokana na ukweli kwamba alikuwa amechangia sana kifedha katika mapambano yao dhidi ya Maotad. Hivyo, alikuwa radhi kufanya hivyo ikiwa LiMioe angemteua kuwa makamu baada ya ushindi, iwapo LiMioe angekubali kuushika uongozi kwa kipindi kimoja na kipindi cha pili ang'atuke amwachie na mwisho, iwapo masharti hayo yangeandikwa chini, yatiwe sahihi na wachanjane chale kwa damu.

### 3.2.2 DAMISI

Alikuwa mkwasi aliyekuwa amekula chumvi na rafikiye Maotad, sifa inayochimuka katika uk 114-115. Tunaambiwa kuwa alikuwa mzee wa umri wa miaka 777 na mwenye upara uliong'ara kwenye jua la asubuhi. Ukoo wake ulitapakaa kila mahali, ilisemekana kwamba alikuwa na jamaa katika kila sayari, jamaa tajiri kwelikweli. Yeye mwenyewe alikuwa mkwasi wa mali na mkurugenzi wa halmashauri mbalimbali.

Vilevile, tunajulishwa kuwa alikuwa kiumbe aliyekereka kwa nadra lakini ingawa hivyo, kwa mara ya kwanza Maotad alimkera. Jambo ambalo lilimfanya amuasi baada ya kumteua U kuwa

kinara wa NUKA. Hata hivyo, hakuonyesha ishara ya kukereka bali aliamua kuondoka pasi na kuaga. Hakufurahishwa kamwe na hatua aliyoichukua Maotad, kwake jambo kama hilo halingewezekana. Kwa mintarafu hii, alimchukia na kumwona kama chanyatia mwenye harufu mbaya, dangumaro aliyependa binadamu asiye na uwezo wowote wa kujisetiri na fasiki asiyetakikana kutembea kadamnasi ya watu. Damisi kwa namna hii aliamua kujiunga na kundi la Amrao lengo likiwa kupinga hatua ya Maotad. Aliamua kuvua kofia aliyokuwa amevalia na kuchomoa mpya iliyovutia ingawa hakutaka kulivaa hadharani palipokuwa na watu wengi. Aliamua kuwaunga mkono wenzake kama Amrao, Saigeo, Avadi, Kamu na Kajo waliovalia kofia mbili zilizokuwa na motifu mbalimbali. Walivalia furahatul-watwana, falastin, swadiri, parasuweli, saadatul-kher na ishrahly, uk 115. Kwa namna hii ni dhahiri kwamba baadhi ya viongozi wengi huficha misimamo yao ya kisiasa hadi dakika ya mwisho ili wasiwaudhi viongozi wenzao waliochangia kuwainua kisiasa.

### 3.2.3 FADHILA

Alifahamika kwa jina lingine kama Chakangi Seconds. Alikuwa mkali sana hivi kwamba hakuwaogopa wanaume hata kidogo, sifa inayojichimuza katika uk 33. Tunaambiwa kuwa, alikuwa ni mwanamume katika ngozi ya mwanamke. Aliwakwaruza vibaya wanaume kwa makucha ya simba marara kwa kuyazika makucha yake yenye sumu katika miili yao na kuwatoa damu. Kiwiliwili chake kilidhihirisha kutobyongoka na ushupavu, hakuonekana katika makundi ya wanawake kwani aliamini kwamba alikuwa mwanamume katika ngozi ya mwanamke. Alikuwa jitu la futi 27 na mwenye vinywa 2 vilivyokuwa na kibarua maalum, kimoja alikitumia kuwakwaruza wanaume na kingine kwa minajili ya kula.

Aidha, alikuwa msaliti na hivyo hakuficha makosa bali aliyaweka wazi hadharani na kuhakikisha aliyehusika amechukuliwa hatua kali bila kupoteza muda. Tunajuzwa kuwa hakuwa na fadhila, alikuwa fidhuli na mkorofi ajabu (uk 33). Alipokuwa mtoto, watoto wenzake walimwogopa sana na walimwita koko. Yeye aliwachinja watoto wawili na kunywa damu yao baada ya kuwachukua, kuwasaga na mwishowe kuwala kwa kutumia kinywa cha kula, tendo alilolifanya kwa sekunde mbili hivyo akapata jina la kimajazi Chakangi Sekonds.

Mbali na kwa na vinywa viwili, alikuwa bibi tajiri na mrembo aliyejua kujipodoa na alionekana nadhifu (uk 33-34). Mathalani siku aliyokuwa amevaa blauzi ya kahawia, sare na rinda lililomkaa sawasawa na lililofanana na rangi yake ya mwili. Mabegani alikuwa amejitwika shali na miguuni alikuwa amevalia viatu vilivyonakshiwa seja za dhahabu, vilikuwa viatu ambavyo thamani yake ingewafadhili maskini wanne chakula cha kila siku kwa miaka minne. Aidha, alijitia wanja na pia kutimua shore, mwili wake ulichukuana na nguo zake zilizopendeza, rangi yake ya ngozi ilichukuana aidha na vipuli alivyojipamba navyo. Maana inayochimuza ni kuwa baadhi ya viongozi wanawake wanapochaguliwa ili kuwakilisha jamii, badala ya kuzingatia maslahi ya jamii kwanza, kazi inakuwa kutumia rasilimali za kuendeleza maendeleo katika uagizaji wa vipondozi ghali huku wakisahau majukumu yao.

### 3.2.4 AVADI

Alikuwa mfuasi wa NUKA aliyezifuata sheria zake tukufu, ila tu Maotad alipokosa kumteua kuwa kinara wa kuendeleza sayari ya NUKA na badala yake kumchagua U, aliamua kumuasi na kujiunga na kundi la Amrao. Jambo hili lilimuudhi sana Maotad ambaye alimshurutisha aasi ushirikiano wake mpya kwa kumdhulumu na kwa hivyo Avadi akajiunga tena na NUKA. Sababu ni kuwa aliogopa kuuliwa na pia hangeweza kutimiza masharti mengine kama vile kulipa deni ya

shilingi bilioni saba aliyopokea kutokana na mafamba, mafamba yaliyomwezesha kukwea ngazi ya utajiri. Hii ndio sababu anarejelewa kama kigeugeu, sifa inayochimuzwa katika uk 73. Tunaambiwa kuwa ingawa alikuwa mweupe kuliko theluji, mara kwa mara alikuwa akibadilikabadilika rangi na kuwa mweusi hasa wakati wa majira ya alasiri kiasi cha kuupiku weusi wa U. Yaani mchana alikuwa mweupe pepepe ilhali usiku aligeuka na kuwa mweusi tititi wala hakuna aliyejua chanzo cha kubadilika kwake, hali iliyomfanya arejelewe kama kinyonga. Madai ya wengi yalikuwa kwamba, alibadilika kulipotokea hatari na katika wakati huu alijikunyata na kujifanya munglu orage. Katika uk 154, Maotad anaghadhabishwa na Avadi kwa kuhama sayari ya NUKA iliyoongozwa na mafamba ilhali ndiyo yaliyomwezesha kupata vyote alivyokuwa navyo kama vile magari, mashamba, nyumba, makaburi, mito, makahaba na akiba katika sayari nyingine. Mbali na ukatili wa Maotad unaochimuka, pia ni wazi kuwa Avadi alikuwa mfisadi aliyekubali kupokea fedha na kulimbikiza mali kwa njia zisizofaa.

Akiwa katika mkutano na Kundi la Amrao, alipokea simu ambayo ilikuwa chanzo cha kudhulumiwa na Maotad (uk 147-150). Kupitia dhuluma hizi, wasiwasi, woga wa kifo na huzuni uliomwingia unachimuka. Baada ya kutoka kwa mkutano, yeye pekee hafiki nyumbani kwake. Alipokuwa mita sabini kabla ya kupinda na kuchukua njia ya baraste iliyoelekea kwake, alikabiliwa na magari mawili, moja mbele na lingine nyuma yasiyokuwa na nambari za usajili na yenye mataa yaliyompofusha. Avadi alichukuliwa na kubebwa unyounyo hadi eneo alilolifahamu, lililokuwa na kasri zuri la kifahari lenye mandhari ya kupendeza ila tu lilikuwa na sifa mbaya, hakuna aliyelifikia akatoka akiwa salama. Kabla ya kuanza safari ya kuelekea asikokujua, alikuwa akitiririkwa na jasho huku moyo ukimpwitika sababu ya woga. Baada ya kufika, alianza kusaga meno yake na kutetemeka kwa woga, akili yake ilienda matembezini na kumfanya akumbuke miji miwili: Odessa na Sobibor ambayo hakufahamu kama ilikuwepo ama

kama ilikuwa katika ulimwengu wa kufikirika, ni majina yaliyokuja akilini mwake kwa kubadilishana, ishara ya kuchanganyikiwa. Ndani ya chumba kimoja, alishtuka sana na maandishi aliyoyaona (uk152):

'WHOEVER ENTERS HERE BECOMES A CADAVER'

'Kila anayeingia hapa hutoka akiwa maiti' (tafsiri yetu)

Alipatwa na mshtuko mkubwa wa moyo, jasho, maumivu makali, kusisimkwa na malaika na kuzirai, yaani alisita kwenda kwa woga ambapo alifanyiwa huduma ya kwanza na watu wale iliyomkumbusha kuwa mtu hakatai wito, bali hukataa aitiwalo. Baada ya kichapo cha mbwa, anaitikia kuasi BORA na kurudi NUKA ili waweze kunuka pamoja na wanasayari wa NUKA na kuendeleza mafamba.

### 3.2.5 ASKARI WA MAOTAD

Hawa walikuwa watiifu, wenye kuzingatia utaratibu, walifuata maagizo yote bila kuvunja hata moja na aidha walikuwa nadhifu, sifa zinazochimuka katika uk147-148. Walimlazimu Avadi aingie ndani ya gari la mmoja wao, tendo walilofanya kwa utaratibu kwani walimjua na kwa kuwa hawakutaka kumdhuru kuzingatia maagizo waliyokuwa wamepewa, kuwa wampeleke akiwa hai na wala sio akiwa mfu. Tunaambiwa kwamba walifanana kama reale kwa ya pili kwa wingi wa mambo kama kimavazi, kiumbo, rangi ya ngozi zao na sauti. Mathalani, walikuwa kama futi saba na nchi saba, yaani warefu kama mlingoti, walisimamisha magari waliyokuwa nayo kwa pamoja, wakaondoka nje kwa wakati mmoja bila kuwepo hata tofauti ya sekunde, walivalia miwani myeusi iliyokuwa na chapa ya polisi, wote walikuwa na upara kichwani uliong'ara kama kioo kwa kupakwa mafuta mengi, viatu vyao vilikuwa na stileto na vilikuwa na

ncha kali mbele na nyuma kama vya mchunga ng'ombe, ncha ya mbele ilikuwa ya chuma nayo ya nyuma ilikuwa ya mpingo.

Pia, walikuwa na utaratibu wa kiwango cha juu. Kwanza, walimuonya Avadi dhidi ya kutozingatia maagizo kwa kuwa kufanya hivyo, kungekuwa ishara ya kukata tikiti yake ya kwenda jongomeo. Walipofika mwisho wa safari yao, walisimamisha gari kwa utaratibu hivi kwamba hata injini yake ilisita kwa utulivu mwingi. Walipoanza kutoka ndani ya gari, viatu vyao vilitangulia huku vikikanyaga chini kwa nguvu na ncha za chuma zilizokuwa zikimeremeta kwa mwangaza wa taa za nje za kasri lile. Baadaye, walitoka nje kwa pamoja na kumwelekeza Avadi katika chumba kimoja kilichokuwa baina ya vyumba vingi vya kasri lile. Maotad alipowaitisha bastola ili amwangamize Avadi, askari hawa walitoa bastola mbili zilizokuwa na ramia kama kumi kwa pamoja, dalili ya mafunzo mema.

### 3.2.6 Nuhu

Alikuwa na macho mekundu ya kikombe na mweusi kama mpingo, weusi uliokolea zaidi usiku wa manane. Alikuwa mpatanishi shupavu wa makundi ya akina Amrao na LiMioe, sifa inayochimuza kutokana na ufafanuzi ufuatao. Kulingana na mwandishi katika uk 139-140, alikuwa nahodha anayefanikiwa kuvusha ng'ambo merikebu hizi mbili bila kupigwa na dhoruba yoyote na kwa kuwashinda nyangumi wote. Aliweza kuwaalika wote waliotaka kuabiri meli hii pamoja nao ili kuwakinga na mvua ya masika iandamanayo na gharika. Hata hivyo, kuna wengine waliabiri na wengine wakabaki wakiwacheka, hawa walipigwa na bumbuazi baadaye kwani hawakuamini matokeo. Kwanza alileta kundi la Fadhila, Boyi, na LiMioe pamoja halafu akawapatanisha na kundi la Amrao na halafu akawahimiza watu wajiunge nao kwani aliamini kundi hili lingeibuka na ushindi. Alikuwa mchache wa maneno ila mwenye hekima nyingi,

iliyofanikisha mradi huu wa upatanisho. Aliwatolea mifano kadha, hasa historia ndefu ya makundi ya Karifa yaliyoshindwa kuja pamoja na hivyo wakashindwa kuwang'oa vinara waovu. Mathalani ELIMO-FR na NUZAPIFU zilizokumbwa na tamaa ya uongozi mwanzoni kabla kuja pamoja. Tamaa iliyochelewesha uhuru wao kwa muda mrefu na kwa njia hii kuzidisha dhuluma kwa wanyonge, dhuluma iliyofikia hatma baada ya viongozi kuamua kuungana pamoja na kupigania uhuru. Aliwakumbusha akina Boyi kwamba umoja kati yao ungepatikana baada ya kumchagua kinara mmoja ambaye angefuatwa na wengine. Kulingana na Nuhu, watu wa Bikerani-Msiige walihitaji dereva mpya ambaye angeweza kuzitawala sayari nyingi kwa pamoja ikiwemo sayari ya NUKA iliyokuwa imetawala tangu kupatikana kwa uhuru.

### 3.2.7 SHANATA

Alikuwa kama manju wa NUKA na kwa hivyo alirejelewa na watu wengi kama kasuku, ukasuku uliowafanya wengi wamfikirie kuwa mbulukwa (uk 129). Aliaminika sana na Maotad na alikuwa rafikiye wa kufa na kupona. Shanata alikuwa amefariki mara kumi na kufufuka mara kumi na moja. Mbali na kufa na kufufuka, yeye hakujua kama aliwahi kufa hata mara moja, wenyeji wa sayari ya NUKA walifahamu kuwa alikuwa amekufa mara kumi na moja naye Maotad alijua kuwa ilikuwa mara yake ya kumi na moja (uk 13).

Alikuwa na miaka mingi ambayo mwenyewe hakutambua ilikuwa mingapi kwa sababu kila alipozaliwa alisema umri wake ulikuwa mara mbili kuanzia kuanzishwa kwa sera ya mafamba, sera iliyoanzishwa miaka 400 iliyopita na kwa hivyo alizidi mafamba kwa miaka 400. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa Shanata alikuwa kipofu ambaye alifuata maagizo ya Maotad bila kujali matokeo ambayo yangemsibu au kuwakumba wengine.

Alikuwa na maumbile yasiyo ya kawaida, mazoea ya kufanya mzaha na kuinamisha kichwa chake chini huku akiigusisha pua yake chini. Pia, alikuwa na maumbile ya kutisha licha ya kuwa kipofu, alikuwa na meno mawili marefu na tena makali kama wembe. Jino moja lilikuwa refu kama futi kumi na saba nalo lingine fupi lilikuwa futi saba. Lile dogo lilijikunja na kuwa kama herufi C, nchani mwa hiyo C liliota kipande cha nyama ambacho ndani yake mlikuwa na kiasi kikubwa sana cha chumvi (uk 20). Ni dhahiri kuwa Shanata alinyenyekea mbele ya Maotad licha ya kuwa alivunja amri mara kwa mara kutokana na ujeuri wake, tendo lililopelekea apate adhabu kali mara kwa mara.

Mara kwa mara alikuwa nadhifu kama siku za kampeni alipovalia kasabu safi, hanjari kutoka Manga huku akiwa amejitia ituri iliyonukia. Alionekana kutojali wakati mwingine na angetafuna tambu alizotoa kwenye kijaluba kilichokosa rangi yake.

### 3.2.8 NIKIABI

Alikuwa na urefu wa futi kumi na rafiki mkubwa wa Maotad. Anadhihirika kama mshauri mkuu wa Maotad hivi kwamba alikuwa mkono wa kulia wake na mwenye jicho moja tu lililotekeleza kazi ya macho mawili. Ni jicho lililokuwa na majukumu kadha wa kadha na liliona mbali sana (uk 11-12). Lilitumika kuchuja viwango vya mafamba na kuangalia ikiwa mafamba ni kamilifu. Licha ya uhusiano wa karibu na Maotad, Maotad alimpuuza mara kadha na kumtaka aondoke katika utawala wa NUKA ila tu Nikiabi alikataa kabisa kwenda kutokana na ukaidi wake. Ilisemekana kuwa hakuwa na mke bali wanawake na kwa hivyo alijiona kuwa kiumbe aliyezaliwa na nguvu zote za kiume na kwa namna hiyo hakuwa hanithi kama walivyofikiria wengine.

### 3.2.9 NGWENA

Alitoka sehemu yenye mto mkubwa na alifahamika sana kwa kurusha cheche za matusi dhidi ya wale waliompinga LiMioe. Alikuwa kiongozi ambaye msimamo wake haungeweza kutabirika hasa wakati wa kutoa hotuba hata na stadi wa maisha ya falaki. Kwa sababu hii, alizidisha maadui baada ya hotuba yake huku hasidi wake mkubwa akiwa ni Amrao. Mivurugano kati yake na Amrao ndiyo iliyofanya abatizwe jina Ngwena. Kutokuwa na msimamo ndiko kulikofanya akorofishane na LiMioe mara kwa mara kwa madai kwamba Azimio la Siri ya Mbuyu au la Mwaujua Mbuyu halikuwa kamilifu miongoni mwa masuala mengine (uk 215-221). Kwanza anamfahamisha kwamba ndege, mumbi aliyekuwa amemchagua kama ishara yao wakati wa kupigia debe Azimio hilo ni alama ya kisirani. Pili, alimfahamisha kuhusu umuhimu wa kuteua viongozi wa mashinani mbali na Damisi aliyekuwa msimamizi wa kampeni hizo. Tatu, alimkumbusha LiMioe kwamba sehemu kadhaa katika Azimio zilikuwa na dosari na kuwa maadui wao wangezitumia sehemu hizo kuwapiga vita. Mathalani, mamlaka ya kinara yaliyokuwa yanapingana na wananchi, suala la urithi aliliona lenye walakini kwani katika jamii, urithi wa ardhi ulikuwa wa wavulana na wala sio wasichana. Msaidizi wa kinara hakuwa na mamlaka hata kidogo, hakuwa na jukumu la kuwateua wasaidizi wakuu na manaibu wao. Alimfahamisha pia kuwa, aliyegombea ukinara hagombei mashinani na kwamba kulikuwa na kosa la kuingizwa kwa mahakama za kidini. Kulingana na LiMioe, ingawa Azimio lilikuwa na walakini, jukumu lao la muhimu lilikuwa kueneza uzuri wake na kuitetea kwa kutoa sababu iwapo wangeulizwa jambo kuhusiana na walakini hizo. Ni wazi kwamba, viongozi wengine ingawa wanatambua kuwa utekelezaji wa jambo fulani kutasababisha madhara kwa jamii, wao hunyamaza tu na kuzidi kuunga mkono suala hilo kwa sababu hawataki kushirikiana na upande

unaotetea ukweli kwa kuwa ndiko mahasidi wao wanakopatikana au labda kwa sababu wanafaidika kwa njia moja au nyingine.

### 3.2.10 ARIJOJO

Arijojo ni mwakilishi wa watu wa Bikerani-Msiige. Alikuwa na nywele zilizokuwa kokakuu na zilizounga neno YATSRA ziliposokotana ila zilipoangaliwa kwa makini maneno hayo yalikuwa YATRSA. Alikuwa na mwili mdogo sawa na kidurango ingawa alikuwa *Homo Sapien Sapien*. Alipoulizwa umri wake alisema kuwa alifikiri alikuwa na miaka ishirini na mitano lakini kutokana na maoni ya waliomfahamu, Arijojo alisemwa kubisha umri wa miaka ishirini na mitano miongo saba iliyopita katika kipindi hicho. Kutokana na maelezo haya, mateso yaliyowasibu wakazi wa Bikerani-Msiige kwa muda mrefu kutokana na dhuluma za Maotad zinachimuzwa kwa uwazi zaidi kupitia Arijojo.

Aidha, tunaambiwa alikuwa na rangi ya kijani kibichi iliyobadilika pindi tu aliporudi ndani kwenye kibanda chake chenye mlango wa kumbesa baada ya kuiepuka miale mikali ya jua. Rangi yake ilibadilika na kuwa ya kijivujivu, rangi ambayo mwenyewe aliichukia. Hii ni rangi ambayo tunaweza kuihusisha na ya jivu lipatikanalo baada ya kuuwasha moto, kuutumia kutekeleza mahitaji muhimu kama upishi wa chakula kizuri na baadaye jivu hili kwa kuwa huwa halina maana tena, mpishi hulitoa na kulimwaga katika pipa la takataka. Kwa namna hii tunajulishwa dhuluma ambazo wakazi hawa walipitia baada ya kuwapigia viongozi kura, haki zao hazikutimizwa, walionekana kama viumbe wasio na faida na walidharauliwa kwa sababu hawakuwa na chochote ila tu kura waliyonunuliwa na viongozi kwa bei rahisi na baadaye kusahaulika kwa miaka mitano pale shughuli kama hii ilitekelezwa. Hii ndio sababu mtunzi

atatueleza kuwa Arijojo aliamini kuwa akiyanywa maji matamu, rangi zake mbili-ya kijani kibichi na kijivu zitabadilika na kuwa nyekundu, yaani atakuwa pia akiogopwa na kuheshimiwa.

Hali kadhalika tunajuzwa kwamba, moyo wa Arijojo ulikuwa sawia na wa binadamu wa kawaida kwa sababu uligonga kadri ya mara 72 kwa dakika moja, sawa tu na wa kiongozi wake Maotad. La ajabu ni kuwa, nyoyo zao zilikuwa tofauti zilipolinganishwa licha ya kuwa reale kwa ya pili kwani ziligonga mara 72 kwa dakika. Kwa hiyo, dhuluma za Maotad dhidi ya wakazi wa Bikerani-Msiige zinachimuzwa. Moyo wake ulikuwa mgumu sana hivi kwamba hakuathirika wala kutoa msaada kwao kutokana na hali mbaya iliyowakumba wakazi hawa ingawa walimwezesha kupata fursa ya kuyanywa maji matamu. Hii ndio sababu nyoyo zao zinadhihirishwa kuwa tofauti kutokana na sifa zao tofauti za ustawishaji wa jamii. Ukweli ni kwamba kama asemavyo mwandishi katika ukurasa wa tatu kuwa sifa za binadamu ndizo huwatenga na wanyama wengine kwa kuwa hata zile sifa za binadamu ambazo tunaona zikiwaleta pamoja kama kundi la binadamu hutokea kuwa tofauti.

### 3.2.11 SAIGEO

Saigeo alikuwa mwanasayari mashuhuri wa NUKA aliyehusika katika shughuli muhimu za uendelezaji wa mafamba. Tunajuzwa kuwa alikuwa kiumbe mwenye shingo ndefu mno na alikuwa na hekima nyingi. Kupitia kwake, mwandishi anachimuza utawala mbaya uliohusisha ufisadi na ulioendelezwa katika sayari ya NUKA. Duru za kuaminika zilibainisha kwamba, Saigeo alikuwa mshiriki mkuu katika kadhia za mfuko wa vito ila tu kwa sababu ya kuenea kwa ithibati za aina hii alitiwa muhuri wa nopro kwa sababu alikuwa mwenyeji wa NUKA na kama ilivyokuwa kawaida yao, muhuri huu ulitiwa kwa mhusika yeyote wa NUKA ili kumpa mamlaka ya kuendeleza mafamba. Nopro ilikuwa sera nyingine muhimu na rasmi iliyotukuzwa katika

NUKA, ilikuwa mfano wa cheti maalum cha kumwalika na kumpa yeyote ruhusa ya kushiriki katika mafamba. Hivyo, ingawa alishiriki katika nyendo hizi zilizoharibu uchumi wa nchi, hakuchukuliwa hatua kutokana na sera rasmi za NUKA na aidha kwa kuzingatia ukweli kuwa alikuwa mwenye hekima ya kiwango cha juu. Aliweza kuyafikia makuu na kutenda mabaya kwa kuwa alikuwa na shingo ndefu iliyomwezesha kuona yaliyokuwa yakitendeka katika sekta mbalimbali, kula na kunywa vyote vizuri na vibaya ambavyo vilimvutia na kumpendeza bila utambuzi wa wakazi wa Bikerani-Msiige.

Katika sayari ya NUKA, wanyonge hawakupewa haki ila wenye uwezo kama Saigeo ambao walitunukizwa zawadi ya nopro. Huu ni ukweli unaochimuza kwa uwazi kutokana na nyendo potovu, hasi na za kinyama zilizotekelezwa na wenye nguvu. Vigogo hawa waliachwa huru hata baada ya kutekeleza maangamizi makali, wangepelekwa mahakamani lakini alasiri ya siku hiyo hiyo mhusika wa kitendo hicho angepata muhuri wa nopro. Mwandishi anadhibitisha wazo hili kwa kutoa mfano unaochimuza dhana kwamba, waliotekeleza maovu licha ya kufahamika na kuchunguzwa, baadaye waliwekwa huru na kesi zao kutupiliwa mbali. Mathalani, aliyehusika katika mauaji ya kikatili kwa njia ya kumkatakata mwenzake au jirani yake kwa kitara na halafu kuikaanga nyama yake kwa mafuta na nyanya kisha akayang'oa macho yake, akayachemsha na kutengeneza mchuzi rojorojo na vilevile akakiweka kichwa chake nje ya mlango wa nyumba yake pamoja na bango ili kuonyesha kuwa ndiye muuaji angelikamatwa lakini hatimaye angeachiliwa kama ishara ya kumpa cheti cha kutekeleza maovu zaidi (uk 88).

### 3.2.12 MASTANJI

Alikuwa rafiki mkubwa wa Maotad kabla ya kutokea uhasama kati yao na hatimaye kuwa maadui wasioweza kupaliana moto, sifa inayochimuza katika uk 46-47. Tunajulishwa kuwa

zamani walikuwa marafiki wakubwa waliokunywa, kula, kucheza mpira wa golf, kuogelea, kulia, kucheka, kucheza *salsa na waltz*, kufa na kufufuka, na hali kadhalika kustarehe na wake wao mbalimbali kwa pamoja. Aidha, alikuwa na mamlaka makubwa katika NUKA aliyopewa na Maotad kabla ya kutorokea katika sayari ya ASIFO. Hili lilitokea baada ya Mastanji kumzaba Maotad kofi zito la kinywa lililomwangusha chini hadi akashindwa kulijibu, hili ni jambo lililokuwa mwiko kufanywa. Maotad hangeweza kulijibu kwa sababu alijipata ameezekwa konde kinywani lililokuwa takriban mizani mbili. Ishara kwamba Mastanji alichukizwa na nyendo mbovu za Maotad na kuamua kumpa mgongo, jambo lililomkasirisha sana Maotad ambaye alimchukulia hatua katili kama ilivyokuwa kawaida yake.

Amri katili iliyotolewa na Maotad dhidi ya Mastanji iliyabadilisha maisha yake milele. Maotad aliamua kumtengea chumba kimoja cha Mkanganyeni kwa jina lingine Auschwitz, jumba la takriban orofa 77 lililokuwa na sifa mbaya, lililopigania kufikia mawingu kwa urefu na lililokuwa na bendera ya sayari ya NUKA iliyopepea juu angani. Vyumba vya juu vilitumiwa na utawala wa Maotad kwa shughuli zao rasmi navyo vya chini 7 vilitengewa wale waliomzaba kofi Maotad kama vile Mastanji na wengine kama Charu, Amrao waliopata kuyazuru mastakimu hayo. Mastakimu ambayo yalikuwa na matokeo matatu, kuingia na kutoka, kuingia na kutoka nusu binadamu au kuingia na kutotoka kabisa. Akiwa hapa, Mastanji alilishwa siafu, pilipili, shubiri na sumu ya *anaconda* kama kifungua kinywa, mlo wa mchana alipewa maji ya batari, vipande vya chupa, gundi ya viatu, samadi na moshi wa tiari ya magari nayo chajio alitayarishiwa panya wa kuchemshwa, msongareli wa kusagwa, sindano za kusagwa, miiba ya kukaangwa, ulimi wa kinyonga, damu ya nzi na mate ya kombamwiko. Hayakuishia kwa ‘vilaji’ yaani mateso aliyopokea mara kwa mara kila siku lakini yalifululiza hadi chumbani alimopulizia maumivu ambapo hakukuwepo na kitanda, kiti wala zulia. Haya ni maelezo yanayofafanua na

kuchimuza ukatili wa Maotad kutokana na uongozi wake mbaya na jinsi watu wengi walipata kuangamia kutokana na dhuluma za aina hii. Mastanji baada ya kudhihirisha uwezo na matumaini makubwa ya kubadilisha maisha ya wakazi wa Bikerani-Msiige, alikamatwa, akateswa ambapo aliathirika sana na kukatishwa tamaa ya ndoto nzuri aliyokuwa nayo kwa wakazi hawa. Baada ya kuondolewa Mkanyageni, alionekana kiumbe dhaifu tofauti na alivyokuwa ameumbwa na Mungu, hakujielewa tena.

### 3.2.13 ROJOO

Rojoo amesawiriwa kama mtu mashuhuri, ambaye hakutisha na aliyemtii Maotad na sheria za NUKA. Jambo la kutisha ni jinsi kifo chake kilivyotokea baada ya kula chapati moja na vipande saba vya nyama ya ng'ombe ambavyo havikutiwa sumu. Ilisemekana kwamba, kama vingetiwa sumu hangekufa. Jambo linalochimuza kutokana na maelezo haya ni kuwa, katika utawala wa Maotad, watu wengi wazuri na mashuhuri waliangamizwa wala sababu ya vifo vyao ilibakia kuwa kitendawili kwa kuwa hata uchunguzi ulipoanzishwa haukufua dafu kutokana na vikwazo vilivyowekwa na wenye kutekeleza maovu hayo.

### 3.2.14 BWANA $O_2$

Alikuwa babake Amrao. Alikuwa wa kwanza kuwazaba makofi viongozi wengi wa sayari nyingi ikiwemo wanasayari wa NUKA. Kulingana na wakereketwa wengi, Bwana $O_2$ alikuwa tegemeo la binadamu la kuishi kwa sababu alikuwa kama hewa ya uhai ambayo ikikosekana maafa mengi na makubwa yangetokea (uk 49). Alikuwa simba wa kukabiliana na viongozi kama Maotad, sawia na alivyokuwa mwanawe Amrao. Maana inayochimuka hapa ni kuwa, Bwana $O_2$ alikuwa mkali sana aliyekabiliana na viongozi ambao hawakuwajibika kama Maotad kwa sababu hakuwaogopa, sifa iliyobainika hata kwa mtoto wake Amrao. Alipendwa na wengi kwa kuwa

alitetea haki zao na kwa namna hii kumwona kama mkombozi wao aliyekuwa na uwezo wa kutimiza ndoto zao kuu za ukombozi walizoziota kila uchao.

Bwana $O_2$ alijulikana na wengi kutokana na tabia ya kuhubiri haja ya ushirikiano. Hii ni sifa inayochimuka katika uk 104, ambapo tunajulishwa kwamba, wazo mojawapo alilolihimiza ni jinsi ya kujihami dhidi ya mahasidi kwa kuinywa damu ya nungumaria. Damu ambayo haikupatikana kwa urahisi ingawa iliponywewa ilitoa hali ya kuchanganyikiwa ama 'konfushon'. Hii ni 'injili' iliyogusa kundi la BORA lililoamua kushirikiana kwa lengo la kushambulia vilivyo kundi la U na Maotad walilotaka kuporomosha kwa mara ya kwanza katika historia.

### 3.2.15 BWANA PAKA

Hili ni jina la kimajazi alilopachikwa kutokana na sura yake iliyojaa masharubu mekundu na aidha alifanana na paka shume aliyeonja damu mbichi. Bwana paka alikuwa kiongozi wa kampuni ya mfuko wa vito na kwa namna moja au nyingine wanachama wake walikuwa akina Avadi. Yeye alipenda kuyanywa maziwa ya wakazi wa Bikerani-Msiige kwa kuyauza na kusema ni vito vya thamana. Kwa mintarafu hii, ufisadi ulioendelezwa katika sayari ya NUKA unabainika na kuchimuza kwa uwazi.

### 3.2.16 ENGINEER

Kupitia kwa Mzee Twajua, tunatambua kwamba Engineer alikuwa mfisadi maarufu aliyehusika katika kubomoa taifa badala ya kulijenga kwa sababu ya ubinafsi wake uliomfanya asahau wananchi. Aliufanya utawala wa BORA kupakwa matope kutokana na nyendo zake chafu, alikuwa kiwakilishi cha mafamba na nopro katika utawala huu, masuala yanayochimiza katika uk 204-211. Alishirikiana na wauzaji katika kujipatia mabilioni ya pesa kutoka kwao. Kazi yake ilikuwa kuandika orodha ndefu ya vifaa vilivyohitajika katika kutekeleza mradi fulani na halafu

kujumlisha hesabu ya vifaa vyote kulingana na bei ya *angolalasting* wala hakuvinunua ila waligawana pesa hizo na muuzaji huku akijipatia fungu kubwa. Mathalani, kama alivyofanya baada ya kuagizia vifaa kadha kama vile tarakilishi mia saba za kisasa, magari ishirini na saba ya spouve V7, satlaiti ishirini na saba za kufichua aliko adui, chupa mia saba za kemikali ya maabara ya kufichua alama za vidole, mashine ya kisasa ya kutengeneza pasipoti za usafiri za kwenda sayari za nje za kielektroniki, monawari wahedi ya kivita iliyo na uwezo wa kubeba ndege saba aina ya F-16 na MiG yenye uwezo wa kemikali za kivita sabini na saba na korodani saba. Ni hesabu iliyofika shilingi bilioni 66 lakini kwa sababu ya tamaa yake, Engineer aliandika hundi ya 666, bei ya *angolalasting* ambapo bidhaa zenyewe hazikuagizwa lakini zililipiwa. Muuzaji aliweza kupata fungu lake la asilimia ishirini ili asitoboe siri.

Kwa kuwa pesa hizo zilikuwa nyingi za kuhifadhiwa katika benki za jamii zetu na kwa kuwa hakuna aliyekuwa na hela kama hizo ila Engineer pekee, ilihalifu azipeleke katika sayari za nje na kuziweka katika akaunti yake ya kibinafsi. Tendo hili lilikuwa chanzo cha kuyumbayumba kwa sayari ya BORA baada ya hela hizo kutolewa katika hazina yake kuu. Hivyo, shida tofauti katika jamii zilianza kubainika kama vile kuadimika kwa dawa katika hospitali, kupungua kwa bajeti ya elimu na ya kukarabati barabara, kupigwa kalamu kazini kwa watu pasi na sababu ya kuridhisha, kuongezeka kwa uvunjaji sheria, kubakwa kwa watoto na kuhangaishwa kwa wanawake, kupanda maradufu kwa gharama za kawi na kuporomoka kwa majengo katika mji wa Kar Pir Mang'ich kulikosababisha vifo vya watu wengi. Ni ujenzi ulioidhinishwa na tume ya Kar Pi Mang'ich ambapo wenye majengo walitoweka baada ya kufanya kazi mbovu. Shida hizi miongoni mwa nyingine zilifanya utawala wa BORA uanze kuagiza msaada kutoka sayari za mbali ukiwemo wa mbwa, yaani hata vitu ambavyo vingeweza kupatikana kwa urahisi katika jamii zetu.

Ongezeko la uharibifu na ukosefu wa amani ulisababisha wananchi washangae kwani vyombo vya ulinzi pia havikupata kununuliwa na bajeti ya shilingi bilioni 666. Hata baada ya kusemekana kwamba kampuni iliyokuwa ilete ala za kivita ingerejesha shilingi bilioni 666 baada ya mwezi mmoja, imani ya wanajamii iliambulia patupu kwani jina la kampuni lilibanwa, mwenyewe hakutambuliwa na vilevile sayari iliyohusika katika sakata hiyo haikujulikana. Juhudi za wengi waliomtaka ajiuzulu kama vile watu kutoka serikalini na upinzani ziliambulia patupu kwa sababu Engineer alikataa abadan kufanya hivyo. Ilimbidi LiMioe, kiongozi wa BORA amhamishe katika sekta nyingine baada ya shutuma kumwendea. Tendo ambalo bado halikuwafurahisha watu kwa sababu walitaka apigwe kalamu. Kitendo cha Engineer kilifanya sayari nyingine za nje zimtilie vikwazo vya usafiri na kumfungia kutoka sayari ya BORA baada ya kushindwa kujibu swali la kwa nini waliokuwa wakifanya biashara au kazi nao hawakulifahamu tendo hilo. Hata ingawa alijitetea huku akidai kwamba wanasayari hao walifanya hivyo kwa sababu ya kutoridhika kwao baada ya yeye kubatilisha ununuzi wa magari katika sayari zao, tetesi zake hazikusaidia. Wanasayari wa nje walifaulu kumfungia nyumbani au nchini bila kutoka nje ya sayari ya BORA. Ni wazi kuwa hata baada ya utawala wa NUKA watawala wa BORA waliendeleza mafamba licha ya kutangaza kwamba wangeyazika milele. Hivyo basi, mafamba katika utawala wa BORA yalisaidiana na mafamba katika sayari nyingine kwa chapa mpya au sakata ya *Angolalasting* kama ilivyokuwa mafamba ya sakata ya mfuko wa vito katika utawala wa NUKA.

Alikuwa mkwasi aliyepata pesa zake kutokana na ufisadi na kuzitumia kwa mavazi ghali pamoja na familia yake, mavazi yaliyobainisha kiwango chao cha ukengeushi tofauti na wakazi wengine waliokuwa maskini kupindukia (uk 201-204). Engineer anapofika katika kibanda kimoja katika soko la Tuga Amor wakiwa na familia yake, mavazi yao na mienendo yao inabainisha jinsi ni

matajiri na kiwango chao cha juu cha ukengeushi. Ukweli unaodhihirika kwa jinsi walivyovalia mavazi yenye chapa ya *angolalasting* na yaliyokuwa ya mabilioni ya pesa. Tunaambiwa kuwa alivalia suti ghali yenye rangi ya kijivujivu, tai nyeusi yenye madoadoa meupe na shati ya samawati, nguo, viatu, tai na vifungo vya suti yake vilikuwa na chapa ya *angolalasting*. Hii ndiyo iliyokuwa fasheni na heshima za mtu na familia zilitokana kwa kuvaa chapa hii nako kutovaa kulivunja heshima hiyo. Bibiye Engineer alivalia mapambo ya dhahabu kama vile kuti, jazi, vipuli, vipini, vishahasi na vidani. Msichana wao alikuwa mashuhuri katika kuvaa kibiritingoma, viatu vyenye ncha ndefu na vilivyobusu ardhi kama vya mama yake. Mvulana wao alivalia suruali kubwa iliyozidi babake kiasi mara tatu, sehemu ya makalio ya suruali iligusa chini na ilivaliwa kinyume huku mbele ikiwa ndiyo nyuma na nyuma ikiwa ndiyo mbele, zipu ya mbele ilikuwa nyuma, mifuko ya nyuma ilikuwa mbele, nywele zake zilinyolewa na kusalia sehemu ya kisogo, alikuwa ametoboa mashimo matatu katika kila sikio na kuweka vigome na mashahasi. Ni dhahiri kwamba haya ni maisha yaliyofurahiwa na wachache waliobahatika kupata nafasi kubwa katika sayari ya NUKA na BORA tofauti na wakaazi wa Tuga Amor na Bikerani-Msiige waliotegemea bidii yao katika vibarua ili aghalabu wapate chakula na mavazi.

### 3.2.17 JOGI

Alikuwa afisa mkuu wa kuzima mafamba na nopro katika sayari ya BORA baada ya kuteuliwa na LiMioe. Alikuwa mfano wa kiongozi mzuri aliyewajibika katika kazi yake, ukweli unaochimuka katika uk 209. Anabainika kama shujaa aliyetekeleza wajibu wake kama ilivyopaswa ila tu alitorokea katika sayari jirani kusalimisha maisha yake yaliyowekwa hatarini baada ya kufichua wizi uliofanywa na Engineer. Kwa mujibu wa majukumu aliyokuwa amepewa, alizindua makosa aliyotekeleza Engineer akiwa katika makao yake makuu ya kutungia sheria za sayari ya BORA. Sakata iliyoibua nadhari kutoka kwa wanasayari wa BORA na wa nje

na iliyopata kufahamika baadaye kama *angolalasting*. Baada ya kuweka wazi sakata hii iliyopata kujulikana na wanajamii kupitia kwa nyenzo mbalimbali za mawasiliano, Jogi alihofia maisha yake na kutorokea sayari mojawapo ya nje ili kuokoa maisha yake. Hivi ndivyo ilivyo katika Afrika ambapo viongozi wanaojaribu kuzindua maovu yanayotekelezwa na viongozi mbalimbali hutishwa kwa njia tofauti baada ya kusema ukweli, jambo ambalo hupelekea wengi kuhofia kuwajibika kazini na kwa namna hii kusababisha ongezeko la utekelezwaji wa maovu.

### 3.2.18 MADAKTARI WA BIANDI NA BAE

Hawa ni madaktari waliokuwa na mabawa na waliokuwa na nia ya kumfanyia Maotad upasuaji ili kumzuia kutokana na madhara ya ufunguo aliokuwa ameumeza kwa miaka 40. Kwa njia hii, walitaka kumwangamiza kupitia ajali ili mwingine apate nafasi ya kuongoza. Kutowajibika kwa hawa madaktari ndiko kumechimuzwa kwa uwazi, hasa wa kutoka Bae. Daktari mkubwa hapa aliyejulikana kama Kachuoheze alitambulika kwa pupa yake ya kutafuta kila mara maji ya kumtibu Maotad lakini hakufaulu. Katika kisa kimoja, bila ufahamu wake, aliukata mguu wa mgonjwa aliyehitajika kung'olewa jino na aidha katika miaka alikuwa ameupasua moyo wa mgonjwa aliyehitajika tu kukandwa mkono. Licha ya juhudi zao, malengo yao hayakutimizika kwani Maotad aligundua njama zao na kutupilia mbali huduma zao na halafu akawatafuta waajiri wengine baada ya kuwafuta kazi. Kama asemavyo mwandishi katika uk 81, Maotad alimtibu bwana Kachuoheze na madaktari wa Biandi na Bae kwa njia ambayo iliwafanya wasiwe wagonjwa tena na halafu akawatafuta madaktari wengine wa kumsaidia ambao hawakuwa na mabawa.

### 3.2.19 KASISI MUMU

Alikuwa kiongozi wa kanisa aliyekuwa na imani kuwa mbali na LiMioe, Boyi na Fadhila, kungetokea mtu mwingine ambaye angekabiliana na U. Hakuwa na msimamo, alikuwa kigeugeu wa vigeugeu, sifa inayochimuza katika uk 141. Mara kwa mara alibadilisha msimano wake kuhusiana na kundi alilounga mkono. Alifahamika na sifa ya kutoa matamshi yaliyogongana na imani yake kama kiongozi wa dini ingawa kwa namna moja au nyingine alichangia katika uimarishaji wa wakazi wa Bikerani-Msiige. Kulingana na fununu zilizoenezwa, ni kama alipendekezwa kumkabili U iwapo Boyi, Fadhila na LiMioe hawangeweza kukubaliana na kumpendekeza mmoja wao awe kinara.

### 3.2.20 KAMU

Kamu alikuwa mtulivu, hii ni sifa inayochimuza kutokana na tabia yake ya kutulia tuli kama maji ya mtungi kwa masaa ishirini na matano, yaani kwa muda mrefu sana. Alipozungumza, sauti yake haikusikika kwa mbali na kwa sababu hii iliwabidi watu wasongee karibu ili angalau wapate kuyasikia maneno ya hekima yaliyokuwa chungu nzima katika usemi wake. Alijulikana vyema na wakazi wa Bikerani-Msiige na pia na Maotad ila tu hakudhihirisha sifa yake ya ukaidi aliyoificha.

### 3.2.21 KANGA

Hili lilikuwa jina la kupachikwa kwa kuwa jina lake asili halikujulikana. Kanga hakuwa tofauti na ndege anayejulika kama kanga kwa sababu alikuwa na madoadoa. Hakujulikana rangi yake haswa kwa kuwa hakuwa mweusi wala mweupe. Alikuwa mfupi kama nyundo, kimo kilichosemekana kilimfanya awe mtulivu na kumfanya Maotad kumwona kama 'lukewarm'.

### 3.2.22 KANJE

Alikuwa mfuasi wa Maotad aliyemsaidia katika kampeni za kumpigia debe U na tajiri maarufu. Alikuwa mkwasi wa mali kama Maotad. Kulingana na ufahamu wa wengi, shilingi zake hazikuweza kuhesabika, labda alizipata kutokana na sifa yake ya ulukuki. Kunao walioamini kuwa alighushi ugimbi kwa kuchanganya makaa na viazi, nao wengine waliamini kwamba, alifanya biashara ya kuyauza makombamoyo katika sayari tofauti. Kulingana na maelezo haya ya uk 128, ni dhahiri kuwa Kanje alilimbikiza mali kwa kutumia nyendo chafu zisizofaa. Tabia ya ufisadi ya Kanje inachimuka, sifa iliyowatawala wanasayari wengi wa NUKA kwa kuwa walilindwa na nopro.

### 3.2.23 WANABIASHARA KATIKA SOKO LA TUGA AMOR

Hawa walikuwa mchanganyiko wa akina baba na mama waliouza vitu mbalimbali. Kulikuwa na matajiri ambao biashara zao zilikuwa zimeimarika kutokana na mafamba na nopro na maskini ambao walijizatiti kujipatia mkate wa kila siku kwa kutegemea wateja ambao hawakujua iwapo wangejitokeza, ukweli unaochimuza katika uk 197-201. Mathalani, mzee aliyeuza dawa tofauti kama vile chirichiri, shimari, mjafari, sanamaki, koto, shubiri, pachori, pakanga, manemane na tinil-armani. Ajuza aliyepanga viungo mbalimbali vya vyakula kama mdalasini, karafuu, pilipili manga, mchikicho, bizari, zafarani na loza alivyovibeba kwa kutumia kikapu kilichochakaa. Alifahamika sana na wakusanya ushuru kwa tetesi zake kali kuwa waliotakiwa kulipa ushuru sio watu kama yeye wasiokuwa na mbele wala nyuma. Aliwaona kama kupe na aliwatusi hadi waliposalimu amri na kwenda zao. Aidha kulikuwa na kibanda cha mama wa makamo cha matunda na mboga kilichosimama kwa uwezo wa mihimili ya fito na chandarua kuukuu ambapo ndizi za aina tofauti kama kiume, mkono wa tembo, mabuki, kisukari na kitofi ziliuzwa. Pia

kulikuwa na maembe, mapera, mikanju, fenesi machungwa, machenza, matufaha na matomoko na hali kadhalika mboga anuwai kama vile mibiringani, sukumawiki na tangopepeta. Katika kibanda kingine, kulikuwepo mama aliyepika chakula na aliyekuwa na wateja wengi. Vyakula alivyotayarisha ni kama vile mkate wa mayai, sinia na mtwabaki. Wanabiashara hawa wanaashiria ukweli kwamba hawa walikuwa watu waliokuwa na nia ya kupata faida ndogo tu kwa lengo la kuwawezesha kuyakimu maisha na jamaa zao, ishara ya hali ngumu ya maisha iliyoendelea kuwakumba wananchi hata wakati wa utawala wa BORA.

Katika soko hili pia kulikuwa na biashara zilizonawiri kutokana na juhudi mbalimbali, hazikuwa za walalahoi. Mathalani, kulikuwa na kibanda kilichotiwa nakshi za aina tofauti za kisasa. Mihimili ya kibanda chenyewe ilikuwa ya vyuma na vitu vilivyokuwa vikiuzwa vilikuwa vya bei ghali kama vile magari makubwa, tarakilishi, chuma, dhahabu, almasi, lulu, akiki na bidhaa za mafuta. La ajabu ni kwamba, walioingia katika kibanda hicho hawakununua chochote ila waliingia na kufanyia vitu vile peksheni na gwaride la heshima na baadaye kubadilishana kadi za kibiashara. Mwanabiashara huyu aliamini kuwa, katika maisha lazima kuwe na mafamba na nopro, jambo alilosema mteja alipokuja na kumpa kadi ya kibiashara iliyokuwa na muhuri wa mapambano dhidi ya mafamba.

### 3.2.24 HITIMISHO

Sura hii imechunguza nafasi ya uchimuzi katika kiwango cha wahusika. Uchunguzi umebainisha kuwa matendo na wasifu wa wahusika yamechimuzwa katika kuelezea migogoro ya kisiasa ya jamii yetu kiasi kwamba tunawatambua wahusika hawa licha ya wao kusawiriwa kwa mtindo wa kimajaribio kupitia kwa majina waliyopewa na mitagusano yao. Pia, tumebaini kuwa njia ya usawiri wa wahusika hawa ni tofauti kabisa na wa jadi ambao wanadhihirisha uhalisia wa kijamii

tofauti na wa riwaya hii ya kimajaribio ya *Mafamba* ambao usawiri wao ni wa kimaajabu hata ingawa kwa hali halisi wanawakilisha binadamu katika jamii.

Kwa mujibu wa sura hii, tumebainisha aidha kuwa, uchimuzi umechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya hii ya *Mafamba*, jambo ambalo linamwezesha msomaji yeyote wa riwaya hii kung'amua kwa urahisi dhamira kuu ya mwandishi ya kuonyesha uozo wa kimaadili kati ya wanasiasa na hali kadhalika kuonyesha maudhui mbalimbali ya ufisadi, dhuluma, ubinafsi, chuki miongoni mwa mengine.

# SURA YA NNE

# UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA MATUMIZI YA LUGHA

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ya nne, tumebainisha uchimuzi katika kiwango cha matumizi ya lugha. Tumeonyesha jinsi lugha ilivyotumiwa katika *Mafamba* imechimuza sifa zinazoakisi maelezo ya Wana-Urasimu tuliyoyazungumzia. Katika matumizi ya lugha, ufasaha wa lugha na ubunaji wa lugha mpya na maneno mapya unajitokeza kwa uwazi katika riwaya za kimajaribio. Tumeangalia uchimuzi katika kiwango cha kisintaksia kwa kuzingatia msamiati, muundo wa sentensi na kiwango cha kisemantiki.

## 4.I UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA KISINTAKSIA

### 4.1.1 UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA KIMSAMIATI

Kiwango hiki kinahusisha uteuzi wa misamiati, kwa namna hii tutajihusisha na masuala ya misamiati. Mathalani, tutajishughulisha na maneno ya Kiingereza, Kiarabu, ya kale, matumizi ya maneno mapya na uchanganyaji ndimi. Tutaangalia athari za matumizi ya misamiati hii katika riwaya ya *Mafamba* kwa kuonyesha jinsi matumizi yake yanachimuza maana mbalimbali katika uwasilishaji wa dhamira na hali kadhalika katika kuondoa uzoevu wa matumizi ya lugha katika riwaya hii.

#### 4.1.1.1 Maneno ya Kiingereza

Maneno ya Kiingereza ambayo yametumika katika riwaya hii yanaweza kugawika katika vikundi mbalimbali. Kwanza, ni maneno ya Kiingereza ambayo hayana visawe katika lugha ya

Kiswahili, pili ni yale ambayo yana visawe lakini mwandishi ameamua kuyatumia katika hadithi. Mwandishi katika riwaya ya *Mafamba* ametumia maneno ambayo hayana visawe katika lugha ya Kiswahili kama *'curl kit'* katika uk 19. Sababu ya kulitumia ni labda kutokana na kukosekana kwa neno hili katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni neno lililoibuka kutokana na mitindo ya kigeni katika muktadha wa ususi. Kwa namna hii, iwapo neno hili lingeelezewa kwa Kiswahili, basi mwandishi angelitoa maelezo kuhusiana na dhana hii, njia ambayo ingesababisha fasili mbaya ya wazo alilonuia kuibua kwa msomaji. Hivyo, matumizi yake labda yalikuwa ya kimakusudi ili kumwezesha kuwasilisha maana halisi aliyokusudia bila kupotosha ujumbe. Sababu ni kuwa alinuia kuchora taswira halisi ya kiti kikuu cha wageni wa Maotad katika sebule yake. Hiki ni kiti kilichokuwa na bakuli ambayo wenye kukikalia walivikwa kama taji, bakuli iliyokuwa sawia na kifaa cha kutengenezea nywele kwa mtindo huu anaourejelea mwandishi *'curl kit'*. Huu ni mtindo ambao unafanya nywele zilainike na unaohusishwa na wenye kujiweza bali sio maskini kama Wakazi wa Bikerani-Msiige. Ni kiti kilichomilikiwa na Maotad pekee na kilichokuwa na nyaya zilizounganishwa na kitovu cha kawi ili kumwangamiza yeyote polepole huku akiwa amestarehe akimsikiza kama ambavyo mhudumu hustareheka akikaangwa nywele zake kwa matumaini kuwa atakuwa nadhifu.

Aidha katika uk 34, mwandishi ametumia neno la Kiingereza *'four course meal'* ambalo halina kisawe chake katika lugha ya Kiswahili. Ili kulielezea, ingembidi atoe maelezo ambayo labda hayangeibua dhana hii kwa msisitizo zaidi kwa mfano kusema 'mlo wa mikupuo minne.' Matumizi ya neno hili basi ni kusisitiza maana aliyokusudia mwandishi. Katika matumizi yake, anaonyesha jinsi Fadhila alivyokuwa mkwasi kiasi cha kuweza kuvalia viatu vilivyokuwa na thamana ya juu ambayo ingeweza kuwakimu maskini wanne kwa miaka minne, kila siku kwa

kwa mlo wa mikupuo minne. Kwa njia hii, mwandishi anachimuza maisha ya kifahari wanayoishi viongozi barani Afrika huku watawaliwa wakisononeka kwa njaa na umaskini.

Hali kadhalika mwandishi ametumia majina yenye visawe katika lugha ya Kiswahili mathalani *'tsunami'* kama ilivyo katika uk 22, 35 na 51. Hili ni neno la Kijapani linalorejelea kimbunga kikali kinachofahamika kutokana na maafa makubwa kinachosababisha. Katika matumizi yake katika uk 22, mwandishi anachimuza mapinduzi yaliyokaribia kwa kishindo kuleta mageuzi katika utawala wa Maotad, na kwa kuwa alikuwa amepata dalili za mapinduzi haya, inambidi basi atafute mbinu za kukaribiana nayo. Mwandishi anasema:

> "Nafsi yake ilimwambia kuwa alikuwa anazidi kuwa mtukutu huku tsunami ikiwadia. Na lazima aitulize tsunami hii".

Katika uk 35, mwandishi analinganisha Maotad na tsunami, kwa kawaida kimbunga huandamana na upepo mkali unaosababisha madhara makubwa sana. Hivyo, licha ya LiMioe kujizatiti kukabiliana naye katika vitimbi vya kumtimua uongozini, hakufaulu kwa sababu mchakato huu uliandamana na mafamba. Hivi kwamba, Maotad alitumia njia zake za ufisadi kupata ushindi dhidi ya LiMioe. Vilevile katika uk 51, ukali wa Maotad unahusishwa na madhara yanayoandamana na 'tsunami' na yanachimuzwa wakati Shanata anamfokea Amrao anayetaka kukikalia kiti kitukufu cha Maotad bila idhini. Anasema:

> "Kifo! Kifo! Damu! Damu! La! Haiwezekani! Mwiko! Uhaini! Tsunami!" alifoka Shanata.

#### 4.1.1.2 Maneno ya Dholuo

Katika sehemu hii, tunaangalia maneno ya Dholuo ambayo yametumiwa katika riwaya ya *Mafamba* ili kuchimuza masuala fulani. Kama walivyobainisha Wana-Urasimu, sanaa ni jumla ya mbinu za fasihi na za kisanaa ambazo msanii huzifinyanga ili kuwasilisha kazi yake kwa

ustadi. Katika uk 20 na 21 mwandishi ametumia neno *'apul apul'* linalorejelea zimwi aliye na maumbile kama ya fisi kulingana na hadithi simulizi ya jamii ya Waluo na ambalo huambiwa watoto wanaolia ovyo ovyo ili wanyamaze.

Katika matumizi yake katika uk 21, mwandishi anaonyesha jinsi waliokikalia kiti kitukufu cha wageni katika sebule ya Maotad kilichounganishwa na nyaya za stima baada ya kumchokoza walivyohasirika. Shanata anapokikalia kiti hiki baada ya kumpa Maotad ushauri wa kushirikiana na sayari ya DiPieLi, jambo ambalo alilipinga vikali Maotad, Maotad anaamua kumzima. Hivyo, anapokikalia anaathirika kiasi cha kuonekana kama zimwi la *apul apul*. Dakika mbili baada ya kukikalia, Shanata anatoa chemichemi ya machozi yaliyobadilika na kuwa damu nzito, damu ambayo haikuwa nyekundu bali nyeusi. Hivi ndivyo alivyogeuka Shanata, binadamu aliyefanana na zimwi la *apul apul* na aliyekuwa na meno mawili marefu na makali kama wembe

Vilevile, kuna matumizi ya neno la Dholuo *'jaduon'g'* linalomaanisha mzee katika uk 92,93,94,97 na 98. Katika matumizi haya yote, mwandishi anachimuza jinsi U alivyoonekana mzee na Maotad na wafuasi wengine wa NUKA kwa kuwa alikuwa mrithi wake Maotad wa kuendeleza sayari yao tukufu. Katika wimbo wa kumtukuza U, wafuasi wa NUKA wanamwamini huyu *'jaduon'g'* ingawa alikuwa katika ngozi ya mtoto. Kulingana nao, U angewapa mambo mema kama mafamba na kuwahifadhi ili waendeleze mafamba. Mwelekeo huu wa Maotad kamwe haukuridhisha wakazi, mwandishi anasema kwamba:

> "Tangazo la Maotad kumhusu jaduon'g lilikuwa ni kombora lililotupwa ghafla na kusababisha madhara makubwa katika kambi ya maadui- LiMioe, Boyi, Sinya, Fadhila na watu wa Bikerani-Msiige hawakuamini" (uk 94).

Matumizi ya neno la Dholuo *'ochunglo'* katika uk 28-29 linaloashiria mdudu mdogo wa jamii ya chungu anayekwenda pamoja na kundi la wenzake na ambaye anafanana na sisimizi. Amrao akiwa kizuizini baada ya kujaribu kukitia kitumbua mchanga, yaani kufanya mapinduzi ya utawala wa Maotad, anaimba wimbo wa kukomesha mafamba daima, huu ni wimbo unaompa matumaini na uangavu kila mara anapoiimba mistari ya wimbo huu. Mwandishi anasema kwamba, ile mistari ya mwisho ya 'kukomesha mafamba' aliiimba kwa nguvu zake zote, nguvu zote alizokuwa amesalia nazo akiwa mle na ambazo hazingeweza kumuua '*ochunglo*' wala kusababisha maumivu kwake. Kwa mintarafu hii, matumizi ya neno hili linachimuza jinsi matumaini ya Amrao ya kumshinda Maotad katika uchaguzi yalikuwa hafifu sana. Hii ndiyo sababu ya mtunzi kusema kuwa, nguvu alizokuwa nazo Amrao hazingeweza kumuuma *'ochunglo'*, yaani mdudu mdogo, wala kusababisha maumivu kwake.

#### 4.1.1.3 Kuchanganya ndimi au kuchanganya msimbo na kuhamisha ndimi au kubadilisha msimbo

Katika uwasilishaji wa maudhui na fani, mwandishi amechanganya ndimi ili kuondoa uzoevu wa kutumia Kiswahili pekee katika uwasilishaji wa ujumbe. Kama alivyosisitiza Shklovsky katika maelezo yetu ya hapo awali, fasihi inao uwezo wa kuifanya hadhira kutazama ulimwengu inamoishi kwa njia tofauti na vile imezoeleka. Aidha, kwa kuwa lugha huipa maana fasihi, lazima iajinabishwe na kufanywa kuwa ngeni kwa kuitumia katika miktadha isiyo ya kawaida.

Kwa mujibu wa Masinde (2007:23), kuchanganya ndimi ni mbinu ya lugha ambapo msemaji hutumia vipashio au mafungu ya maneno ya lugha mbalimbali katika harakati za kutumia lugha moja katika mazungumzo. Matumizi ya mtindo huu katika *Mafamba* mbali na kuonyesha athari ya kujua lugha nyingi, kwa njia moja au nyingine yanatokana na ukweli kwamba, dhana husika

hazingejitokeza vizuri katika lugha moja na hivyo hii ni juhudi ya kutaka kueleweka ipasavyo kwa kukosekana kisawe mwafaka. Katika uk 112 anasema:

> "Nje ya Hakuna Uma, spouve V7 ilijivuta taratibu…."

'Spouve V7' ni muundo wa gari ambao hauna kisawe katika Kiswahili na kwa hivyo mwandishi angetumia jina 'gari' kurejelea muundo huu, basi athari ambayo alinuia msomaji aipate ingepotoshwa. Kwa mintarafu hii, alitaka kuchimuza aina ya magari ya kifahari yanayoendeshwa na viongozi na aidha maisha ya starehe wanayofurahia baada ya kuchaguliwa kuwakilisha wanajamii. Waliokuwamo ndani ni akina Avadi, Kamu, Damisi na Kajo ambao walikuwa na nafasi kubwa katika sayari ya NUKA, sayari iliyofahamika kwa mapana na marefu kutokana na mafamba. Kwa kuwa walikuwa wafuasi wa Maotad, inaarifu kwamba waliishi maisha ya anasa (luxurious) kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao.

> "Magurudumu yake yalikuwa na upana mkubwa- aina ya 277/7 chapa BF Goodrich. Ilikuwa na viti saba kikiwemo kile cha dereva. Spouve V7 ina nguvu zaidi ya mara saba na saba ya Airbus A380" (uk 113).

Aidha, katika uk 197, matumizi ya mtindo huu yametumika lakini hapa sio kwamba mwandishi alikosa kisawe bali inavyodhihirika, alidhamiria kuwasilisha ujumbe wake kwa njia yenye mvuto zaidi ili ujumbe wake uchimuze. Katika kulielezea soko la Tuga Amor, anafafanua namna lilivyokuwa soko la ajabu ambalo lilikuwa na takriban kila kitu, vitu vilivyokuwa na uhai na visivyokuwa na uhai. Anasema kwamba: "Ungeuliza lori jipya la *wide load* ungeambiwa "labeka!", ungeuliza kichwa *fresh* cha binadamu ungeambiwa "hewalla!"…." Katika kuelezea 'wide load' kwa Kiswahili, mtunzi angelielezea dhana hii kuwa 'lori pana la kubebea mizigo' lakini kwa kufanya hivyo, taswira halisi ya makuu yaliyopatikana katika soko hili

hayangejitokeza kwa uwazi zaidi kama ilivyojitokeza kwa kuchanganya ndimi hapa. Hali kadhalika, matumizi yake ya jina 'fresh' pamoja na maneno mengine ya Kiswahili yanaashiria kwamba iwapo jina la Kiswahili 'mbichi' lingetumika kama mbadala wa 'fresh' vilevile athari ya kuchimuza aina ya biashara iliyohusika hapa ya kuwauza hata watu wenye uhai haingebainika kwa urahisi. Kwa mintarafu hii, mbinu za uwasilishaji huibua athari ya uajinabishaji kwenye kazi ya kifasihi kwa kutufanya tuisawiri kwa njia mpya.

Vilevile, kubadilisha msimbo au kuhamisha ndimi alikokufanya mwandishi katika kiwango kingine kunabainisha kwamba, masuala mengine hayangeweza kusisitizika kwa kutumia lugha ya Kiswahili pekee kwa kuwa katika lugha hii, dhana hiyo haina njia nyingineyo ya kuisisitiza hata kwa kutumia kisawe. Mathalani, matumizi ya *'micro-mini'* badala ya kibiritingoma katika mfuatano wa maneno ya Kiswahili. Iwapo neno kibiritingoma lingetumika, basi maana ya neno 'micro' halingeibuka, hivyo, mtunzi alitaka kuonyesha aina ya nguo iliyovaliwa na msichana wa Engineer ambayo mbali na kuwa kibiritingoma ama fupi, ufupi huu haukuwa wa kawaida kwa kuwa ilikuwa fupi sana. Anasema:

> "Majuzi tu alikuwa anacheza foliti ugani. Leo, alichapa micro-mini skirt na blauzi iliyoelewana na micro-mini skirt hiyo- kwa kiwango cha rangi- ya samawati" (uk 203).

Sababu hizi hizi ndizo zinazobainika katika matumizi ya neno *'senior citizen'* katika mfuatano wa maneno ya Kiswahili kama ilivyo katika uk 176, "Mafamba alikuwa ni senior citizen wa NUKA". Kwa hivyo, mwandishi angetafsiri dhana 'senior citizen' labda kwa mujibu wa TUKI (2009:797) kama 'mzee' au 'mstaafu' basi maana halisi haingehisika. Aidha angelifafanua kama kwa mfano 'raia mwenye cheo kikubwa' vilevile ingembidi msomaji kwanza atue kidogo ili atafakari zaidi kuhusiana na maana anayonuia mwandishi. Kwa sababu hii, kuhamisha ndimi

huku ni chaguo la mwandishi la matumzi ya mbinu ainati katika uwasilishaji fani na maudhui ili kuchimuza masuala yenye uzito.

Mbinu ya kuhamisha msimbo pia imetumiwa ili kuchimuza masuala tofauti. Istilahi hii kwa mujibu wa Masinde, (k.h.j) ni pale ambapo mzungumzaji huacha matumizi ya lugha moja na kuanza kutumia nyingine bila kuzichanganya. Kuhamisha ndimi kumeelezewa na wanaisimu kama ubadilishaji wa matumizi ya lugha moja kwa nyingine katika harakati za kimawasiliano (Richards na wengine 1985; Habwe 1990:90). Hii ni tofauti na ilivyo katika ubadilishaji wa kimsamiati (lexical borrowing) , hivi kwamba katika kuhamisha msimbo, maneno hudhihirisha sifa za lugha nyingineyo inayohusika tofauti na ilivyo katika ubadilishaji wa kimsamiati ambapo maneno huhusishwa katika lugha kwa kuzingatia mifumo ya kifonolojia na kimofolojia (Bentahila na Davies 1982 kama alivyonukuliwa na Rayya 2002:). Kwa mfano:

> "Alipewa makoa rasmi na personal assistant. Watu walipouliza mbona, walipata jibu: '*A senior citizen deserves a personal assistant!*' Mafamba alikuwa anaheshimika hata na maskini" (uk 176).

Aidha katika uk 204-205, mazungumzo kati ya Engineer na muuzaji yanaenda hivi:

> *"No problem sir.* Hii haiko hapa lakini nitatumana mpagazi mara moja dukani. *What type sir?" (uk 204).*
>
> "Hapana. *Just had some coffee."*
>
> *"Oh. Coffee? What type?"*
>
> *"Native cofffe.* Kahawa ya humu humu kwetu." (uk 205)

Matumizi ya mtindo huu na mwandishi kama ilivyo katika uk 176 ni labda kwamba, alinuia kuleta karibu suala la muktadha, yaani nafasi halisi ya mafamba na kwa njia hii kuchimuza wazo kwamba mafamba katika utawala wa Maotad yalikuwa na heshima kuu, heshima inayowiana na ya raia mkuu aliye na msaidizi mahususi. Katika uk 204 na 205, mwandishi anachimuza dhana kwamba, Engineer na muuzaji ni watu wa tabaka la juu na kwa mujibu wa mahusiano yao, wanajitambulisha kama kundi la watu waliokengeuka labda kwa kuwa walipata nafasi ya kusoma na kupata ujuzi wa lugha tofauti kwa kuwa walitoka katika familia tajiri tofauti na wakazi wa Bikerani- Msiige ambao ni maskini. Hali kadhalika, labda matumizi haya yanatokana na mazoea yao katika mitagusano yao ya kibiashara ili kurahisisha mawasiliano yao. Sababu za kuchanganya na kuhamisha ndimi kwa ujumla wake huweza kutokana na sababu ya athari ya lugha ya Kiingereza hasa kwa kizazi hiki kipya na kutokana na athari za mitagusano yao na tamaduni nyingi. Matumizi ya lugha hii hujitokeza kama fumbo ambalo msomaji hupaswa kulifumbua na kwa njia hii kuchimuza ujumbe unaohusika.

#### 4.1.1.4 Maneno ya kale

Ukale wa maneno kwa mujibu wa ufafanuzi wa Wales (1989:39) ni kuendelea kutumia sifa za kiisimu ambazo sio za kisasa, aghalabu kwa njia ambayo sio ya kawaida. Anasisitiza kwamba, ukale huu hubainika sana sana katika lahaja za kimaeneo. Istilahi hii kulingana na ufafanuzi wa Iribe Mwangi na Mukhwana (2011:38) ni lahaja zinazomtambulisha mzungumzaji kwa mujibu wa kule anakotoka katika jamiilugha fulani na huitwa pia lahaja za kijiografia. Cystal (1997) kama alivyonukuliwa na Iribe Mwangi na Mukhwana (2011:33) anafafanua lahaja kuwa mtindo bainifu wa lugha kieneo na kijamii unaobainishwa na seti maalum za maneno na miundo ya kisarufi. Polome (1967:19), anasisitiza kuwa katika kuzishughulikia lahaja za Kiswahili, ni muhimu kuweka mpaka baina ya lahaja za pwani na kisiwani ambapo Kiswahili kilikuzwa na

lahaja za bara. Kwa mintarafu hii, neno la kikale 'ng'andu' linalotokana na lahaja ya kingozi linalorejelea dhahabu na linapatikana hususan kwenye tenzi za zamani na halitumiki tena katika mazungumzo au uandishi wa kila siku. Hata hivyo mwandishi amelitumia katika uk 50 ili kuonyesha namna fedha zilitumiwa vibaya na Maotad hata katika unakishaji wa milango kwa dhahabu badala ya kuzitumia katika uimarishaji wa maisha ya watawaliwa.

#### 4.1.1.5 Maneno ya kubuni

Ubunifu wa maneno ni mbinu nyingine inayojitokeza katika riwaya hii. Chopasa ni neno lililobuniwa na mwandishi kurejelea chombo cha kupaza sauti, yaani kwa jina maarufu makrofoni. Chopasa ni mojawapo ya vifaa vilivyopatikana katika sebule ya Maotad vilivyotokana na sera ya mafamba. Kwa namna hii, mtunzi anachimuza uozo wa kimaadili uliokita mizizi. Kweli, ni aibu kwa mtu kama Maotad kumiliki kipaza sauti kwa njia hii potovu. Ugandhi aidha, ni neno lililobuniwa na mwandishi kurejelea mapambano ya amani. Wakazi wanaongozwa na Mzee Twajua kung'amua silaha mwafaka ya kuwang'oa viongozi wafisadi uongozini. Yaani, mapambano ya amani na wala sio kutumia silaha hatari ziwezazo kusababisha umwagikaji wa damu kama inavyobainika katika uk 246. Kwa kulitumia neno hili, umuhimu wa amani unachimuzwa na kusisitizwa

#### 4.1.1.6 Maneno mageni

Maneno mageni pia yametumiwa katika riwaya ya *Mafamba* ili kuchimuza mambo tofauti. Maneno ya Kiarabu, Kilatini, Kijerumani na ya Kibengali yametumiwa. Neno Saadatul-kher linalorejelea aina ya kofia ni neno la Kiarabu linalomaanisha 'heri' na lililopewa jahazi lililojengwa mnamo 1929 huko Lamu na Mhindi kwa jina la utani 'Shiti Leso' kwa kuwa alikuwa na duka la kuuza leso na kanga. Kwa mujibu wa matumizi yake katika uk 115, hii ni aina ya

kofia walizozifaa wana kikundi wa BORA miongoni mwa kofia zingine. Hivyo, hawa ni watu waliokuwa wamemiminiwa heri na fanaka za ushindi katika hatua zao zote za kuomba kura kwa wananchi, baadaye kundi hili lilipata ushindi mkubwa. Neno la Kilatini *Kayfabe* linaashiria kitu cha kuigizwa ama cha uwongo au kitendo cha kuweka siri. Kwa mujibu wa matumizi yake katika uk 121, mwandishi anachimuza ukweli kwamba, wafuasi wa BORA walikuwa na siri nyingi walizotakikana wazihifadhi kama njama ya kumzima U. Ila tu kama inavyodhihirika, siri hizi hazikuwepo kwani badala ya kuungana ili kutimiza siri zao, mtunzi kupitia kwa mbinu ya kiangaza mbele anatudhihirishia kusambaratika kwa kundi hili baadaye. Jambo linalobainika muda mfupi tu baada ya kundi hili kuchukua usukani.

*Parameshwarmera mahanhe*, ambalo ni neno la Kihindi linalomaanisha 'Yesu ndiye Mtukufu' na *duniya Banane wale-thera-jayho* linalomaanisha 'Yesu ndiye Muumba wa mbingu na dunia' yanachimuza imani waliyokuwa nayo wafuasi wa kundi la NUKA na BORA kuhusiana na uwezo alionao Yesu mwana wa Mungu wa kuwapa ushindi kama inavyobainika katika uk 172. *Arbeit Macht Frei* ambalo ni neno la Kijerumani katika mlango mkubwa wa chuma wa kuingia katika kambi ya Wanazi ya Auschwitz, nchini Poland, linamaanisha 'kazi itakufanya kuwa huru'. Kwa hivyo, Wayahudi walioingia kupitia mlango huu walifikiri wangefanya kazi kwa nia ya kuachiliwa huru baadaye na badala yake waliuawa kwa hewa ya sumu, mambo yaliyofanyika chini ya maongozi ya kiimla ya Adolf Hitler. Kulingana na matumizi yake katika *Mafamba*, mwandishi anachimuza ilivyokuwa katika lango la kuingia Mkanyangeni, jumba ambamo watu waliomkosea Maotad walipata kudhulumiwa. Ni jumba lililokuwa na kibao kilichoandikwa 'Arbeit Macht Frei' na kwa njisi hiyo, walioingia hapo walikuwa na matumaini kuwa sheria ingewapata bila hatia na kutoka huko wakiwa huru, ila tu yaliyotendeka yalikuwa kinyume na matarajio yao. Yaliyomfika Mastanji ni mfano mwema wa ukweli huu.

Kutokana na maelezo haya yote ya uchimuzi katika kiwango cha kimsamiati, ni wazi kuwa uandishi katika riwaya za Kiswahili umebadilika kwa kiwango kikubwa hivi kwamba, upya wa utunzi unabainika katika riwaya za kimajaribio au mpya. Katika riwaya hii, kuna matumizi ya misamiati tofauti kwa kiwango kikubwa. Sababu ni kuonyesha ugeni katika riwaya ya Kiswahili unaohusishwa na riwaya hii mpya na aidha kusisitiza usomi wa riwaya unaowezesha wataalamu mbalimbali kubobea kwa huu uandishi kutokana na mitagusano na tamaduni tofauti. Katika riwaya za kimapokeo, matumizi ya misamiati mbalimbali haibainiki kwa kiwango kikubwa kama ilivyo katika riwaya mpya.

### 4.1.2.0 UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA MUUNDO

#### 4.1.2.1 Urudiaji

Hii ni mbinu ya kurudiarudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani. Mwandishi huhusisha michakato ya kimofolojia kwa kurudia neno, sehemu ya neno au shina. Takriri katika kazi ya kifasihi mbali na kuibua athari ya kiujumi, huchimuza maana tofauti. Mathalani kama inavyojitokeza katika uk 38. Mtunzi amerudia maneno ‘zilisita’, ‘zilianza’ na ‘ziliendelea’ ili kusisitiza mlio wa sauti. Aidha katika uk 8, ukatili wa Maotad unachimuzwa kwa namna inayodhihirisha msimamo alioushikilia wa kutong’atuka mamlakani hata ingawa muda wake wa kutawala kulingana na sheria ulikuwa umeyoyoma. Ili kusisitiza jambo hili anasema: “Siendi! Siendi! Siendi.” Pia ni dhahiri kwamba wafuasi wa Maotad walijitayarisha vilivyo kumpa ushauri ili kuonyesha hekima yao ila tu Maotad mwenyewe alitaka kuambiwa jambo kinagaubaga kwani hakuwa na subira. Shanata anapomwambia Maotad kuhusiana na siri alizokuwa nazo kuhusiana na utawala wa NUKA, anarudiarudia neno ‘siri’ ili kusisitiza umuhimu wa ujumbe wake.

> "Nina siri tatu," Shanata alianza. Shanata alianza. "Siri hizi ni za watu wawili. Siri hizi ni za watu wote. Hiyo ndiyo siri ya NUKA. Mwanzoni siri itakuwa ya watu wote...." (17-18).

Hali kadhalika urudiaji wa viwakilishi vya njeo ijayo (ta) na iliyopita (li) vimetumika kama inavyobainika katika mfano ufuatao. Matumizi yake yanaashiria kwamba, wakazi walikuwa na matumaini ya kujitokeza tena kwa mambo mazuri waliyoyashuhudia kitambo hasa kuhusiana na utawala wa hapo awali walioumezea mate wakiulinganisha na wa Maotad ulioandamana na dhuluma za aina yote. Imani yao ilikuwa kuwa kutapatikana tena usawa wa kibinadamu kama walioonja katika sayari ya DUNIA. Kwa mfano:

> "Zipo imani miongoni mwa wakazi wa sayari nyingine kuwa sayari ya DUNIA i*ta*fufuka iwapo i*li*kufa, i*ta*rudi iwapo i*li*enda ziarani, i*ta*amka iwapo i*li*anguka, i*ta*jitegua iwapo i*li*jitega, i*ta*jifichua iwapo i*li*jificha, i*ta*jinasua iwapo i*li*jinasa, i*ta*simama dede iwapo i*li*tambaa. Imani ya wengi i*li*kuwa ni kwamba, kuna siku moja, naam, siku moja tu, siku moja katika kalenda, kalenda tunayoijua sisi, hata kama ni baada ya miaka elfu saba ambapo DUNIA i*ta*onekana tena" (uk 26).

Urudiaji umetumika pia katika nyimbo. Wimbo katika ukurasa 27-28 unathibitisha dhamira ya Amrao ya kukomesha mafamba yaliyokuwa yamezidi katika utawala wa NUKA. Alinuia kutetea haki za wanyonge ili kuinua hali ya mwananchi wa kawaida kinyume na ilivyokuwa ambapo wanyonge walinyanyaswa kwa njia ainati mwaka baada ya mwaka. Wimbo huu unasisitiza mwamko mpya katika harakati za kumpinga Maotad kama ifuatavyo:

> Mimi Amrao nina wajibu
>
> Mimi Amrao nina wajibu
>
> Mimi Amrao nina jibu
>
> Mimi Amrao nina jibu

Wajibu wangu

Wajibu wangu

Wajibu wangu

NI KUKOMESHA MAFAMBA

NI KUKOMESHA MAFAMBA

NI KUKOMESHA MAFAMBA

Ni wazi kwamba Maotad alikuwa na imani kuwa kamwe dalili za kushindwa katika uchaguzi zikibainika angejaribu njia nyingine mbadala aliyoizoea ya kuiba kura ili kujipatia ushindi. Ili kutilia mkazo wazo hili, maneno tofauti yamerudiwa kama vile:

> "Alijua. Alijua vema. Vema sana. Mradi ilikuwa ni karata ya ushindi, alitarajia kuitumia baadaye, hatimaye. Baadaye karata zingine zitakapoisha, ataitoa ile karata ya mwisho-Ile iliyokuwa kifuani. Ile karata ya ushindi. Hiyo karata ya mwisho pia hakuwa na hakika kama itampa ushindi. Hakuwa na hakika. Hakuwa na jingine hata hivyo" (uk 62).

### 4.1.2.2 Urefu wa sentensi

Katika riwaya ya *Mafamba*, mwandishi ametumia sentensi ndefu na fupi kama njia ya kuwasilisha ujumbe wake. Ubainishaji wa uchimuzi katika kiwango cha urefu wa sentensi hutegemea idadi ya marudio ya aina ya sentensi iliyotumika katika matini husika. Kama sentensi ndefu zimetawala fupi, basi inahalisi kwamba zimechimuzwa kuliko zile fupi na hivyo hivyo ikiwa sentensi fupi ndizo zinatawala. Athari ya uchimuzi katika kiwango hiki cha urefu wa sentensi ni kutilia mkazo. Mathalani katika mfano ufuatao, sentensi fupi zimetawala ndefu kuonyesha ukamilifu wa matendo, ni mfano wa dhuluma zilizowaandama watawaliwa:

> "Katika chumba kimoja humo, watu walikuwa ni wengi. Sauti zilisikika. Sauti za juu. Sauti za chini. Kimya. Kelele. Kimya. Kelele. Mayowe. Nduru. Vicheko. Vurumai. Ilikuwa ni kama *periodical market*. Ilikuwa ni mfano wa Onitsha. Vurugu iliendelea. "Mikono ilitupwa juu. Mikono mingine ilitupwa chini. Teke. Moshi. Moshi mweusi. Tena moshi mweusi. Ukungu. Tena ukungu mwingi. Watu wale hawakuonekana vema. Wengi wao walikuwa wanaganzaganza. Walirushiana viti, magayagaya, misala, jamvi wakilaumiana wenyewe kwa kughafilisha kazi na upyororo. Katika sauti hizo, moja ilikuwa ikisikika na kupenya" (uk 136).

Pia katika riwaya ya *Mafamba,* kuna wakati ambapo sentensi ndefu zinatawala fupi kama katika mfano ufuatao:

> "Kulizuka kambi mbili. Kambi moja iliegemea chaguo la Maotad kumchagua jaduon'g ambaye kwa sasa alifahamika kuwa ni U. Naam, U. Huyu U alihitajika kuchukua mahali pa Maotad. U alikuwa amekula asali udogoni, na utamu ulikuwa ungali gegoni" (uk 98).

#### 4.1.2.3 Usambamba

Kwa mujibu wa Jakobson (1966:429), sifa za usambamba ni ruwaza ambapo kuna aina fulani ya mfanano baina ya maneno yaliyofululiza kwa utaratibu ama yanayojitokeza mara kwa mara. Leech (1969:62-63) na Wales (1989:335) wanasema kuwa usambamba ni urudiaji unaofuata ruwaza ya kimuundo hasa katika kirai ama kishazi. Hivyo ni mbinu ambapo mtunzi wa kazi ya kifasihi hurudia maneno au maana fulani kwa kupanga vipashio vya kisintaksia. Huu ni mtindo unaotumika katika riwaya za kimajaribio ili kuendeleza mtindo wa uandishi na usomaji na kuchimuza ujumbe kwa namna inayoufanya utambulike bila tashwishi. Mathalani katika mfano ufuatao, urudiaji wa maneno 'ni kweli', 'alijua' na 'ndoto' yanachimuza ukweli kwamba Maotad alishiriki katika unywaji wa *rumkis malt*, alifahamika katika NUKA, nia ya Amrao na chuki kati

yake na Maotad inabainika na hali kadhalika azma ya Maotad ya kujipendekeza kwa Amrao kwa kumpa nafasi ya Kajo bila kujali inachimuka. Kwa mfano:

> "Ni kweli alishiriki *rumkis malt* na Amrao. Ni kweli Amrao sasa alijulikana katika sayari ya NUKA. Ni kweli Amrao angelishiriki kumnyima Kajo maji yake. Na pia ni kweli kuwa Maotad alimchukia Amrao. Ni kweli kuwa Maotad alikula njama kumzima Amrao. Ni kweli pia kuwa Maotad na Amrao walikuwa ni maadui. Maotad alijua. Amrao alijua na kufahamu. Ni ile ndoto. Ndoto mbaya. Ndoto nzuri... "Lakini tutamwondoa vipi Kajo?" ... "Niachie hayo. Ataondoka tu. Damu haitamwagika. Na ikimwagika, damu mali ya udongo!" Maotad alimhakikishia Amrao... Niachie hayo. Ataondoka tu. Damu haitamwagika. Na ikimwagika, damu mali ya udongo!" (uk 68).

Aidha mbinu hii inajitokeza katika wimbo unaotungwa kwa niaba ya sayari ya NUKA ili kutukuza mafamba kwa kiwango kinachochimuza msimamo wa sayari hii wa kupenda au kuchukia walioelekeza hisia za aina hii kwayo na aidha wa kuabudu mafamba kama ilivyo katika uk 52.

> NUKA ikipenda huna budi kupenda
>
> NUKA ikichukia huna budi kuchukia
>
> Ikiwa hupendi NUKA pia yumkini haitapenda
>
> Mafamba, Mafamba ni hali ya maisha
>
> Maisha ya binadamu
>
> Mafaaaaamba!!

Katika matumizi ya usambamba katika riwaya hii, mwandishi anabainisha umuhimu wa usambamba wa sintaksia hivi kwamba, miundo ya kisintaksia inaelekea kulingana kuzingatia nafsi, virejeleshi na ngeli ya nomino *mtoto* kama inavyojitokeza katika mfano huu:

> "*A*litarajiwa kuwa ni *m*toto *m*changa *a*mbaye... *A*litarajiwa kuwa *m*toto *a*mbaye *u*ngelimwita ... *Ni m*toto *a*mbaye yumkini *u*ngelimwuliza... *Ni m*toto *a*mbaye bado hawezi kuandika herufi O. *Ni m*toto asi*ye*jua tofauti ya moja na sifuri" (uk 91).

Hali kadhalika, matumizi ya usambamba katika riwaya hii yanadhihirika pale ambapo neno moja linarudiwarudiwa ili kuchimuza ujumbe kama ilivyo hapa:

"Toboa! Toboa! Toboa!"... uk 248

"Debe! debe! debe!" uk 249

...Damu! Damu! Damu!" uk246

..., "Okoa jahazi! okoa jahazi!" uk 249

#### 4.1.2.4 Maswali ya balagha

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:27), hii ni mbinu ya uwasilishaji wa usemi kwa njia ya kushawishi na kuathiri msikilizaji. Msemaji huuliza maswali ambayo hayahitaji kujibiwa kwani majibu huwa dhahiri kwa msikilizaji. Holman (1976:452) anasema kuwa, mbinu hii hulenga kumshawishi msikilizaji kwa kumpa changamoto ya kuyapata majibu ili awe mshirika wa mchakato wa mawasiliano wala sio kuwa msikilizaji tuli. Kwa hivyo, msikilizaji hupata hamasa ya kuyachangamkia anayoambiwa na kuwa makini kwa kuwa ni mambo yanayojitokeza kwa uwazi.

Maswali ya balagha katika *Mafamba* yametumiwa kuonyesha athari ya kishairi na kusisitiza ujumbe. Katika mfano ufuatao, mwandishi anachimuza utekelezwaji wa ufisadi katika sayari ya NUKA. Maotad anapowaita Kamu, Kanga, U na Avadi ili awaambie siri kuhusiana na urithi wa kinara wa NUKA, Shanata, Kajo na Nikiabi wanashindwa kuelewa sababu za watu hawa kutoka kwa Moatad wakiwa na tabasamu kiasi cha kuona magego yao ya ndani. Wanaanza kufikiria na kutoa nadharia kuhusiana na furaha hii yao. Kulingana na maswali wanayojiuliza, ni wazi kwamba kilichofurahisha nafsi zao hasa katika sayari hii ni zawadi nononono zilizotolewa na Maotad kama vile mashamba, misitu, ukubalifu wa kutoa na kupokea mlungula miongoni mwa zingine. Pia ujanja wa Maotad unajitokeza, yeye ni kiongozi aliyeweza kuchezea akili za watu ili kuwaleta karibu naye kwa lengo la kuwafurahisha na kuwafanya wamuunge mkono daima. Angewaahidi makuu ambayo hangeyatimiza kutokana na ubinafsi wake na tamaa. Kwa mfano:

> "Ni tabasamu ambazo Shanata na Nikiabi hawakuwa wameziona kwa watu hao. Walianza kutoa nadharia zao. Labda ni mafamba. Walipewa zawadi gani? Mashamba? Kandarasi, kazi ya malatifu wao? Mlungula? Misitu? Mito? Vyoo vya wakazi wa Bikerani-Msiige? Barabara? Viwanja vya shule? Kununua kampuni ya mfuko ya C-K-C? Kampuni ya akaunti mpya katika sayari za mbali? Briefcase za manoti? Uanachama katika kampuni ya mfuko wa vito? Kupewa nafasi ya kukutana na mwenyekiti wa kampuni ya mfuko wa vito Bwana Paka? Au labda kuahidiwa kupewa nafasi kama kinara mpya wa NUKA? Nadharia hizi ziliendelea kuwazonga akili" (uk 76).

Vitisho vya Maotad dhidi ya Avadi vinachimuzwa pia kupitia mbinu hii. Maotad aliwadhulumu watu kwa njia kadhaa na alitaka kuonyesha kwamba, hakuna aliyemwonyesha mgongo ambaye alifikwa na mazuri. Bwana Kachuoheze na Amrao ni baadhi ya waliojipata matatani baada ya kujaribu kuhusika katika utekelezaji wa nyendo tofauti kinyume na matakwa yake. Anamtisha

Avadi kwa kuasi NUKA kwa sababu anataka daima akae katika sayari ya NUKA anapofanikiwa kupata mafamba na vitu vizuri vya ufisadi. Kupitia kwa maswali ya balagha anayomuuliza baada ya kumteka na kumshurutisha asalimu amri, ni dhahiri kuwa Avadi hangefaulu kwani Maotad angemwekea vikwazo maishani na kumzuia kusonga mbele ili kutimiza ndoto zake. Hii ni tabia mojawapo ya viongozi ya kuwadhulumu wenzao ambao huamua kuzingatia mielekeo ifaayo. Wanapotambua kuwa wametorokwa na baadhi ya wafuasi wao wa karibu wajuao siri zao, huwalazimisha kuwa wafuasi wao tena kwa masharti kwamba wakikosa watakumbana na kifo. Jambo linalomotishwa na hofu yao ya kupatikana kwa mashahidi wa kusema ukweli unaohusu tabia zao katili. Kwa mfano:

> "Unafikiri Amrao atafaulu? Amefeli mara ngapi?"
>
> "Alipojaribu yeye na Bwana Kachuoheze, alifaulu?...
>
> "Wewe umeshiriki mafamba. Leo unasema hapana? (uk 153…)
>
> "Unamwita mafamba shetani ati. Hukushiriki chichiri?"
>
> "Huna chochote ulichonacho bila mafamba. Chichiri ni dhambi?"….
>
> "Mbona sijakuua?"
>
> "Mbona sijakuua?"… "Sikuhesabu mpaka saba?" (uk 154)

Mzee Twajua, mwanakijiji wa Tuga Amor anapowahamasisha wakazi hawa kuhusiana na kushikilia msimamo thabiti wanapowachagua viongozi na wala sio kufanya uamuzi mbaya wa kuwafanya waendelee kuteseka baada ya kupiga kura, anawauliza maswali ambayo hayakuhitaji majibu. Maswali haya yanaonyesha kwamba, hata baada ya utawala wa BORA kuchukua usukani, mafamba hayakuweza kuzikwa bali yaliendelea kunawiri licha ya matumaini yao kuwa

BORA ingeleta mabadiliko katika nyanja mbalimbali. Kwa mintarafu hii, kupitia kwa maswali haya, dhamira mojawapo ya mwandishi inachimuza. Hali inayozikumba jamii za barani Afrika ni tabia ya viongozi ya kuendeleza aina yote ya maovu mbali na kuonyesha misimano thabiti na ukakamavu katika uongozi kabla ya kuchaguliwa. Wanapochaguliwa, muda mfupi hauishi kabla hawajabadilika na kuwa kama watawala wabaya wa awali kwa kufuata nyayo zao. Mbinu hii inakoleza pia hasira za mwandishi kuhusiana na mambo haya yanayotekelezwa na viongozi bila kujali woga na hasira zitakazokumba hadhira kwa kuwakumbusha matukio wanayoyajua. Kwa mfano:

> "Shetani mafamba. Aliuliwa? Kuja kwa BORA kulimuua mafamba? Kulimuua shetani? Kuliuua ufisadi? Kuliuua ulanguzi? Ni nini haswa maana ya mafamba? Ni nini haswa maana ya shetani? Mafamba amezikwa au amefufuka? Mafamba ni kiumbe ama si kiumbe? Mbona anarejelewa kama kitu kilicho na uhai na mara nyingine kama kitu kisicho na uhai? Kuna kitu kilicho na uhai na wakati huo huo hakina uhai?" (uk 190).

Ufafanuzi huu wa uchimuzi katika kiwango cha muundo unabainisha kuwa, upya katika riwaya ya kimajaribio hutokea pia katika kiwango cha kimuundo. Licha ya kuwa muundo katika riwaya za kimajaribio huonyesha uhuru wa kiujumi, kwa kiwango kikubwa, muundo huu huonyesha ukweli kwa wasomaji kuhusiana na jinsi viongozi wanavyovunja thamani ya uzalendo kwa watawaliwa. Kwa hivyo, matumizi ya mbinu kama urudiaji, usambamba na urefu wa sentensi katika riwaya hizi ni kusisitiza ukweli wa balaa inayopatikana barani Afrika kutokana na utaratibu wa uongozi. Kwa sababu hii, waandishi wa riwaya hizi huvunja kaida za uandishi zinazohusishwa na riwaya za kimapokeo kwa kuelezea umma mambo yanayosibu mataifa kama ya kidini, utandawazi na ya kisiasa.

## 4.2.0 UCHIMUZI KATIKA KIWANGO CHA KISEMANTIKI

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004:201), semantiki ni utanzu wa isimu unaochunguza maana katika lugha ya mwanadamu na hushughulikiwa katika viwango vyote vya lugha, kama vile sauti, maneno na sentensi. Richards na wengine (1985) wanairejelea istilahi hii kuwa 'stadi ya maana.' Kwa hivyo, umuhimu mkuu wa lugha ni kufaulisha uwasilishaji wa maana ambapo ujumbe hubainika kutokana na maana yake na aidha kufuatilia ufafanuzi wa maana zilizobebwa na vipashio vya lugha vinavyohusika. Katika kiwango hiki basi, tutaangalia mbinu ambazo zinachangia uchimuzi wa uwasilishaji wa maana katika riwaya ya *Mafamba*.

### 4.2.1 Uhaishaji

Hii ni mbinu inayotumiwa kuelezea vitu visivyokuwa na uhai ama vya kidhahania kama ambavyo vina uwezo wa kibinadamu. Uhaishaji umetumika katika riwaya hii kuhusisha vitu ambavyo kwa kawaida havifai kuhusishwa. Sababu mojawapo ya kufanya hivi ni nia ya mwandishi ya kuonyesha kuwa binadamu kwa kiasi kikubwa katika jamii ya kisasa anaongozwa na sheria fulani na anategemea vifaa fulani maishani mwake. Kupitia kwa mbinu hii, ujumbe fulani unasisitizwa na kuchimuza kama ilivyo katika uk 60-61. Katika mfano huu, mwandishi anaupa ukurasa nguvu za kuongea ambazo kwa kawaida hubainika kwa wanadamu pekee. Kutokana na matumizi haya, mwandishi anachimuza jambo kwamba sheria za NUKA kama zilivyodhihirika katika maandishi ya katiba ya nchi, zilibainisha wazi kuwa muda wa Maotad wa kuendelea kuongoza ulikuwa umekwisha na kwa hivyo kamwe hakutakikana kuendelea kuwa kinara wa sayari yoyote ile hata NUKA. Kwa kuwa hata wakazi wa Bikerani-Msiige walielewa bayana ukweli huu, walimtaka Maotad aheshimu sheria hizi kama zilivyojitokeza katika ukurasa au karatasi mahususi ya sheria za NUKA. Kwa mfano:

> "Ukurasa ulitoa sauti...... Sauti iliipa ukurasa uhai. Ukurasa alisema: Maotad, ni lazima akiache kile kiti. Muda wako wa kukikalia umekwisha... Ukiendelea kukikalia, utakuwa unavunja sheria hii unayoisoma hivi sasa. Sasa ukurasa alianza kuzungumza na nafasi yake na kumtetemesha. Ukurasa aliendelea: ... uk 60. Ukurasa alimaliza kutoa kauli yake. Maotad alimaliza kumsikiliza. Waliagana. Ukurasa aliendа zake uk 61..... Wakazi ambao walimtaka Maotad kumheshimu karatasi ama labda ukurasa" (uk 70).

Katika dondoo linalofuata, mwandishi anachimuza umaarufu uliopewa sayari mpya ya BORA iliyokuwa imeanza kujishikashika na kupata wafuasi kutoka sehemu kadha za Bikerani-Msiige. Imani ya wakazi hawa ilikuwa kwamba, sayari hii tofauti na ya NUKA ingewawezesha kupata ukombozi walioutamani na kuumezea mate baada ya madhila kuwaandama kwa takribani miaka 40. Sayari ya BORA ilitarajiwa kuzalisha matunda ainati ya ukombozi yaliyotawala ndoto za wakazi hawa kila siku. Matumaini yao yalikuwa kwamba, viongozi wa sayari hii kama vile LiMioe, Boyi, Amrao, Fadhila miongoni mwa wengine wangeimarisha vuguvugu katika sayari ya NUKA na kuzindua sauti za wanyonge na hali kadhalika kufikisha mwisho mateso yaliyowaathiri kwa njia moja au nyingine kama kukaliwa, kutukanwa, kunyanyaswa, kunyonywa, kudhulumiwa, kunajisiwa na kunyang'anywa mali yao bila sababu. Mfano:

> "Majina mengi yalipendekezwa. Mwishowe jina BORA lilishika. BORA akawa ni kama safina. BORA akawa ni mkombozi wa wale waliokaliwa, waliotukanwa, waliokanyagwa, walionyonywa, waliodhulumiwa, walionajisiwa, waliokamuliwa na Maotad pamoja na utawala wa NUKA" (uk 101).

Aidha katika mfano unaofuata, mwandishi amevihusisha vitu tofauti ili kuchimuza kwa uwazi mambo kadha wa kadha. Kwa mintarafu hii, vifaa vya kiteknolojia vimehusishwa kuonyesha jinsi binadamu katika jamii hii ya kisasa kwa kiasi kikubwa hawawezi kuishi bila kuvitegemea

na kwa kufanya hivi ujumbe unatiliwa mkazo. Kwanza, gari linasemekana kutafuna mchanga, sifa hii ya 'kutafuna' inahusishwa na viumbe wenye uhai. Kwa kulitumia, mwandishi anaonyesha mwendo wa kasi ambao gari la askari wa Maotad lilikuwa limeendeshwa nao ili kumfikisha Avadi alikotakiwa kwa dharura. Yaani, katika sebule kuu ya Maotad mkabala wa mtaa wa Bikerani-Msiige ili kujibu mashtaka ya kuasi NUKA. Huu ni wakati ambapo Avadi baada ya kutoka mkutanoni na akina Amrao alitekwa na kuongozwa kuingia kwa hili gari ili kupelekwa asikokujua (uk 147). Mtunzi anachimuza jinsi sehemu ya barabara ya kuelekea kwa Maotad ilivyokuwa mbaya hivi kwamba ilifanya gari hili 'kukohoa kwa dhiki'. Kwa namna hii, Maotad ni mfano wa kiongozi ambaye kamwe hakujishughulisha na maendeleo ya jamii kama kuimarisha miradi ya kukarabati barabara.

> Gari *lilitafuna* mchanga sawasawa na kuacha nyuma biwi la ghubari na hatimaye *kuzinyanyasa* kona saba hivi kabla ya kuchukua barabara iliyonyooka......Palikuwa na mashimo mengi tena makubwa kataka sehemu hiyo jambo ambalo lilifanya gari lile *kukohoa kwa dhiki* (uk 148). ....., derava alipinda na *kuitafuna* barabara nyingine tofauti na iliyokuwa nyembamba (uk 149).

Viongozi wengi wanafanana kihulka na Maotad kwani baada ya kuchaguliwa, wao hulaza damu katika kutekeleza maendeleo ambayo hunuiwa kusaidia jamii kwa jumla. Wao huyajali matumbo yao, kuwekeza pesa kwa manufaa yao wenyewe katika benki za nchi za nje na kulimbikiza mali. Hivyo, mwandishi anatuchorea taswira halisi ya makao rasmi ya Maotad penye nyumba kubwa iliyozungukwa na taa za rangirangi 'zilizochoka' kumngoja mgeni aliyetarajiwa. Ingawa kulikuwa usiku, picha inayojengeka akilini mwetu inaashiria kwamba kulikuwa kunang'aa kama mchana. Hali kadhalika, mtunzi anachimuza ukweli kuwa polisi wa Maotad hawakuwa watu hivi hivi, walikuwa na mafunzo kabambe kulingana na utaratibu unaojitokeza kupitia kwa matumizi ya mbinu hii. Wanapotoka ndani ya gari, viatu vyao vinatanguliza na vinakanyaga chini kwa

nguvu, ni wazi kwamba viatu havina uwezo wa kutembea wala haviwezi kukanyaga chini kwa nguvu kama havijavaliwa. Ufuatao ni mfano:

> Nyumba kubwa ilionekana kwa umbali na taa za rangirangi *zilisinziasinzia* kana kwamba *zilichoka* kungoja mgeni huyu aliyekuwa mita chache kuzifikia.....Nguzo za taa za umeme zilifukuzia hapa na pale. Ziliashiria kuwasili kwa mgeni maaalum (uk149). Walianza na kutoka ndani ya gari. Viatu vyao *vilitangulia. Vilikanyaga* chini kwa nguvu (uk 150).

Dondoo linalofuata linaonyesha pia matumizi ya mbinu hii ya uhusishaji katika kuchimuza sifa bainifu za mafamba. Hili ni neno linalowakilisha anwani ya riwaya hii na kwa namna hii, uozo wa kimaadili wa viongozi katika jamii yetu na barani Afrika unamulikwa na kujitokeza kwa uzito zaidi. Istilahi hii kwa mujibu wa TUKI (1981:148) ni mambo yasiyokuwa ya uadilifu; hila au udanganyifu. Ufafanuzi huu unaafiki jinsi mafamba yanavyorejelewa katika kifungu hiki cha maneno ambapo mafamba yanahusishwa na mambo tofauti ili kuonyesha manufaa waliyoyapata wale walioyaabudu. Kwa kuwa mafamba yalikuwa na uwezo wa 'kufa na kufufuka', kufa kwa maana ya kukoma kutekeleza nyendo chafu kwa viongozi na kufufuka kwa maana ya kuziendeleza nyendo hizi daima, hivyo basi waliotaka kuyaendeleza kama wanasayari wa NUKA waliweza kutekeleza nyendo zote mbaya zilizofurahisha nafsi zao. Kwa sababu hii, mafamba yalitumiwa kusababisha vifo kwa wale waliojaribu kufichua mienendo potovu ya viongozi katika NUKA, haki za wanyonge zilinyonywa kupitia kwa mafamba kama kubadilisha kesi kwa niaba ya waliopendelewa zaidi na kwa njia hii kubadilisha uongozi katika mataifa ya Afrika kama ilivyokuwa katika jamii yetu enzi za utawala wa Maotad na aidha ilivyojitokeza katika utawala wa BORA hadi sasa. Dondoo hili linabainisha haya:

> "Mafamba ilihusiswa na shetani. Mafamba ilikuwa kama mwanadamu ila hakufa. Alizaliwa, alikula, alikunywa, alilala, alicheka, aliugua, alicheza, aliimba, alihuzunika, alikimbia lakini

hakufa... Alisababisha vifo. Alikuwa mjumbe wa kifo (uk 164). Mafamba likuwa ni shetani ambaye alikuwa na uwezo wa kufa na kufufuka... Mafamba alikuwa ni shetani ambaye alichukiwa na kuabudiwa. Waliomchukia walimwabudu na waliomwabudu walimchukia. Mafamba alifurahi njinsi alivyozifurahisha nafsi za watu... Alikuwa ni mwanadamu na mshirika wa kila upande... Leo mafamba alicheka. Kesho angelikunyemelea na kukunyonya. Leo angelikukumbatia na kesho akupige kabari... Ambacho hawakufahamu ni kuwa mafamba aliweza kuzikwa lakini pumzi yake haikuweza kukatika. Alivuta pumzi tu... Mafamba alikuwa ni *senior citizen* wa NUKA. Alipewa makao rasmi na personal assistant... Mafamba alikuwa anaheshimika hata na maskini, (uk 175-6). Mafamba ilibatilisha 'ndiyo' kuwa 'hapana' na 'hapana' kuwa 'ndiyo'. Mafamba iliwanyima wanyonge haki zao, (uk 181). Mafamba ni shetani mwovu...Mafamba ni tomondo ambaye lazima atolewe kutoka majini...Mafamba ni ibilisi ambaye ameangamiza mataifa mengi ya Karifa, (uk 240). Mafamba ni kama mtoto. Anazaliwa, anakaa, anatambaa, anasimama dede, anakamatia kuta za nyumba, na hatimaye anakwenda tata mpaka anapoweza kwenda kwa miguu yake bila usaidizi wowote" (uk 241).

Hali kadhalika, matumizi ya mbinu ya uhusishaji yalimwezesha mwandishi kuchora taswira halisi ya ajali iliyomkumba LiMioe katika makutano ya barabara ya kutoka Nzambani kuelekea Kar Pir Mang'ich. Kwa njia hii, mtunzi anachimuza ajali hii mbaya iliyokaribia kumfikisha jongomeo LiMioe wakati ambapo alihitajika sana katika historia ya jamii yetu ili kubadilisha hali ilivyokuwa. Kulingana na maelezo, kila mmoja anayeisoma sehemu hii anaathirika kihisia kwa kuwahurumia waliokuwa ndani. Katika ajali hii, gari liliota mbawa, magurudumu yake yakaibusu barabara kama ifanyavyo ndege ikipaa angani na hatimaye gari likaruka juu. Kweli kunusurika kwa waliokuwemo ndani ni kutokana na kudura za Mungu, na kwa namna hii mwandishi anachimuza jinsi LiMioe alivyoumia anaposema kwamba 'Yeye na maumivu walikuwa marafiki wa chanda na pete', yaani aliumia sana. Anasema:

"Gari la LiMioe likala, likatafuna na kuimeza sawasawa barabara kutoka Nzambani hadi kufikia makutano ya barabara ielekeayo Kar Pi Mang'ich- bila dereva kuushika usukani (uk 169)... Mosi, mbili, tatu, nne, tano, sita...na mara moja, gari liliota, mbawa. Magurudumu yake yakaanza kuibusu barabara kama ambavyo ndege inavyoiacha ardhi ikipaa angani. Na mara, magurudumu yale yalisalimiana na barabara mara ya mwisho. Yaliagana na barabara kabisa. Yalipoacha tu barabara, magurudumu yalibadilika yakawa matendegu! Gari liliruka, juu, juu juu kama tiara na kisha lilirudi chini mbio likifululiza moja kwa moja hadi gofu lililoachwa na mwenyewe baada ya kunyang'anywa shamba na utawala wa Maotad (uk 170)... LiMioe hakuweza kutoka pale kitandani alikolazwa hospitalini. Yeye na maumivu walikuwa marafiki wa chanda na pete. Alimtembelea maumivu na maumivu akamjulia yeye LiMioe hali" (uk171).

Ingawa matumizi ya mbinu hii ya uhusishaji yanadhihirika pia katika riwaya za kimapokeo, matumizi yake katika riwaya mpya ni ya kiwango kikubwa ili kuhusisha kwa makusudi mambo ambayo hayafai kuhusishwa. Lengo kuu la kufanya hivi ni kusisitiza masuala haya ambayo kwa hali halisi yanahusu jamii zetu kwa kuyawasilisha kwa njia inayoyafanya mapya kulingana na namna tunavyoyafahamu.

### 4.2.2 Uhalisiaajabu

Katika riwaya hii, mbinu hii imetumika kwa kiwango kikubwa. Ni mbinu inayojitokeza sana katika riwaya za kimajaribio kama hii ili kuchimuza ukweli halisi kwa wasomaji. Kulingana na Wamitila (2003:274), sifa hii ni ya kuyaeleza matukio ya kifantasia, ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Anasisitiza kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana. Baadhi ya mifano ya matumizi ya mbinu hii ni kama ifuatavyo:

"Gari la LiMioe likala, likatafuna na kuimeza sawasawa barabara kutoka Nzambani hadi kufikia makutano ya barabara ielekeayo Kar Pi Mang'ich- bila dereva kuushika usukani (uk 169)... Mosi, mbili, tatu, nne, tano, sita...na mara moja, gari liliota, mbawa. Magurudumu yake yakaanza kuibusu barabara kama ambavyo ndege inavyoiacha ardhi ikipaa angani. Na mara, magurudumu yale yalisalimiana na barabara mara ya mwisho. Yaliagana na barabara kabisa. Yalipoacha tu barabara, magurudumu yalibadilika yakawa matendegu! Gari liliruka, juu, juu juu kama tiara na kisha lilirudi chini mbio likifululiza moja kwa moja hadi gofu lililoachwa na mwenyewe baada ya kunyang'anywa shamba na utawala wa Maotad (uk 170)... LiMioe hakuweza kutoka pale kitandani alikolazwa hospitalini. Yeye na maumivu walikuwa marafiki wa chanda na pete. Alimtembelea maumivu na maumivu akamjulia yeye LiMioe hali" (uk171).

Ingawa matumizi ya mbinu hii ya uhusishaji yanadhihirika pia katika riwaya za kimapokeo, matumizi yake katika riwaya mpya ni ya kiwango kikubwa ili kuhusisha kwa makusudi mambo ambayo hayafai kuhusishwa. Lengo kuu la kufanya hivi ni kusisitiza masuala haya ambayo kwa hali halisi yanahusu jamii zetu kwa kuyawasilisha kwa njia inayoyafanya mapya kulingana na namna tunavyoyafahamu.

### 4.2.2 Uhalisiaajabu

Katika riwaya hii, mbinu hii imetumika kwa kiwango kikubwa. Ni mbinu inayojitokeza sana katika riwaya za kimajaribio kama hii ili kuchimuza ukweli halisi kwa wasomaji. Kulingana na Wamitila (2003:274), sifa hii ni ya kuyaeleza matukio ya kifantasia, ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Anasisitiza kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana. Baadhi ya mifano ya matumizi ya mbinu hii ni kama ifuatavyo:

### 4.2.2.1 Kifungua kinywa cha kundi la BORA

Wakati wa mikutano ya kundi la BORA, kifungua kinywa kinaitishwa hasa wanapopanga mikakati ya kuleta upatanisho. Katika harakati hii, wanaitisha vyakula vinavyopatikana Haponaseremwige na ambavyo ni tofauti. Fadhila anaitisha sasamlanda, kahawa, sambusa iliyotiwa nyigu na nyama ya kalakanje. Boyi naye anaitisha Pombo, ngisi, kahawa, shinarupia, zelabia, sambusa iliyotiwa nyama ya loma na nga'ndu. Naye LiMioe anaitisha manda, ngogo, na zamburu wa kukaanga, nyama ya nguva na mapafu ya kulasitara (uk 103-104). Amrao naye anaagiza mijusi ya aina mbalimbali kama kengewa kupikwa, guruguru wa kukaushwa, mjombakaka wa kuchomwa na nanigwanzula wa kukaangwa, naye Saigeo anaagiza nyama ya mnimbi iliyorashiwa pilipili manga, kumbikumbi wa kukaangwa kwa mafuta ya kasuku na kuku wa mangisi aliyekaukia (uk 110). Ladha zao zilikuwa tofauti hivi kwamba kama ni nyama ya ndege ilikuwa tofauti, kama ni samaki alikuwa tofauti na kama ni mboga ilikuwa tofauti na wala hakuna aliyeuliza mwenziwe sababu ya kukipenda chakula fulani. Hata hivyo, waliitisha kinywaji kimoja cha nungumaria kilichopendwa na wote. Kwa mujibu wa maelezo haya ni wazi kwamba, ingawa wanasiasa hawa walikuwa na malengo na matumaini tofauti ya kisiasa yanayoashiriwa na chakula tofauti walichokila, walishirikiana kwa pamoja ili kuyatimiza malengo hayo, na hii ndio sababu wanakunywa kinywaji kimoja cha nungumaria.

Licha ya kuwa mbinu hii inadhihirika katika riwaya za kimapokeo kama *Kusadikika* (1951) ya Shaaban Robert, matumizi yake katika riwaya mpya yanatokea kwa kiwango kikubwa katika vipengele tofauti kama uhusika, mandhari na matukio. Umuhimu wa matumizi haya ni kuelezea ukweli bila kutumia njia ya moja kwa moja, kuonyesha taathira za kiteknolojia au kitamaduni katika jamii zetu na aidha kuonyesha kuporomoka kwa takriban kila kitu katika jamii kitamaduni, kiuhusiano, kiuchumi na kadhalika.

#### 4.2.2.2 Utabibu

Mwandishi anatumia dhana hii ya utabibu, yaani jinsi wanahewa walivyojaribu kumwangamiza Maotad ili kuwasilisha ukweli huu. Anaelezea kuhusu Biandi, makao makuu ya madaktari waliokubuhu na wenye mabawa. Hawa ni madaktari waliojaribu mara kadha kumfanyia Maotad upasuaji ili kuutoa ufunguo aliokuwa ameumeza kwa miaka 40 lakini walishindwa. Walimpenda sana na kwa sababu hiyo hawakutaka ufunguo huo umdhuru. Ingawa walimpenda, tunaelezwa kuwa, siku hiyo waliimba Maotad *sumt dan liwl og!,* wimbo wa kumfukuza mamlakani. Waliwazuru madaktari wenzao kutafuta sindano na prokeni lakini baadaye wakasema angetibiwa na maji tu yaliyotolewa na madaktari wa Bae baada ya mabishano kuwa prokeni haingeweza kumtibu. Bae ilikuwa hospitali kubwa iliyokuwa na madaktari wenye mabawa waliokuwa kilomita tatu kutoka Biandi ambapo kulikuwa na daktari mkubwa, bwana Kachuoheze ambaye alitambulika kwa pupa yake ya kutafuta maji ya kumtibu Maotad kwa kutoa ufunguo uliokuwa tumboni mwake lakini hakufaulu. Tunajuzwa kuwa Maotad alimtibu Kachuoheze pamoja na madaktari wa Biandi na Bae na wakatibika milele bila kupatwa na ugonjwa tena. Aliwapa adhabu kali. Hivyo, Maotad alisaidiwa na kuwategemea madaktari wengine ambao hawakuwa na mabawa lakini waliokuwa na hekima nyingi ya utabibu. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa Maotad alikuwa amechukiwa na wengi na hivyo wanahewa pia walijaribu kumwangamiza ingawa hawakufaulu. Anapogundua njama zao, anawafuta kazi na kubadilisha njia zake za usafiri (uk 80-81).

#### 4.2.2.3 Lugha zilizotumika katika sayari mbalimbali

Tunaelezwa kuwa kila sayari ilikuwa na muundo wa lugha yake. Katika sayari hizi, baadhi ya konsonanti na vokali za lugha zilichukiwa mno na viongozi na wanasayari. Herufi nyingine

ziliaminiwa kumwalika ziraili nyakati za magharibi nazo nyingine zilisababisha ufukara wa milele. Baadhi ya herufi zilihitaji kutangulia nyingine na pia kufuata nyingine, pia herufi nyingine hazikupaswa kufuatana kwa muundo wa konsonanti na vokali na kwa sababu hii baadhi ya lugha zilifuata muundo wa KVK na nyingine KVKV kama ilivyokuwa katika NUKA. Kwa mfano sayari ya NUKA ilichukia herufi 'I' kwa kuwa ilikuwa mwiko kufuata herufi 'M'. Kwa mujibu wao, kufuatana huku kungesababisha umaskini kwa vile ilitajwa kuwa herufi kigeugeu. Walitumia herufi 'A' kuifuata herufi 'M'. Herufi 'B' pia ilisemekana kusababisha umaskini ikitokea kabla ya herufi 'M'. Aidha, herufi F ikiwa kati ya herufi A na R ingesababisha umaskini hivyo ilijitokeza kati ya A na A ili kutupilia umaskini mbali. Herufi A ilipendeza watu wa sayari ya NUKA kwa kuwa ilitumika sana kumalizia maneno mengi na kwa hivyo maneno mengi katika sayari hii yalianza kwa herufi M na kumalizia kwa A (uk 31-32). Kwa mujibu wa ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa sayari ya NUKA ilipendelea sana kutekeleza maovu na hii ndiyo sababu mazungumzo yao yalihusisha masuala ya mafamba.

### 4.2.3 Taswira

Ni matumizi ya lugha kwa namna inayojenga picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji. Ullmann (1964:177) anairejelea dhana hii kuwa tamathali ya usemi inayoelezea kitu kinachofanana na kingine. Ullmann (k.h.j:178) anasema kuwa kuna njia kadha za kutofautisha taswira na tamathali zingine zinazoonyesha mfanano wa kitu au jambo. Kwake, taswira haiwezi kubainika pasipo na mfanano dhahiri na sifa inayotambulika na kuwa lazima taswira hiyo idokeze kitu kinachovuta nadhari kwa uzito na kisichotarajiwa kwa njia yoyote. Pia, kitu hicho chafaa kidhihirishe athari ya mshangao kutokana na utambuzi wa elementi mbili za tajriba zilizo tofauti.

Katika ukurasa wa kwanza, mwandishi anatuchorea taswira halisi ya mtaa wa Bikerani-Msiige na kasri la kifahari ambalo liko mkabala wa mtaa huu. Bikerani-Msiige ni mahali palipoishi watu maskini walioishi katika nyumba za madongoporomoka zenye milango ya mabati huku milango ya vioo ikiwa ni magunia ya sukari. Hii ni taswira iliyokuwa kinyume na sehemu iliyokuwa mkabala wake ambapo kuliishi wakwasi kwelikweli kwenye kasri la kifahari lenye dari iliyotiwa nakshi kwa mpingo na yenye mataa maridadi ya thurea na sakafu iliyotengenezwa na jiwe la marmar na hali kadhalika palipokuwa na mandhari mazuri yenye kivuli kutokana na miti anuwai. Taswira hii inatudhihirishia namna wenye mali wanavyojitenga na maskini mbali na kuwa karibu nao. Hawa ni viongozi ambao jukumu lao ni kuanzisha miradi ya kuwainua kimaisha kwa kujenga nafasi za kazi lakini badala ya kufanya hivi wanawatazama tu wakiteseka na kulala njaa. Mwandishi ametumia mbinu hii kuonyesha mwanya wa kitabaka katika jamii unaosababishwa na ufisadi wa wanaohusika, ulaghai na jinsi viongozi wanavyolimbikiza mali bila kuyajali maslahi ya wananchi.

Hali kadhalika, mwandishi katika uk 19 anatuchorea taswira halisi ya kiti rasmi cha wageni waliomtembelea Maotad katika sebule kuu. Ni kiti kilichojulikana kunguni wake na wengi hata ingawa wengine hawakufahamu kabisa, baadhi ya waliofahamu kilichosheheni waliomba ruhusa kuongea wakiwa wamesimama na ila wengine hawakuonyesha wasiwasi wowote. Hiki ni kiti alichowakaribisha wageni wake na wale walipata kukikalia baada ya kumchokoza walipata cha mtema kuni. Ni kiti kilichokuwa na swichi nyuma yake na chenye nyaya nne zilizofululiza kutoka kiti hicho kuungana na kitundu cha kawi kilichokuwa ukutani. Kiti hiki kilikuwa na nyaya nne ambapo mbili zilifikia sehemu ya kupumzisha mikono yote miwili nazo zingine mbili zilifululiza kutoka ukutani hadi kando ya kichuma kifupi cha kustarehesha miguu. Juu ya kiti hicho sehemu ya kulegezea kichwa ilikuwa na kifaa kama bakuli ambacho mwenye kukikalia

kiti hicho alivikwa kama taji kama ambavyo toto shoo huvikwa akiwa saluni wakati nywele zake zinakaangwa. Hii ni taswira inayochimuza uozo wa kimaadili wa Maotad licha ya kuwa kiongozi aliyepaswa kuwa mfano mwema kwa wote. Hii ilikuwa njia mojawapo ya kuwazima mahasidi wake.

Hali kadhalika, mtunzi amechora taswira ya ilivyokuwa siku ya mwisho ya mkutano wa kundi la BORA. Kwa mujibu wa maelezo yake katika uk 176, uwanja ulikuwa umejaa sana hivi kwamba sindano haingeweza kupata nafasi ya kisimama wima wala mtu aliyekuwa na sifa teule ya kulenga shabaha duniani hangeweza kutumia manati akamkosa mtu pale, uwanja ulikuwa umefurika furifuri. Anaeleza kuwa huu ni mkutano uliotembelewa na sampuli yote ya viumbe wenye uhai kama wadudu, wanyama na ndege. Vichwa vya waliohudhuria vilionekana kwa mbali kama sisimizi weupe waliobeba chichi, wengi wakiwa wamekaa chini, wengine juu ya mabodi ya magari na wengine kwenye miti kama kwamba kila mtu alikuwa pale. Wakiwa wamesubiri walioandaliwa kwa siku hiyo muhimu katika historia ya jamii yetu, LiMioe aliletwa pale uwanjani kwa machela, akiwa amevikwa nguo ya bandeji iliyomsetiri kote mwilini. Jicho lake moja alilielekeza umati na moja alilifunga na kulifungua kwa wepesi wa marisau huku akilifunga na kulifungua. Kama anavyosema mtunzi, aliendelea kukopesakopesa macho yake kana kwamba alikuwa *genetically linked to Tippu Tippu*. Nalo kundi la wanamuziki wa GIMA lilitumbuiza umati kwa kibao chao SISI IMARA. Kutokana na maelezo haya, ubora wa kundi la BORA unachimuka na imani yao kwa LiMioe hata baada ya kuhusika na ajali mbaya iliyopelekea alazwe hospitalini na kumtenga na kampeni za kundi hili aliloliongoza kama kinara mkuu na aliyetarajiwa kusambaratisha nyendo chafu za NUKA.

Taswira katika riwaya mpya zinatumika kuonyesha hali halisi ya mambo kama yanavyotendeka katika taifa au mataifa tofauti na riwaya za kimapokeo zinazoelezea hali halisi ya maisha ya

binadamu. Kwa namna hii, dalili za ukuaji wa lugha ya Kiswahili zinabainika kwa kutumia mbinu hii kusisitiza uozo wa kimaadili wa viongozi, tofauti za kitabaka kati ya walionavyo na wasionavyo miongoni mwa masuala mengine yanayoathiri jamii.

### 4.2.4 Sitiari

Istilahi hii kwa mujibu wa Lugwiri (2011:24) ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili tofauti au vyenye hulka tofauti pasipo na matumizi ya viungo vya lugha au vilinganishi kama vile, 'ja', 'mithili ya', 'mfano wa', 'kama' na kadhalika. Ulinganishaji huu huwa wa moja kwa moja ambapo kitu kimoja hutajwa kuwa kingine. Mbali na kudhihirisha ubingwa wa mtunzi, sitiari hulenga kusisitiza ujumbe katika kazi ya kifasihi. Hata hivyo, kulingana na Habwe (1999:65), sitiari huwa za urongo kwa kuwa zinavunja kanuni ya ukweli katika mawasiliano kama ilivyoelezwa na Grice (1975). Kwa maoni yetu, hii ni tamathali muhimu katika fasihi kwani inadhihirisha matumizi ya lugha kisanaa na aidha kuchimuza ukweli unaowahusu watu mbalimbali katika jamii, hasa katika riwaya za kimajaribio na kwa hivyo haifai kuchukuliwa kuwa urongo. Mwandishi ametumia sitiari kuchimuza mambo tofauti katika riwaya ya *Mafamba* kwa kufafanua sifa za kitu, mtu au jambo kwa kikihusisha na tabia za kile kinacholinganishwa nacho. Kwa namna hii, matumizi ya sitiari hujenga hisia au picha fulani ya suala linalorejelewa.

Katika uk 5, mtunzi analinganisha Arijojo na simba marara, mnyama mkali aishiye msituni na alaye nyama. Anachimuza jinsi Arijojo alivyopandwa na hasira na kubadilika kuwa mkali kama simba mwenye njaa ambaye tayari amepata mnyama awezaye kuwa kitoweo kizuri cha kukidhi njaa yake. Hasira zake zinazidishwa na udhalimu wa Maotad na machungu ya kushindwa kukabiliana naye ili kumwondoa uongozini. Anapoitazama picha yake iliyotundikwa ukutani,

hasira za mkizi zinampanda na kumfanya kuwa simba marara na kuanza kuitandika ile picha barabara kwa ncha ya bakora yake. Mwandishi anasema:

> "Hasira zilizidi kumpanda. Hakuwa Arijojo tena. Alikuwa ARIJOJO- simba marara aliyekuwa amechomwa mwiba mawindoni." (uk 5)

Katika wimbo wa kutukuza mafamba, sitiari inatumiwa kuonyesha sifa za mafamba. Mafamba yanarejelewa kuwa mtu safi na maisha ya binadamu. Huu ni wimbo ambao ulitungwa na wakereketwa wa Maotad kwa dhamira kuwa, ujihusishaji na mafamba ni njia safi na nyororo ya kuendeleza maisha ya binadamu. Kwa hali hii, mtunzi anachimuza utawala mbaya wa Maotad, mtindo unaowatawala takriban viongozi katika jamii. Kwa mfano:

Mafamba mtu safi sana

Mafamba mtu safi sana

Mafamba mtu safi sana

Maisha ya binadamu

Mafaaaaamba!!

Aidha, kupitia matumizi ya mbinu hii katika uk 11, jukumu mojawapo la Nikiabi linachimuzwa. Kulingana na maelezo haya, Nikiabi alikuwa ni mkono wa kulia wa Maotad na mwenye jicho moja. Kwa maana kuwa, alikuwa mshauri mkuu wake na tegemeo lake kuu katika kumjulisha na kumuelimisha kuhusiana na masuala kadha wa kadha ambayo yangemwathiri kwa njia moja au nyingine au kuhusiana na mambo ambayo angeyafanya Maotad ili kufanikisha miradi yake ya mafamba.

Sitiari imetumiwa kudhihirisha kwa uwazi jinsi msichana wa Engineer alivyokuwa mtoto mdogo aliyeanza utundu wa kutokuwa makini katika mtindo wake wa kuvalia ambao ulinuia kuwavutia watu tofauti. Katika matumizi haya, tunaambiwa kuwa 'mwanawe wa kike alikuwa ni toto shoo machachari kwelikweli' (uk 203). Machachari ni hali ya kutokuwa na makini ya kufanya jambo au hali ya kutotulia, ni utukutu au utundu nayo maana ya Toto shoo au kibahauli kwa mujibu wa Olali (2008:257) ni msichana aliyebalehe tu hivi karibuni na ambaye hujaribu kutembea kwa mikogo na kuvalia nguo za kubana akiwa na matilaba ya kujiachia ovyo kwa kila mtu.

### 4.2.5 Matumizi ya italiki

Kwa mujibu wa Shaw (1972), italiki hutumiwa kutofautisha mawazo, maneno na dhana mbalimbali ili kuleta msisitizo kwa msomaji. Maneno na mawazo hutiwa mkazo ili kumfanya msomaji aizingatie matini kwa uangalifu. Msomaji huathirika na kumakinika na kumwezesha atambue ujumbe. Sanaa ni jumla ya mbinu za fasihi na za kisanaa ambazo msanii huzifinyanga ili kuwasilisha kazi yake kwa ustadi. Olali ametumia italiki katika *Mafamba* kama mkakati na mtindo wake wa uandishi kwa njia inayochimuza waziwazi masuala anayonuia kuonyesha umuhimu wake kwa kuyasisitiza. Mbali na kwamba ametumia italiki kuonyesha maneno mapya na ya kigeni, misamiati ya lugha ya Dholuo na maneno ambayo kwa njia moja au nyingine yanaweza kusababisha kutoeleweka kwa hadithi, matumizi yake ya italiki kwa mfano katika aya nzima sio jambo la kawaida katika riwaya hii ya kimajaribio. Matumizi ya mbinu hii katika riwaya za kimajaribio ni kuupa ujumbe kipaumbele, kuusisitiza na kuonyesha mvunjiko wa jamii.

Mathalani, matumizi ya italiki katika dondoo lifuatalo yanaonyesha upotovu au ukaidi, kutokuwepo kwa uangavu na mvunjiko wa jamii. Hivyo, mienendo ya kisirisiri ya Maotad ya

kushurutisha na aidha ya kuhodhi idhaa za kitaifa zinachimuzwa kwa uwazi. Matumizi haya yanatuwezesha kutafakari kuhusu kila neno, sentensi au usemi ulioandikwa kwa italiki kwa njia inayoibua uelewa zaidi. Ni wazi kulingana na hadithi kuwa yote yaliyotangazwa kama inavyobainika katika dondoo lifuatalo yalikuwa kinyume na ukweli. Kuteuliwa kwa Avadi kama makamu wa Maotad na Maotad mwenyewe kulitokea baaada ya Avadi kushinikizwa kuyakubali masharti yote yaliyohusiana na kuasi kundi la NUKA na kujiunga kwake na kundi la BORA. Hali kadhalika wakazi wa Bikerani-Msiige hawakuwa wameapa kumuunga mkono U, bali huu ulikuwa mkakati wa Maotad wa kuwatatanisha ili wampigie kura. Kwa mfano:

> *"Hii ni Idhaa ya Redio NUKA. Habari ambazo zinatufikia katika chumba chetu cha habari zasema kuwa Avadi ameteuliwa kama makamu wa Maotad. Anaanza kutekeleza wajibu huo mara moja. Wakati huo huo, aliyekuwa makamu wa Maotad Bwana Saigeo ameachishwa kazi mara moja baada ya kujiunga na kundi haramu la BORA. Habari nyingine zasema kuwa kundi haramu la BORA ambalo linaongozwa na Amrao limepata pigo kubwa kufuatia kuhama kwa Avadi na kujiunga tena na NUKA. Akihojiwa, Avadi alisema kundi la BORA lilikosa mwelekeo na kwamba viongozi wake walikuwa wanatawaliwa na tamaa ya uongozi pasipo na sera maalum ya kuinua hali ya maisha ya wakazi wa Bikerani-Msiige. Avadi alikana madai eti alishinikishwa kulihama BORA baada ya kuahidiwa kiti cha makamu wa Maotad. Alisema ilikuwa ni hiari yake mwenyewe na hawezi tena kushirikiana na viongozi wa BORA kama vile Amrao ambaye alimtaja kama mbinafsi na mpenda ukabila. Habari zaidi za hivi punde zinasema wakazi wa Bikerani-Msiige wameapa kumuunga mkono U dhidi ya upinzani wa BORA. Katika kiapo walichokula na kundi la MK, walikana madai kuwa walilazimishwa na kundi hilo kumuunga mkono U. Mwisho wa taarifa hii ya habari kutoka idhaa ya Redio NUKA, Kar pi Mang'ich" (uk 157).*

Matumizi ya italiki katika dondoo lifuatalo yanachimuza kutimizika kwa ndoto za ukombozi kwa Wakazi wa Bikerani-Msiige kufuatia kushindwa kwa U na kwa NUKA kwa jumla. Ushindi huu

unapokelewa na tabasamu na furaha nyingi na wakazi hawa waliokuwa na imani ya kupata kiongozi mpya ambaye hakuhusiana na Maotad, aliyekuwa na hekima ya kuongoza na kutambua shida zao. Hii ni taarifa ambayo inaziponya nyoyo zao kwa kuwa waliamini mabadiliko yangetokea katika nyanja mbalimbali na kuboresha maisha yao. Taarifa ilisema:

> *"Hii ni Idhaa ya redio NUKA. Habari zinazotufikia katika chumba chetu cha matangazo zasema kuwa LiMioe amepata ushindi mkubwa wa idadi ya treya za vyakula baada ya kuhesabiwa kadamnasi ya watu kutoka sayari za nje. Boyi anakuwa makamu wake. U ambaye ni kiongozi wa kundi la NUKA amezipokea habari hizo kwa unyenyekevu mkubwa akisema shughuli hizo zilikuwa za haki tena huru. Aliahidi kushirikiana na utawala mpya wa LiMioe... Mwisho wa taarifa hii ya habari kutoka Idhaa ya Redio NUKA, Kar pi Mang'ich" (uk 181).*

### 4.2.6 Herufi kubwa

Herufi kubwa zimetumiwa kwa njia mbalimbali, mtindo huu unapatikana kwa kiwango kikubwa katika riwaya za kimajaribio kama *Mafamba*. Matumizi haya yanatokea katika kiwango cha neno ambapo neno moja linaandikwa kwa njia ya kuchanganya herufi kubwa na ndogo au kuandikwa kwa herufi kubwa pekee badala ya kuliandika kwa kuanza kwa herufi kubwa kama ilivyo katika nomino za pekee. Mbinu hii kwa mujibu wa Mgullu (1999:136-7) ni nomino ambazo hutaja vitu vya pekee, yaani kitu mahususi kwa sababu ni chenyewe tu hapa duniani kama majina ya watu, miji, nchi, mito na kadhalika na zinazoandikwa kwa kuanza kwa herufi kubwa. Kwa maoni yetu, herufi kubwa katika riwaya za kimajaribio au mpya hutumiwa kuchimuza kwa kuashiria mambo kadha wa kadha kama kuashiria nguvu, umilikaji na ubabadume, huonyesha masuala mazito, kusisitiza jambo, kuonyesha mtindo wa kiunguungu, huonyesha upaaji, ufikaji juu au kileleni kwa jambo, inatumika na msanii kuashiria kwamba kinachosemwa ni muhimu zaidi ya mengine

na huonyesha azma yake kwa msomaji ya kufuatilia neno. Kama tulivyotaja hapo awali, matumizi ya mbinu tofauti za lugha hudhihirisha ufasihi- matumizi ya kipekee ya lugha.

Herufi kubwa zimetumiwa kama ifuatavyo katika riwaya hii; LiMioe katika uk 8, ARIJOJO badala ya Arijojo (uk 5), MAFAMBA badala ya Mafamba (uk 240), MAZIMWI badala ya mazimwi katika (uk 70), DiPieLi, PiDi na DiPieNi (uk 6). Aidha katika riwaya hii, herufi kubwa zinatokea kwa katika sentensi, mwanzoni mwa kila sura na hali kadhalika katika kuandika ujumbe muhimu kama wa anwani katika gazeti na pia katika aya kama ifuatavyo;

> "VEMA ULICHOKITENDA. LABDA HUKUWA NA HIARI. LAKINI HUKUNITEGEMEA MIMI. UNGELIFANYA HIVYO, UNGELISALIMIKA. NYIE MNAOFANANA NA WANADAMU NIMEWAPA UHURU WA KUFANYA MAAMUZI YENU WENYEWE. UMEFANYA UAMUZI WAKO. UAMUZI WAKO NI MBAYA. UTAJUTA. UTAJUTA HIVI KARIBUNI. LAKINI SIZINGATII MATUKIO YA NYUMA. NAANGALIA YA SASA. YA SASA YANAFINYANGA YA USONI. YA USONI YANATEGEMEA YA SASA. NITAKUPA FURSA UWE MAKAMU WA MAOTAD. NUKA IMESHIRIKI MAFAMBA. UNAFAHAMU SITAKI MAFAMBA. MAFAMBA IMESABABISHA UMASKINI SEHEMU NYINGI NA HUSUSAN KARIFA. MAKABURI YAMENYAKULIWA. NINASISITIZA MAKABURI KWA SABABU WATOTO WANGU LAZIMA WAYATUMIE KAMA ZULIA WANAPOKUJA KWANGU. WEWE UMEAMUA KURUDI KUSHIRIKI MAFAMBA. VEMA. NENDA. LAKINI UKUMBUKE KUWA MUDA WAKO KAMA MAKAMU WA MAOTAD NDIO UTAKUWA MFUPI KATIKA HISTORIA YA KARIFA" (uk 158).

Matumizi haya ya herufi kubwa kwa kiwango hiki kikubwa ni njia mojawapo ya kutofautisha riwaya za kihalisia na za kimajaribio. Kwa mtazamo mwingine katika riwaya hii yametumika

kuonyesha kutokuwa na msimamo au ugeugeu hasa panapotokea mchanganyiko wa herufi kubwa na ndogo katika neno.

### 4.2.7 Kweli kinzani

Hii ni mbinu inayotumiwa kuelezea kauli au tamko ambalo licha ya kuwa linaonekana kujipinga lenyewe lina ukweli Fulani, Wamitila (2003:99). Matumizi yake katika riwaya mpya yanadhihirisha uhodari au ustadi wa mtunzi katika matumizi ya lugha mbali na kuwa pia ni njia ya ubunifu wake. Athari ya matumizi yake ni kuchimuza maneno na kusisitiza dhana katika ujumbe husika. Athari za uchimuzi zinabainishwa na uhusishaji wa matendo yanayokinzana na hivyo kutoa picha halisi ya yanayorejelewa. Pia, humwezesha msanii kuweka dhahiri uzito wa kihisia katika fikra za mhusika hasa kuhusiana na mtazamo wake wa ulimwengu. Matumizi ya kiujumi ya lugha, huvutia wasomaji kwa njia mpya na yenye kuibua hisia katika lugha, suala linalochukuliwa kutokea bila mpangilio. Katika riwaya ya *Mafamba*, mbinu hii imejitokeza kwa uwazi ili kubainisha ukweli mbali na kuwa matumizi yake yanadhihirisha ukinzani.

Katika dondoo lifuatalo la uk 27, mtunzi anataka kuonyesha kuwa ingawa Amrao na Maotad walitaka kuangamizana, hakuna hata mmoja aliyefaulu kumdhuru mwingine licha ya juhudi zao. Pia, kama ilivyo katika mfano wa uk 61 ni dhahiri kuwa wadhifa aliokuwa nao Maotad kama kiongozi wa NUKA ndio uliowavutia wengi kiasi kwamba hata yeye mwenyewe hakutaka kuacha kuongoza. Kwa sababu hakuwa na budi bali kuuacha, ilimbidi amchague mrithi wake na ambaye alimfahamu. Katika mfano wa uk 67 kama ilivyo hapa chini, ni wazi kuwa Kajo alielewa fika kuwa atapokea vitisho kutoka kwa Maotad kwa kuwa Maotad alipuuza mawaidha ya wengi yakiwemo yake kuhusiana na ushirikiano wake na Amrao. Kwa mintarafu hii, Kajo alikuwa mmoja wa wale waliotimuliwa na Maotad na wadhifa wake kupewa Amrao. Hali

kadhalika, katika mfano wa uk 108 kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo, ni wazi kuwa kundi la akina Fadhila lilikuwa limejitayarisha vilivyo kukabiliana na la U. Dondoo hizi hapa:

"Amrao alitaka damu ya Maotad na Maotad alitaka damu ya Amrao. Waliwindana usiku na mchana, mchana na usiku. Maotad alishinda. Amrao alishinda. Wote walishinda. Wote walishindwa," (uk 27).

"Kiti kimoja ndicho kilichokuwa muhimu hata hivyo- chake. Nacho hakutaka kukiacha. Nacho alitaka kukiacha. Nacho angemwachia nani? Nacho angemwachia fulani. Fulani huyo hakumjua. Fulani huyo alimjua. Kweli, alimjua. Alimjua lakini hakumfahamu" (uk 61).

"Onyo hili la rangi ya damu halikumshtua Kajo, licha ya kutoijua maana yake. Alijua onyo la rangi ya damu halikuwa na uhusiano na *rumkis malt.* Onyo la rangi ya damu lilikuwa na uhusiano mkubwa na *rumkis malt.*Zile "hatutaki" na "tunataka" zilipuuzwa na Maotad" (uk 67).

"Ndiyo tujipange. Maana hatujajipanga." Fadhila alijibu.

"Tumejipanga."

"Hatujajipanga."

"Tumejipanga."

"Hatujajipanga." (uk 108)

### 4.2.8 Methali na misemo

Methali ni muhtasari wa maneno ya kisanii yenye maana pana, ni mtindo wa lugha iliyofupishwa ili kutoa picha halisi ya jambo. Matumizi ya lugha katika fasihi humwezesha msomaji kukiona kitu, jamii au tajriba kwa njia mpya. Kwa mujibu wa Finnegan (1970:390), methali hupatikana takriban kila mahali barani Afrika na hubainika hasa katika maeneo wanapoishi Wabantu.

Hutumika katika tamaduni za Kiafrika kama njia ya kujielezea, kutoa taswira ya kitu au jambo na katika kuelezea mawazo ya kidhahania kwa kufinyanga lugha. Kwa ujumla, methali hutumiwa kutahadharisha au kuonya juu ya matendo mbalimbali, kufunza maadili, ni njia ya kupamba lugha au maongezi, hukosoa na kukashifu, hutumiwa kutoa mashauri, hufunza bidii na jitihada kwa wanadamu, hutumiwa kuelimisha jamii na pia kuliwaza na kufariji. Ingawa sifa hizi hubainika pia katika riwaya za kimapokeo, matumizi yake katika riwaya mpya kwa kawaida ni kukoleza masuala yanayosibu mataifa kwa mfano tabia za viongozi.

Methali kadha wa kadha zimetumiwa katika riwaya ya *Mafamba* na mwandishi ili kuchimuza maana tofauti na kuwasilisha dhamira yake. Katika uk 5, mwandishi anatumia methali 'kimya kingi kina kishindo kikuu' kuonyesha kimya cha Maotad baada ya Arijojo na Amrao kuungana ili wamfukuze mamlakani. Kimya hiki kama anavyosema mwandishi hakikupendeza na kama ilivyo maana ya methali hii, mtu ambaye huwa ni mnyamavu kwa muda mrefu huweza kuwa hatari anapokasirika. Kwa sababu hii, Maotad anabadilika na kuwa kiumbe wa kutisha na kukataa kabisa kutoka uongozini baada ya tukio hili la akina Arijojo (uk 6).

Matumizi ya methali 'umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu' katika uk 56 yanasisitiza nguvu za kushirikiana kwa wanadamu na wenzao maishani katika mambo yote wafanyayo. Hivyo, Maotad alitaka ushirikiano na Amrao, yaani kuungana kwa sayari ya NUKA na PiDiENI na kuwa kitu kimoja ili kutimiza azma yake ya kukabiliana vilivyo na kundi la LiMioe ili alishinde.

Boyi, mmoja wa wafuasi wa kundi la BORA alielewa kwamba, yeye, Fadhila na LiMioe hawangeweza kuwa vinara wa kundi la BORA. Ili kusisitiza ufahamu huu anatumia methali 'fahali wawili hawakai katika zizi moja' kama ilivyo katika uk 142 kuashiria kuwa, ingawa wote walishindania kuwa viongozi na walijihisi kuwa na uwezo huo, kamwe haingewezekana

kutwikwa jukumu la uongozi kwa pamoja. Aidha, wangeishi kubishana kwani wote walikuwa na uwezo sawa na hawangeweza kusikilizana kwa kuwa kila mmoja alitaka kuwa mkuu.

Aidha, kama inavyojitokeza katika uk 139, LiMioe aliamini kuwa ingekuwa bora apewe mamlaka ya kinara wa BORA kwa kuwa yeye na U walitoka katika jamii moja ya QiQu na hivyo ingekuwa bora amkabili kwa kuwa dawa ya moto ni moto. Methali hii 'dawa ya moto ni moto' imetumika kuonyesha jinsi LiMioe alivyohisi kwamba ushindi ungekuwa wake iwapo wao wawili wangekabiliana. Sababu ni kuwa walitoka katika kabila moja na kwa njia hii hakungekuwa na mgawanyiko wa kura na aidha mivutano ya kitabaka haingekuwepo wakati wa kupiga kura. Wanajamii wangemchagua aliyekuwa na uwezo zaidi kutegemea hulka na uwezo.

Semi ni tungo fupi za kisanaa zinazotumiwa kupitisha mafunzo na ujumbe wenye maana mahususi katika jamii kwa kutumia picha na ishara. Matumizi ya misemo katika kazi ya kifasihi hasa huwa kuchemsha bongo, kuchochea hisia fulani, kusisitiza jambo, kuhimiza na kufunza maadili, kupanua matumizi ya maneno na kuonyesha adabu katika lugha. Semi nyingi zimetumika katika riwaya ya *Mafamba*. Katika kuonyesha jinsi Kajo alivyokuwa na tabia ya kumpa Maotad sifa asizostahili, mtunzi anaelezea sifa hii kwa kutumia semi. Anasema: 'aliyefanya kampeini kubwa Amrao asinywe *rumkis malt* alikuwa Kajo, maarufu katika kumpaka Maotad mafuta kwa nyuma ya chupa' (uk 67). Kumpaka Maotad mafuta kwa nyuma ya chupa ni semi inayochimuza tabia mojawapo ya rafiki mkubwa wa Maotad, Kajo ambaye alifanya hivi kwa lengo la kupewa zawadi nono za mafamba.

Kutimuliwa uongozini kwa Saigeo na Maotad wakati ambapo wakazi wa Bikerani-Msiige walimtazamia kuwa kinara wa NUKA baada ya Maotad kustaafu kunachimuzwa kupitia kwa matumizi ya semi. Mwandishi anasema: "Maotad alikwishaamua kumzika Saigeo kwenye kaburi

la sahau. Na kweli alimzika- akiwa hai" (uk 88). Kwa Maotad, Saigeo alikuwa kama mwanafunzi na kama ilivyo, hakuna uwezekano wa mwanafunzi kumfunza mwalimu wake. Licha ya Saigeo kuwa msaidizi wa karibu wa Maotad, Maotad alikataa kabisa kumwachia uongozi.

Avadi anaposhurutishwa kuasi kundi la BORA na Maotad, anaamua kutii ili kusalimisha maisha yake. Ili kusisitiza umuhimu wa mwelekeo wake wa kusalimu amri, anatumia msemo "mwenye nguvu mpishe" na "wengi wape" (uk 159). Hakuwa na budi ila kusalimu amri kwa kuwa alifahamu kupigana na Maotad ni kama kushuka kutoka mchongoma, yaani mti wenye miiba. Kujiingiza vitani kwake Avadi kungemletea madhara chungu nzima na kwa hivyo alijizuia balaa kubwa kwa kutokuwa mkaidi.

Ili kufafanua kuwa watu mbalimbali walielewa na wengine hawakufahamu kabisa sifa mahususi za kiti maarufu cha wageni wa Maotad, mwandishi anatumia msemo 'kujua na kutojua kunguni mwake.' Yaani, kunao waliofahamu kilichosheheni katika kiti cha wageni cha Maotad na wengine hawakuwa na habari kabisa (uk 19).

### 4.2.9 Jazanda

Jazanda ni matumizi ya maneno yenye maana fiche. Katika riwaya hii, mtunzi ametumia jazanda mbalimbali kuashiria maana tofauti. Uchimuzi katika kazi ya kifasihi huambatana na kuvifinyanga vipengele vinavyojitokeza kwa uwazi. Matumizi ya mbinu hii katika riwaya za kimajaribio ni kukejeli na kuonyesha ujinga wa jamii na uongozi. Ili kuonyesha jinsi uongozi unavyotazamiwa na wengi kutegemea uzuri na manufaa, anatumia neno 'maji matamu' kama inavyotumika katika uk 4. Anasema: Arijojo naye aliamini maji "ni matamu, matamu na mataaaaaamu." Kila mmoja kama vile Amrao, LiMioe na Maotad mwenyewe walinuia

kuyanywa maji matamu yaani, kuwa viongozi ili wapate fursa ya kuingia chumbani. Matumizi ya jazanda 'chumbani' yanaonyesha jinsi watu hawa walitamani uongozi na wengine kama Maotad walikatalia katakata kuondoka uongozini kwa sababu ya manufaa aliyofurahia kila siku kama inavyojitokeza katika uk 6, 'Maotad alikataa katakata kuondoka kutoka chumbani'.

Mazoea ya viongozi ya kuwaangamiza watu ambao hupinga utekelezwaji wa nyendo mbovu na kukomesha uchunguzi wa vifo vyao kunadhihirishwa kwa kutumia jazanda. Kifo cha Rojoo kwa mfano kinatokea baada ya kula chapati moja kwa vipande saba vya nyama ya ng'ombe ambavyo havikutiwa sumu. Hii ni jazanda inayoashiria mauaji ya kisiasa ambapo watu huuawa na viongozi na sababu ya vifo vyao inabanwa kwa wananchi (uk 7).

Mwandishi anapoonyesha jinsi Amrao alivyofungwa jela ama kizuizini wakati wa utawala wa Maotad, anatumia jazanda ya 'kusukumwa ndani kula maharagwe' (uk 24). Huu ulikuwa wakati ambapo alijaribu 'kumwagia mchanga ndani ya kitumbua' yaani kujaribu kupinga serikali au kupindua utawala wa Maotad (uk 24). Ili kuelezea hatua ya kupiga kura, mwandishi anatumia jazanda ya 'vyakula kupakuliwa kwenye treya', yaani kura ziliwekwa kwenye visanduku vya kupigia kura kama ilivyofanyika wakati wa kupigia debe katiba na kura za baada ya miaka mitano zinazofanyika mara mbili katika riwaya hii.

### 4.2.10 Tashbiha

Neno hili linatokana na kitenzi 'shabihi' kwa maana 'kulingana na' au 'kuwa sawa na'. Vitu viwili hulinganishwa kwa kutumia vilinganishi: 'kama', 'mithili ya' na kadhalika. Hutumiwa katika kazi ya kisanaa na msanii ili kuwasilisha maana inayokusudiwa kwa mvuto zaidi. Olali ametumia tashbiha ili kulinganisha mambo tofauti, ulinganisho huu wa moja kwa moja unasisitiza na kuchimuza masuala kadha. Ili kuchimuza kwamba hakuna aliyeweza kubaini ikiwa

sayari ya DUNIA ama ya NUKA ndiyo iliyokuja kwanza anasema 'Ikiwa DUNIA ndiyo iliyokuja mwanzo ama NUKA, hili lilikuwa suala changamano kulitatua kama vile kupata jawabu kuhusu nani kati ya kuku na yai kaja mwanzo' (uk 27).

BORA inapojidhihirisha vilivyo kwa wananchi na sera zake kuwavutia, watu wengi wanapendezwa nayo. Wao waliona kuwa ubora wa BORA ndiyo iliyokuwa sera haswa ya kuigwa. Ili kuonyesha namna ilivyoenziwa nao kutokana na imani yao kuwa ilikuwa nzuri, mtunzi anasema: "Wao walikuwa kama abiria walioomba dereva lifti lakini hawakutaka kushuka kutoka kwa gari kwa vile ile lifti ilikuwa na kitu" (uk 101). Kwa kuwa askari wa Maotad walikuwa warefu sana, ili kusisitiza urefu wao, tashbiha hii inatumiwa: "Walikuwa ni watu warefu kama mlingoti-kiasi kama futi saba na nchi saba" (uk 148).

### 4.2.11 Kinaya

Kinaya ni hali ya mambo katika riwaya au hadithi kuwa kinyume na matarajio kama ambavyo imetumiwa katika riwaya ya *Mafamba.* Kwa mujibu wa Wales (1989:263), maana halisi hutokea kuwa kinyume ya maneno yaliyoelezwa na huwa mfano wa kejeli au dhihaka ambapo maelezo huashiria shutuma au dharau. Matumizi yake katika riwaya mpya ni kuonyesha ukosefu wa matumaini kwa wanajamii na kutowajibika kwa viongozi barani Afrika. Kwa sababu hii, lugha ya Kiswahili inakua kwa kiasi kuwa masuala ya kitaifa yanaelezewa kwa kuitumia kupitia kwa fasihi. Sayari ya NUKA inafahamika na utekelezwaji wa mambo mabaya na wafuasi wake. Ili mwandishi kuonyesha ukweli huu, anatumia kinaya kuisifu sayari hii kwa lengo la kusisitiza zaidi maovu yaliyokidhiri. Anasema: 'Sasa sayari hii iliitwa NUKA-sayari maarufu kupita sayari zote. Ndiyo, sayari ya NUKA. Sayari ambayo ilipata umaarufu wake kutokana na vitu vingi vyenye kuvutia- matapishi, hewa mbaya, mbwedu, dondandugu, uvimbe na kuliko yote,

mafamba. Naam, MAFAMBA' (uk 8). Ni kinaya kwamba licha ya sayari ya NUKA, DiPieNi, PiDi na DiPieLi kuwa sayari, wanasayansi hawakuwa wamezitambua, vitabu vingi vilichapishwa kuhusu sayari ya Dunia na pia Mars na wala sio sayari hizi (uk 11).

Aidha, ni kinaya kwamba, licha ya Maotad kuambiwa kila mara aende kwa kuwa muda wake ulikuwa umekwisha, yeye alijiona kijana sana na jibu lake kuhusiana na suala hili lilikuwa kinyume ya matarajio yao, "siendi." Alijihisi kama shababi na alizidi kusema haendi, alijiona mwenye miaka michache, yaani 720 akijilinganisha na viongozi wengine walioishi miaka 1440, yeye alikuwa nusu tu yao.

Hali kadhalika, ni kinaya kwamba Maotad alijua sababu ya watu mbalimbali kumpigia kelele za Maotad *sumt dan liwl og! Maotad sumt dan liwl og!*, sauti ambazo hakutaka kuzisikia kwa sababu zilimtisha, kumkata ini, kumtia homa, kiwewe, hofu na huzuni kila mahali. Hii ni kwa sababu alitakikana kuvichukua virago vyake na kuondoka ofisini kama kinara wa NUKA na kiongozi wa wakazi wote. Nafsi yake inaathirika kwa kiasi kikubwa na kumpelekea kutafuta mawaidha ya suluhu kwa viongozi wa sayari nyingine. Pia aliendа kwa mafundi waliosifika kwa kupiga ramli, kwa wanajimu gunge na mwisho kwa kitabu kilichoandikwa sheria za haki ya sayari ya NUKA ambapo ukweli dhahiri wa kutii amri ya karatasi ulipatikana (uk 59-60).

### 4.2.12 Chuku au udamisi

Istilahi hii kwa mujibu wa Wamitila (2003:31) ni hali ya kuikuza sifa ya kitu fulani kuliko kawaida, dhamira ikiwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo kwa njia inayochimuza masuala fulani katika kazi husika. Mwandishi ametumia chuku katika riwaya hii ili kusisitiza kwa kukiuka kaida za matumizi ya lugha zinazodhihirisha ufasihi kwa makusudi. Katika uk 7, anaelezea kuhusu sayari ya NUKA kwa njia ya kutilia chumvi ili kusisitiza jinsi sayari hii

ilivyoundwa kitambo sana na ilivyopata kufahamika na wengi. Anasema kuwa NUKA ilikuwa sayari ya zamani sana iliyopata kuumbwa wakati muumba alipoiumba KARIFA yapata miaka 4000 iliyopita. Sayari nyingine zilizoundwa zilikuwa kama vile NUZAPIFU, NUTA na ELIMO-FR na iliyopata kujulikana zaidi ilikuwa NUKA ambayo zamani ilitambulika kama NUKIA. Baadaye, wakazi wa Bikerani-Msiige waliibatiza jina jipya NUKA baada ya kuudhika na Maotad.

Fadhila anasemekana kuvalia viatu vilivyonakishiwa seja ya dhahabu ambavyo thamana yake ingewafadhili maskini wanne *four couse meal*, yaani mlo wa mikupuo minne kwa miaka minne kwa kuwa alikuwa na uwezo wa kifedha (uk 34). Siku ya mkutano wa mwisho wa kundi la BORA, uwanja wa mkutano ulikuwa na watu wengi sana. Ili kuchimuza wazo hili, mwandishi anafafanua jinsi ulivyokuwa umejaa watu hivi kwamba ulitapika na sindano haingeweza kupata nafasi ya kusimama wima (uk 176). Tabia ya Ngwena ya kuongeza mahasidi kila wakati inadhihirishwa kwa njia inayotia chumvi maneno. Ngwena alikuwa ni kati ya viongozi ambao waliposimama kutoa hotuba yoyote, kila mtu angeweza kutabiri atakachokisema hata kama ni stadi wa maisha ya falaki. Kilichojulikana ni kuwa baada ya kila hotuba, alikuwa ameongeza maadui zaidi kwenye orodha yake ya maadui (uk 216).

Katika riwaya hii mpya, mbinu hii inatumika kutia chumvi mienendo ya wanadamu inayowavutia sana na kwa hivyo kuwezesha waandishi kuelezea sifa zao bainifu kulingana na matendo yao bila woga. Masuala mazito yanayotendeka ulimwenguni huweza kuelezwa ili kuhamasisha jamii.

### 4.2.13 Ndoto

Kwa mujibu wa Malcom (1959:94), ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu ambaye yuko macho au amelala na yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikra za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, malengo, matarajio na matamanio. Ndoto basi, husafirisha tabia na sifa za mtu kwa sababu huambatana na matukio kadha katika maisha ya mwotaji na hali kadhalika picha halisi ya mambo anayowaza. Kulingana na Freud (1953:14), ndoto ni ushahidi wa kumbukumbu za matukio na mawazo ya mwotaji na hutokana na shughuli za kimawazo na mambo yaliyohodhiwa katika ung'amuzi bwete wa binadamu. Istilahi hii kwa mujibu wa Wamitila (2003:298) ni sehemu ya akili ya mtu inayohodhi fikira, mawazo, hofu na mitazamo hasi isiyokubalika na jamii yake ambapo hofu na mawazo hayo hujitokeza kwa njia ya ndoto. Hivyo, ndoto kama muundo wa uchimuzi katika kazi ya fasihi humfanya msomaji atafakari motisha kuu ya matumizi yake. Katika riwaya mpya, ndoto zinadhihirisha jinsi binadamu katika ulimwengu anavyojiona kama kiumbe anayeishi ama aliye katika dunia ya pili ila tu ndoto hizi zinaonyesha hali ya maisha yanayomwandama kutokana na mienendo yake na mambo yanayomzunguka. Lugha ya Kiswahili imekua hivi kwamba, ruwaza ya maisha ya binadamu inaweza kuelezwa kwa kutumia ndoto.

Ndoto nyingi zinabainika katika riwaya ya *Mafamba*. Kama ndoto ya kijinamizi inayootwa na KEFO na PiDi na kusimuliwa na Boyi. Katika ndoto hii, Boyi anasimulia jinsi usiku wa manane wakazi wa KEFO na PiDi waliamka na kujipata na makovu mashavuni mwao yaliyohitilafiana kutoka mkazi mmoja hadi mwingine. Kila mmoja alikuwa na ishara moja ya kovu iliyofanana katika kila sehemu ya mwili wake. Makovu haya yaliyotamalaki katika miili yao yalikuwa yamefinyangwa kwa herufi F, A, M na B kwa kutumia chuma moto.

Baadhi yao walikuwa na makovu machache ilhali wengine walikuwa na mengi. Kwa wengine, herufi hizo zilikuwa zimeandikwa kwa ustadi na zilionekana zikiwa nyingi huku zingine zikiwa shaghalabhaghala. Kwa mashavu yao, kulikuwa picha ya aina zote chafu. Fundi aliyeziandika herufi hizo alitumia uma mkubwa wenye ndimi tatu na cheche za moto nchani na hakuonekana vizuri, alikuwa ni kama ukungu au pamba. Kiwiliwili chake fundi huyo kilikuwa ni kama moshi uliojenga kizungumkuti kwa herufi zilizoonekana wazi. Herufi hizo zilikuwa T, O, M na D ambapo herufi A ilijitokeza mara mbili (uk 41-42). Hii ni ndoto inayochimuza jinsi Maotad mshirika mkuu wa mafamba alivyowaambukiza wakazi mbalimbali tabia ya kuabudu mafamba, tabia ambayo waliikumbatia kwa kuwa waliipenda kiasi cha kuifanya kuwa hali yao ya maisha.

Katika ndoto nyingine uk 62-65, Maotad anaota ndoto ya kijinamizi, ndoto inayomjia mara kwa mara. Katika ndoto hii, anawaona swila saba walioota ndimi zenye cheche kali za moto ambao walikuwa wakimfukuza huku hasira zimewapanda. Walikuwa na vichwa vya watu ambao aliwatambua kama LiMioe, Amrao, Boyi, Sinya na Fadhila ila sura ya saba haikuonekana vizuri na ndiyo iliyokuwa ikiwahimiza wengine kumfukuza. Swila huyu ambaye sura yake haikuonekana vyema alitokomea na kutokea na majoka mengine matatu yenye vinywa vitatu kila mmoja. Hawa waliungana na wale saba huku majina yao yakiwa yameandikwa utosini. Walikuwa na mabawa na majina yao ni Ka-MJ, Jimase, Alekimu na sura ya Rojoo, sura ambayo haikubainika hapo awali. Hawa walitoa sauti za kutisha za kumfukuza Maotad, walimtaka achukue mizigo yake ya mafamba kama vile masanduku, vikombe, sahani, nguo na vyote vilivyokuwa vimebeba mafamba. Mikononi, walibeba silaha za aina nyingi kama vile mawe, mishale, mikuki, mitambo, sumu, visu, rungu pamoja na nguo nyekundu iliyokuwa na maneno 'MAFAMBA SI MTU SAFI. Mwanzoni, Maotad aliweza kukimbia mbio lakini baada ya muda mfupi alijaribu kukimbia lakini akashindwa. Walimfukuza huku wakimfungia barabara baada ya

kutambua karata zake na kumtangulia alipokimbilia kutafuta usalama na kwa pamoja walimsukumia mateke mazito makalioni ambapo aliamka kutoka usingizini.

Hii ni ndoto inayobainisha woga wa Maotad wa kuondolewa uongozi na kuwa akina Amrao, Boyi, Fadhila na LiMioe walikuwa mfano wa akina Rojoo, Ka-MJ, Jimase na Alekimu ambao walipata kuishi katika sayari ya NUKA lakini kutokana na juhudi zao za kupigania ukombozi wakafa vifo vya ajabu ambavyo havikufahamika vilivyotokea. Walikuwa wanapinga vikali mafamba yaliyoendelezwa na Maotad. Hawa ni watu waliokuwa na mwelekeo wa kimtimua Maotad uongozini kama walivyofanya akina LiMioe baada ya kuelewa njama zake na jinsi alivyokuwa akiwachezea watu akili. Utabiri wa ushindi wao unajitokeza katika ndoto hii ambapo anasukumiwa mateke na baadaye kufungiwa barabara.

**4.2.14 Nyimbo**

Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti ya kupanda na kushuka na hunuia kutumbuiza, kukejeli, kufunza, kubembeleza, kuliwaza na kusifu. Kulingana na Mukhata (2011:53), nyimbo hutumiwa kusawiri hali za kisaikolojia za wahusika za kuibua mawazo na hisia zao za ndani zinazowakumba na pia katika kupeleka mbele kisa na maudhui ya kazi. Nyimbo nyingi zimejitokeza katika riwaya hii ili kuondoa ukinaifu na kuchimuza maana tofauti. Uchimuzi katika matini za kifasihi huibua athari fulani kwa msomaji. Kwa kuwa kuna aina tofauti za nyimbo kama vile nyimbo za mapenzi, za arusi, mbolezi, za dini, vita, za watoto miongoni mwa zingine, nyimbo zinazojitokeza katika riwaya hii ni za kisiasa. Hizi huimbwa ili kuwasifu au kukashifu viongozi au uongozi. Matumizi ya nyimbo yanaonyesha mabadiliko katika uandishi wa riwaya za Kiswahili ambapo hisia za binadamu zinaelezwa.

Katika uk 27-28 wimbo unaotungwa na kuimbwa na Amrao akiwa kizuizini unatuonyesha matumaini aliyokuwa nayo. Alikuwa na imani ya kuleta mabadiliko na kwa namna hii kutetea haki za wakazi wa sayari zote, kufungua kambi za kusoma, kuongeza vituo vya afya, kujenga barabara, kuleta usalama, kufufua uchumi na kukomesha mafamba. Naye Maotad alikuwa na imani tofauti kama kiongozi wa NUKA, alinuia kuendeleza mafamba daima kwa kuwa yalisababisha maendeleo katika NUKA kama vile ya ukarabati wa barabara na kuleta mvua. Kwa wafuasi wake, mafamba yalikuwa mtu safi na maisha ya binadamu wala hawakujali mitazamo ya wengi kuhusiana na mafamba mathalani kama yalikuwa mtu, jitu, aina ya dhehebu ama sera (uk 29-30).

LiMioe pia anaimba wimbo wa mafamba hasa anapotambua kuwa uongozi wa Maotad ulifanikishwa na mafamba katika kinyang'anyiro cha kubaini mshindi katika kipindi cha baada ya miaka mitano ambapo kura zilipigwa. Anapotambua kuwa sera ya mafamba ndiyo iliyomwezesha Maotad kupata ushindi, anauimba wimbo wa aila yake ila tu anabadilisha mahali pa NUKA na kuwa PiDi. Sababu ni kuwa, hapo awali alikuwa mshirika wa NUKA aliyehusika na nyendo kama zake. Kwa mintarafu hii, ni wazi kuwa viongozi wote wanapenda mafamba na wengi hufikiria uwezo na nguvu za mafamba na kuamua kuzitegemea wakati ambapo njia za kawaida hazizalishi matunda wanayoyataka (uk 35-36).

Wimbo wa uk 92-94 unachimuza jinsi U alivyotazamwa na kundi la NUKA kama mwenye uwezo wa kuongoza tofauti na alivyokuwa akitazamwa na wanakikundi wa BORA. Kwao, U alikuwa mzee kamili na wala sio mtoto. Alikuwa na uwezo wa kuwapa mambo mema kama mafamba, kuleta konfushoni kwa wakazi wa Bikerani Msiige na hali kadhalika kuwahifadhi ili waendeleze mafamba kutokana na hekima yake iliyokuwa sawia na ya Maotad. Pia, walifurahia kwa sababu Maotad alimchagua badala ya Saigeo, Avadi, Kanga, Kamu na Amrao. U

hakuwaogopa 'paka', yaani wafuasi wa NUKA wa tangu zamani ambao walifurahia *'cerelac'* (maziwa) yaani, vitu ainati vilivyotokana na mafamba.

### 4.2.15 Ukweli bunilizi

Ukweli katika bunilizi ni mbinu ya kuwasilisha ukweli kama tunavyojua lakini kupitia mbinu za kibunilizi ambazo ndizo zinazotofautisha sanaa na mapisi au historia. Kulingana na Wamitila (2003:298), dhana hii hurejelea ukweli fulani wa maisha ya ulimwengu unaosawiriwa katika fasihi na wenye sifa za kilimwengu. Ni mtindo wa riwaya ya kimajaribio wa kueleza mambo ambayo hayaelezeki kwa njia ya kawaida. Mwandishi huchukua tukio la kiuhalisi na kuliunda vingine ili kulisisitiza. Uandishi huu unatofautisha riwaya za kimapokeo na mpya, ithibati kwamba lugha ya Kiswahili inakua kila uchao. Utaratibu katika kazi ya kifasihi ni muundo na kwa hivyo hufuata utaratibu na mfumo fulani katika kuchimuza maana. Riwaya ya *Mafamba* ambayo tunaihakiki kama riwaya ya kimajaribio au mpya inaelezea historia ya Kenya, yaani msuko wa matukio ni reale kwa ya pili ukinasibishwa na historia ya taifa hili letu. Ni matukio ya tangu mwisho wa uongozi wa Rais mstaafu Moi (Maotad), utawala wa Emilio Mwai Kibaki (LiMioe) hadi utawala wa kugawana mamlaka baina ya Kibaki na Waziri Raila Amolo Odinga (Amrao).

Mambo mengi yanayodhihirisha uhalisi wa hadithi hii kujumlisha jamii yetu ni pamoja na kuungana kwa Rais mstaafu aliyekuwa wa KANU (NUKA) na Raila Odinga aliyekuwa wa NDP (DiPieNi) na kuunda chama kipya kinachorejelewa na mwandishi kama NUKA YAMP-NUKA MPYA (uk 22). Joseph Kamotho (Kajo) kutimuliwa kama katibu mkuu wa KANU mpya na mahala pake kuchukuliwa na Raila Odinga baada ya kuteuliwa na Maotad. Kibaki (LiMioe), Wamalwa (Boyi) na Ngilu (Fadhila) kuungana na kuunda muungano wa kisiasa NARC (BORA)

na baadaye kuungana kwa kundi la Amrao na lile la Kibaki na kuunda BORA (Narc Rainbow). Vilevile kushurutishwa kwa Avadi (Mudavadi) kuwa makamu wa rais wa Maotad na Maotad. Kitendo kilichomfanya awekwe katika kumbukumbu za historia ya Kenya kama makamu wa rais aliyepata kutawala kwa muda mfupi.

Aidha, kuteuliwa kwa Kibaki kama mgombezi wa urais na wanachama wa BORA na kuweka mkataba wa makubaliano mojawapo likiwa kuunda katiba mpya kwa siku mia moja ili kubuni nyadhifa zaidi za uongozi kama uwaziri mkuu wa Raila. Jambo ambalo halikutimizika kwa siku hizo. Kibaki kupata ajali katika makutano ya njia ya kutoka Nzambani, Kitui na kuelekea Nairobi-Kar Pi Mangi'ch na jinsi Amrao aliendeleza kampeni zake na uchaguzi wa mwaka 2002 ukaendelea. Kibaki kupata ushindi mkubwa kwa asilimia kubwa huku U akishindwa. Narc (BORA) kuchukua usukani huku Kibaki akiwa Rais na Wamalwa (Boyi) akiwa makamu wake na baadaye kuteuliwa kwa Moddy Awori (Damisi) kuwa makamu wa Rais baada ya kifo cha Wamalwa.

Mgawanyiko wa Narc uliosababishwa na uundaji wa katiba ambapo kulizuka makundi mawili. Kundi lililounga na kuongozwa na LiMioe na kushabikiwa na Saigeo (George Saitoti), Mungatana (Ngwena) na Moddy Awori na lililopinga la Amrao (Raila), Kalonzo (Kamu), Musalia Mudavadi (Avadi) na Chebii Kilimo (Bi.Zaraa) miongoni mwa wengine. Kura ya maoni kuhusiana na katiba iliyopingwa mwaka wa 2005 kulisababisha kushindwa vibaya kwa mrengo wa Kibaki. Jambo lililopelekea mawaziri wote waliopinga wafutwe kazi na kwa njia hii mzozo mkali ukazuka. Huu ukawa mwanzo wa uhasama wa kisiasa hadi mwaka wa 2007 ambapo uchaguzi mwingine ulifanyika na wengi kama Moddy Awori (Damisi) wakatimuliwa uongozini na wananchi.

Hali kadhalika, kuzuka kwa suitafahamu za kumtambua mshindi kati ya Raila na Kibaki kwani hakukujulikana bayana aliyekuwa mshindi katika uchaguzi wa mwaka 2007. Hali iliyosababisha kuzuka kwa vita na uharibifu wa mali na vifo. Hali iliyolegea baada ya mkataba wa amani wa kugawana mamlaka kati yao, jambo lililotekelezwa na mwananchi kutoka nchi ya nje, na kukaundwa baraza la mawaziri arobaini (uk 252). Matukio mengi ya kikatili yaliyotokea wakati wa utawala wa Moi yanadhihirishwa kama vile kifo cha Robert Ouko (Rojoo) uk 7, uongozi wa Jomo Kenyatta (Jokaga) uk 228, na upinzani mkali wa kisiasa wa $O_2$ (Oginga Odinga) uk 49.

Mandhari ya mahali na wakati yanachimuzwa kupitia mbinu ya ukweli katika bunilizi. Bikerani-Msiige ni mahali panaposawiriwa kama mtaa wa mabanda-kibera ambako ni sehemu karibu na alikoishi Maotad. Pia matumizi yake yanabadilika na kuwa kiwakilishi cha taifa au nchi ya Kenya kama inavyobainika katika uk 236 "Wakazi wa Bikerani-Msiige wanaombwa kurudi kazini kuendelea na ujenzi wa Taifa." Aidha kasri la Maotad linasawiriwa kibunilizi, hili lilikuwa jumba kubwa na lenye vyumba vya mateso kwani Avadi anapopelekwa huko, chumba kimoja kilikuwa na damu mbichi (uk 152). Mahali pengine pa mateso palikuwa mkanyangeni, yaani '*nyayo house*' ambapo watu wengine kama vile Charles Rubia (Charu), Matiba Stanley Njindo (Mastanji) na Raila walipata kuteswa (uk 48).

Hoteli zimesawiriwa kibunilizi, Haponaseremwige- Serena na Hakuna uma-Norfolk, mahali palipofanyiwa mikutano ya siri ya kisiasa kwa kundi la Amrao na LiMioe. Mji mkuu wa Bikerani- Msiige ni Kar Pi Mang'ich (Nairobi- mji wa maji baridi) ambapo mikutano katika mji huu ilifanyika katika Come-K (Kamukunji), mahali ambapo Maotad alifanyia U (Uhuru) kampeni za urais na Tortoise- Ran Court (Kasarani), mkahawa mkubwa ambao mandhari yake yalikuwa kama ya Haponaseremwige ila tu hapa kulikuwa na ukuta mkubwa uliozunguka ili kuwahami wageni mashuhuri waliokwenda pale kujituliza na kupunga hewa.

Madaktari wa Biandi-wanajeshi wa Nanyuki Airbase na wa Bae-Eastleigh Air base wanasawiriwa kibunilizi. Taasisi ya bunge pia, inasawiriwa kama nyumba ya kuzitunga sheria na jumba kuu la midahalo. Mikoa ya Kenya imebuniwa kama Ma, Ai, Fa, Ao, Me, Bi na Au (uk 234-235). Wakati pia haukusazwa katika ubunifu huu ili kurejelea tarehe muhimu katika historia ya Kenya. Mathalani, umri wa Maotad ulikuwa miaka 720 (72), sayari ya NUKA ilikuwa na miaka 400 (40) tangu kuundwa kwake. Wakati wa utawala wa Maotad, ilimchukua LiMioe miaka 200 (20) kumuasi Maotad, na kuwa kwa miaka 100(10), Maotad alikuwa na uhusiano mwema na Arijojo. Tarehe mbalimbali katika kalenda ya jamii yetu pia zimebainika kibunilizi. Tarehe ya uchaguzi baina ya U na LiMioe ilikuwa 12/27/2200 (27/12/2002). Pia kura ya maoni imesawiriwa kibunilizi 11/12/2500 (11/12/2005) uk 213. Tarehe ya uchaguzi wa Rais kati ya Amrao na LiMioe ilikuwa 12/27/2007 (27/12/2007), tarehe iliyoleta masikitiko kwa wengi (uk 241). Hatimaye, tarehe ya kutiwa sahihi ya kugawana mamlaka kati ya LiMioe na Amrao 2/28/2800 (2/28/2008) uk 252 na ilipofika tarehe 4/13/2800 (13/4/2008) sayari ya BORA ilizaliwa upya na viongozi wapya.

Wahusika wengine waliosawiriwa kibunilizi Nikiabi-Nicholas Kiyator Biwott, Shanata- Sharrif Nasir Taib, Kanga-Katana Ngala, Bwana Paka-Kamlesh Pattni, Kanje-Njenga Karume, Mumu-Mutava Musyimi, Engineer-Mshirika wa Anglo-leasing, Ngwena-Danson Mungatana, Bwana Twajua- Sauti au watu wanaopinga ufisadi, Sinya-Simon Nyachae, Bwana Kachuoheze-Hezekaya Ochuka, Ka-MJ- JM Kariuki na Alekimu- Alexander Kipsang' Mugo.

## 4.3 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeelezea nafasi ya uchimuzi katika kiwango cha matumizi ya lugha. Tumebaini kuwa, utanzu wa riwaya ya Kiswahili umebadilika kutoka kwa utunzi wa riwaya za

kimapokeo hadi riwaya mpya, athari inayobainika kwa jinsi waandishi wana uhuru wa kufinyanga lugha zaidi kwa kuyaweka wazi masuala yanayotokea barani Afrika. Pia, tumebainisha kuwa matumizi ya lugha katika riwaya hii yanachimuza maana tofauti zinazodhihirisha kwa uzito masuala muhimu ambayo mwandishi alinuia kuyasisitiza. Aidha, tumebainisha kuwa, matumizi haya ya lugha katika riwaya hii yanadhihirisha sifa za Wana-Urasimu kama mitindo mipya ya uwasilishaji wa kazi ya kifasihi kwa njia inayochimuza ujumbe, uajinabishaji au kufanya ajabu ambapo vipengele vya lugha hutumiwa kwa njia inayovitokeza kwa uwazi tofauti na njia ya kawaida na kuonyesha ufasihi, ambao ni matumizi ya kipekee ya lugha. Hivyo, uchimuzi katika kiwango hiki unaweka ukweli kuwa dhana ya uchimuzi katika riwaya hii ni nguzo kuu katika uendelezaji wa dhamira na maudhui.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura hii ambayo ni ya mwisho katika utafiti wetu, tumejadili kwa muhtasari matokeo ya utafiti huu kuhusiana na yale tumeyatekeleza na kuyaibua. Tunakusudia kubaini iwapo madhumuni yetu ya utafiti yameafikiwa, kupima nadharia tete za utafiti wetu na hali kadhalika kutoa mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu.

## 5.1 KUHUSU MADHUMUNI YA UTAFITI

Tulidhamiria kutekeleza madhumuni yafuatayo katika utafiti huu:

Kwanza, tulidhamiria kuonyesha nafasi ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio au riwaya mpya ya Kiswahili ya *Mafamba*. Tumetekeleza dhamira hii katika sura ya tatu na ya nne ambapo tumeonyesha uchimuzi katika kiwango cha wahusika na matumizi ya lugha. Kwa kufanya hivyo, tumebaini kuwa usimulizi katika riwaya hizi unayachimuza mambo kadha kupitia kwa wahusika na matumizi ya lugha kwa njia inayodhihirisha kwa uwazi na uzito masuala nyeti ambayo licha ya kukumba jamii zetu, hujitokeza kwa sura sawia katika mataifa ya Kiafrika.

Katika uhakiki wetu wa riwaya ya *Mafamba* kama riwaya ya kimajaribio, tumebaini kuwa kwa kiasi kikubwa muundo wa riwaya hizi ni tofauti na za jadi kwa kuzingatia vipengele vya msuko, usimulizi na matumizi ya lugha. Haya ni mambo tuliyoyagusia katika sura ya kwanza ambapo tuliweka wazi sifa kuu za riwaya hizi na katika sura ya nne ambapo tulibainisha kuwa utanzu wa riwaya umekua kwa kiwango kikubwa kutoka uandishi wa kimapokeo hadi wa kimajaribio. Katika sura ya pili, tulielezea msuko wa riwaya ya *Mafamba* ambao unajenga uelewa wa riwaya

hii na aidha kuchimuza dhamira na maudhui. Katika sura ya tatu, tulionyesha kuwa usawiri wa wahusika unaelekea kubatilisha dhana nzima ya uhusika ila tu wanadhihirika katika jamii kulingana na matendo na tabia zao. Katika sura ya nne, tumethibitisha kwamba matumizi ya mbinu tofauti na mwandishi katika uandishi wa riwaya hizi unachimuza sifa za uandishi za Wana-Urasimu kama uajinabishaji na ufasihi na ukuaji wa utanzu wa riwaya kiuandishi.

Pia, tulinuia kuonyesha kuwa utanzu wa riwaya ya Kiswahili unakua kila uchao kwa sababu ya matumizi ya mitindo mipya ya uandishi. Wazo hili ni dhahiri kutokana na utafiti wetu kwa jinsi uchunguzi wetu wa riwaya ya *Mafamba* umebaini ukweli huu. Katika riwaya hii, mtunzi ametumia mbinu ya ukweli bunilizi ili kuelezea baadhi ya matukio yaliyotendeka katika utawala uliopita na uliopo katika taifa letu ili kubaini jinsi watawaliwa huathirika kutokana na uongozi mbaya wa viongozi ambao sifa zao huelekea kufanana muda mfupi tu baada ya kuchaguliwa. Mwandishi amefanikiwa kuyafafanua masuala haya kutokana na mbinu ainati katika uwasilishaji wa dhamira yake, jambo ambalo halingefaulishwa kwa kutumia mitindo ya jadi ya uandishi.

Uchunguzi wetu wa riwaya ya *Mafamba* ambayo ni ya kwanza ya Olali umebaini kuwa, hii ni riwaya ya kimajaribio mbali na kuwa inaweza kuhakikiwa kwa njia nyinginezo kwani inadhihirisha sifa tofauti za riwaya hizi kama upya katika usanii na maudhui kulingana na namna yanavyowasilishwa, ndoto zinazoingiliana na ukweli, mchezo wa lugha na miundo mipya inayojaribu kuasi kwa makusudi uhalisia unaohusishwa na riwaya za jadi. Huu ni uhalisi unaotokana na mjadala wetu wa sura ya tatu na nne ambapo lugha imetumiwa kutilia mkazo na kuchimuza hali ilivyokuwa na ilivyo sio tu katika nchi yetu, mbali hata katika ujirani wetu.

Ili kufikia malengo haya, tulitumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi kama kifaa cha uchanganuzi. Katika kutumikiza mwelekeo huu, tulilenga kuonyesha kuwa fasihi humwezesha msomaji

kukiona kitu, jamii au tajriba fulani kwa mwanga mpya kutokana na sifa ya uajinabishaji, kama ambavyo tumefanikiwa katika utafiti wetu kuchimuza mambo mbalimbali yaliyodhihirika katika kiwango cha wahusika na matumizi ya lugha. Katika uwasilishaji wa riwaya ya *Mafamba,* hulka na sifa bainifu za wahusika zimechimuzwa na hali kadhalika katika matumizi ya lugha, kanuni kuu za Wana-Urasimu zimechimuzwa kutokana na jinsi mtunzi amebadili kwa makusudi elementi za lugha.

## 5.2 UPIMAJI WA NADHARIA TETE

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete tatu kuu:

Kwanza, dhana ya uchimuzi imechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya ya *Mafamba.* Uchunguzi wetu umethibitisha ukweli wa nadharia tete hii. Katika riwaya hii ya *Mafamba*, mtunzi amekiuka kimakusudi kaida za matumizi ya lugha na kuwafanya wahusika na vipengele vya mtindo wa lugha vijitokeze. Hali hii ya kujitokeza au kuchimuza imetumiwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya hii kwa ambavyo mienendo, hali ya wanaohusika na matukio yaliyotokea kitambo yanatambulika bila tashwishi. Ni mbinu iliyotumiwa kwa usanii mkubwa ili kutoa taswira kamili ya mapambano kamili kati ya wanasiasa na ukatili wao hasa wanapopigania uongozi.

Wananchi wamesawiriwa kama watu muhimu wenye kuleta mabadiliko nchini mwao kupitia kwa uamuzi wao wakati wa kupiga kura. Aidha, ni wazi kuwa wao hupokea dhuluma za aina tofauti kutoka kwa viongozi wanaowachagua kwani wao hughairi nyendo zao pindi tu wanapoibuka washindi. Uchimuzi wa masuala haya unavuta makini ya wasomaji, kuzitekenya na kuziathiri hisia zao na kwa namna hii kuwa msingi wa kuyakumbuka matukio haya yanayotoa mafunzo mengi kwa mzalendo yeyote wa nchi. Kwa mintarafu hii, nadharia yetu ya pili kuwa

dhana ya uchimuzi ndiyo mhimili mkuu wa dhamira katika uendelezaji wa riwaya ya *Mafamba* inajibainisha. Ni msimamo wa tasnifu hii kuwa, bila ya matumizi ya uchimuzi, riwaya hii ingepwaya katika dhamira yake. Dhamira kuu ya kuonyesha uozo wa viongozi inafanikishwa kupitia uchimuzi wa wahusika na matumizi ya lugha ambapo pia maudhui mbalimbali yanabainika.

Nadharia tete ya tatu ya utafiti huu ilidai kuwa, *Mafamba* ni riwaya inayoweza kuhakikiwa kama riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili mbali na kuwa inaweza kuhakikiwa kwa njia nyinginezo. Uchunguzi wetu umethibitisha dai hili kuwa la kweli. Hii ni kwa sababu riwaya hii inaweza pia kuhakikiwa kama riwaya ya kihistoria kwani mchakato wa matukio yote ya riwaya yanahusu historia ya nchi ya Kenya. Pia inaweza kuhakikiwa kama riwaya changamano kufuatilia muundo wake ambao si sahili na hali kadhalika kama riwaya ya kisanaa kwa kuwa ufundi wa kiutunzi unachukua nafasi kubwa.

Kimsingi, uchimuzi umechukua nafasi kubwa katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba* katika kiwango cha wahusika na matumizi ya lugha kwa kiasi ambacho dhamira ya mtunzi inajitokeza. Kwa jumla, utafiti huu unatilia mkazo kwamba uchimuzi ndio nguzo kuu ya uendelezaji wa riwaya hii katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Matumaini yetu ni kwamba, utafiti huu utakuwa msingi bora wa uchanganuzi wa uchimuzi na aidha wa riwaya za kimajaribio. Kwa kuwa utafiti wetu unahusu dhana ya uchimuzi katika riwaya hii, bado tafiti zaidi zinahitajika kwa kuzingatia mielekeo mingine ya kuihakiki riwaya hii. Kwa sababu hiyo tumependekeza utafiti zaidi kuhusu mambo yafuatayo:

1. Kuihakiki riwaya ya *Mafamba* kama riwaya ya kimajaribio au mpya kwa kuzichanganua sifa muhimu za riwaya hii.
2. Kutathmini nafasi ya uchimuzi katika makala mbalimbali yaliyochapishwa.
3. Katika uchunguzi huu, tuligundua kwamba riwaya hii mbali na kuwa ya kimajaribio inaweza kuhakikiwa kwa njia nyingi. Hivyo, uchunguzi zaidi unahitajika ili kuihakiki kama riwaya ya kisanaa, ya kihistoria au changamano.

**MAREJELEO**


Atsiaya, M. A. K. (2002) *Uhakiki wa Sigana kama Drama ya Kimajaribio*. Tasnifu ya Shahada ya uzamili . Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Baldic, C. (2001) *Oxford Concise Dictionary of Literary Terms*. Oxford: Oxford University Press.

Cluysenaar, A. (1976) *Introduction to Literary Stylistics*. B. T Batsford Limited: London.

Crystal, D. (1997) *Dictionary of Linguistics and Phonetics*. 4th edition. Oxford: Blackwell.

Erlich, V. (1969) ***Russian Formalism.*** 3rd Edition. The Hague: Mounton & Co.N.V Publishers.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa*. London: Oxford.

Finke. D. (1989) *Literary Criticism and Theory: The Greeks to the Present*. London: Longman.

Fokkema, D. W. & Kunne-Ibsch, E. (1979) *Theories of Literature in the Twentieth Century*. USA: C. Hurst & Company.

Freeman, D. C. (1970) *Linguistics and Literary Style*. University of Massachussets: Holt Rhinehart and Winston.

Freud, S. (1953) *The Interpretation of Dreams*. London: Hogarth Press.

Holman, C. H. (1976) *A Handbook of Literature*. Indianapolis: The Odysseypress.

Habwe, J. (1999) *Discourse Analysis of Swahili Political Speeches*. Tasnifu ya Shahada ya uzamifu. Imechapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Iribemwangi, P. I. na Mukhwana, A. (2011) *Isimu Jamii.* Nairobi: Focus Publishers.

Kadenge, K. E. (1982) "*Deviation and Foregrounding in chosen Swahili literary texts.*" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili: Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

*Kamusi ya Karne ya 21* (2011) Nairobi: Longhorn Publishers.

Kezilahabi, E. (1990) *Nagona.* Nairobi: Vide~muwa Publishers.

............... (1991) *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University press.

Leech, G. N. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Leech, G. N. na Short, M. A. (1981) *Style in Fiction: An Introduction to English Fictional Prose.* London: Longman.

Lugwiri, P. O. (2011) *Stiari, Taashira na Tashibiha katika Uwasilishaji wa Dhamira katika Utenzi wa Tambuka*: Uhakiki wa kimtindo. Tasnifu ya shahada ya uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Malcon, N. (1959) *Dreaming* U.S.A: Routledge and Kegan Paul Ltd.

Masinde, E. W. (2007) *Mawanda ya Isimu- Jamii*. Nairobi: Cedar-Pine Lithographics.

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard textbook Graphics and Publishers.

Mgullu, R. S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mkufya, W. E (1999) *Ziraili na Zirani.* Dar es Salaam: Hekima Publishers.

Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991) *Riwaya ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University press.

Mukhata, C. W. (2011) *Uhakiki wa riwaya ya Nyuso za Wanawake na Said Ahmed Mohamed: Mtazamo wa Saikolojia Changanuzi.* Tasnifu ya shahada ya uzamili. Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mohamed, S. A (2001) *Babu Alipofufuka.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Olali, T. (2008) *Mafamba.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

…………... "Structure and Anti- structure of Swahili Novel: A Stylistic Analysis of *Babu Alipofufuka"* katika The Nairobi Journal of Literature. Na. 6 ya mwaka 2010.

Polome, E. C. (1967) *Swahili Language Handbook.* U.S.A: Centre for Applied Linguistics.

Rice, P. na Waugh, P. (1996) *Modern Literary Theory: A reader.* USA: Arnold.

Richards, J. et al (1985) *A Dictionary of Applied Linguistics.* London: Longhorn.

Selden, R. (1995) *The Cambridge History ofLiterary Criticism: from formalism to Poststructuralism.* Great Britain: Cambridge University Press.

…………... (1988) *The Theory of Criticism fron Plato to the present*: A reader. AddisonWesley Longman Ltd.

Shaaban, R. (1951) *Kusadikika.* Nelson: London.

Shaw, H. (1972) *A Dictionary of Literary Terms*. NewYork: McGrawHill.

Timmamy, R. (2002) *Mombasa Swahili Women Wedding Songs: A stylistic Analysis*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. imechapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.

TUKI (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

............... (2006) *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili Toleo la Tatu*. Dar es Salaam.

Ullmann, S. (1964) *Language and Style*. Oxford: Basil Black well.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2001) *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.

.............. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

............... (2002) *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

............... (2003) *Kamusi ya fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

............... (2004) *Musaleo!* Nairobi: Vide~muwa Publishers.

............... (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Wales, K. (1989) *A Dictionary of stylistics*. London: Longman Group.